ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tano – Tarehe 3 April, 2012

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (*Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuja kuwasilisha Hati Mezani juu ya Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya 2009. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kuamka katika hali ya Afya njema. Lakini pia Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hati Mezani ya kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya Mwaka 2009. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 85

Uwiano Katika Nafasi za Ubalozi Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny Mhe. Hassan Hamad Omar) - Aliuliza

Baada ya malalamiko mengi kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kuhusu kutokuwepo kwa uwiano katika kushika nafasi za ubalozi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, kulikua na matarajio kua katika teuzi mpya za mabalozi kungekua na Wazanzibari wengi zaidi ili kupunguza tatizo hilo.

(a) Kwa hatua ya Rais wa Jamhuri ya Tanzania hivi karibuni kuteua mabalozi watatu tu kutoka Zanzibar kati ya mabalozi kumi walioteuliwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haioni kua hatua hiyo inaongeza ukubwa wa tatizo la kutokuwepo kwa uwiano katika nafasi za ubalozi kwa pande mbili za Jamhuri ya Muungano.

(b) Je, Serikali haioni kua hatua hiyo inaonesha kua wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaonekana kudharau malalamiko ya viongozi na Wazanzibari kwa ujumla.

(c) Kwa hivi sasa Tanzania ina mabalozi wangapi na maafisa wangapi waliopo katika balozi zetu nje za nchi, na kati ya mabalozi na maafisa hao, wangapi wanatoka Zanzibar.

(d) Wizara ya Mambo ya Nje ambayo ni taasisi ya Muungano ina jumla ya wafanyakazi wangapi na kati ya hao wangapi wanatoka Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika mkutano wa nne na mkutano wa sita wa Baraza la Wawakilishi wakati wa kipindi cha maswali na majibu nilijibu maswali Nam. 70 na 200 ambayo yamefanana kabisa na swali hili la Mhe. Hamad, hata hivyo pamoja na majibu hayo naomba tena kutoa majibu yafuatayo:-

(a) Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mamlaka ya Kikatiba kufanya uteuzi wa Mabalozi wa Tanzania. Uteuzi wa mabalozi uliofanyika ni sehemu tu ya kujaza nafasi zilizowazi za mabalozi. Ni mapema sana kusema kua hakuna jitihada zinazochukuliwa kwani bado kuna nafasi takribani 14 zinazotarajiwa kuwa wazi kutokana na mabalozi hao kutarajiwa kustaafu wakati wowote kuanzia sasa. Ni vyema tuvute subira tuone busara za Mhe. Rais.

(b) Mhe. Spika, si kweli kwamba kuna kupuuziwa kwa jambo hili. Serikali zote mbili zimekua zikifanya kazi kutatua changamoto hizi katika kuongeza wigo wa watumishi wa Zanzibari kufanya kazi katika Taasisi za Muungano ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambayo tayari imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Usaili wa Maafisa wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa uliofanyika hapa Zanzibar unawahusisha Wazanzibari peke yao. Njia hii hutoa fursa zaidi kwa Wazanzibari, kujiunga na utumishi wa mambo ya nje.

(ii) Wazanzibari 10 wenye shahada ya kwanza wamepelekwa chuo cha Diplomasia (CFR) kwa ajili ya kuandaliwa na kuajiriwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa mara watakapomaliza masomo yao.

(iii) Aidha Uteuzi wa Mhe. Ramadhan Muombwa ambaye ni Mzanzibari kuwa Balozi na Naibu Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa. Jambo ambalo ilikua ni kilio cha muda mrefu cha Zanzibar kutaka uwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

(c) Mhe. Spika, kuna mabalozi 32 kati yao mabalozi wanne wanatoka Zanzibar aidha kuna maofisa wa mambo ya Nje 35 kwenye Balozi zetu nje ya nchi, kati ya hao 10 tu ni Wazanzibari.

(d) Mhe. Spika, Wizara ina jumla ya watumishi 432 kati ya hao 40 ni Wazanzibari.

Mhe. Spika, jitihada za makusudi zimeanza kuchukuliwa ili kuwezesha vijana wengi kutoka Zanzibar kusomea masuala ya dipomasia ili zinapotokea nafasi za ajira mpya waweze kuajiriwa sambamba na wengine wanaotoka Tanzania Bara. Utaratibu huu utasaidia kupunguza pengo lililopo na kuleta uwiano unaotarajiwa. Lakini jambo la msingi ni kuwaandaa vijana wetu pamoja na kufanya bidii wao wenyewe katika masomo yao ili kukidhi vigezo na sifa katika soko la ajira.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Waziri amesema kwamba Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mara zote anakua akitumia busara katika kuteua nafasi kama hizi. Bila shaka tumekuwa tukipata nafasi mbali mbali za mabalozi.

(a) Naomba kumuuliza kwa kua hii ni nchi kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 2, suala hili la uteuzi wa mabalozi, linahitaji busara au ni haki kwa Zanzibar.

(b) Ametwambia kuna wafanyakazi 40 kati ya 432, hivyo kupatiwa kwa wafanyakazi 40 huoni kwamba kunatokana na kukosa kuwa Afisi ya Mambo Nje hapa Zanzibar. Je haiwi busara sasa kwamba Afisi ya Wizara ya Mambo ya Nje, Afisi ndogo ikawepo Zanzibar ili na Wazanzibari wakapata nafasi ya kuomba nafasi hizi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika suala langu la msingi kwamba Rais wa Jamuhuri ya Muungano ndiyo mweye haki kikatiba ya kuteua Mabalozi. Na kwa vyovyote vile katika kuteua kwake hushauriana na Rais mwenzake wa Zanzibar kwa wale wanaotokea Zanzibar. Ninachosema hapa ni busara kwa msingi kwamba hivi sasa kumetokea nafasi 10, katika hizo nafasi tatu wakachaguliwa Zanzibar.

Na kwa kua kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba kunatarajiwa kustaafu mabalozi wengine kama 14. Kwa hivyo nilikua naomba tuvute subirá, tuone busara za Rais kama ambavyo anavyoendelea kufanya wajibu wake

wa uteuzi. Kwa hivyo ni haki ya Zanzibar kupata mabalozi lakini pia ni mamlaka ya Kikatiba ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo. Hivyo kwa vyovyote vile busara zake zitahitajika katika ku tekeleza wajibu huo.

Mhe. Spika, suala la pili kuhusu nia ya kujenga Ofisi. Ni mtazamo wa Wizara yenyewe ya Mambo ya Nchi za Nje kujenga Afisi kubwa zaidi hapa Zanzibar. Hivi sasa tunayo Afisi ndogo ya Mambo ya Nchi za Nje lakini wanafikiria kujenga Afisi kubwa zaidi ya ile iliyopo.

Mhe. Spika, cha msingi hapa ni uwiano wa ajira, suala la msingi si kujenga Afisi, tunapendelea Afisi kujengwa lakini suala la msingi ni ile haki ya kujua asilimia yetu katika ajira na kiwango maalum kitakachotengwa. Utaratibu huo sasa utawekwa kisheria kwa taasisi zote za Muungano ili Zanzibar ipate haki yake iliyosawa ndani ya Jamuhuri ya Muungano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa kua Zanzibar ni Nchi na ni moja katika nchi zinazounda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Na kwa kua hakuna uwiano unaotambulika wa kuweza kuchukua nafasi zikiwemo hizo za kidiplomasia, tena ni nafasi nyeti kama zile za CDF na NGP.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba Wazanzibari wale wanaokataa Muungano wa sampuli iliyopo sasa wakiwamo uwamsho hawakufanya kosa.

(b) Kwa kua Mhe. Waziri amesema kwamba Wazanzibari waendelee kusoma ili waweze kuhodhi hizo nafasi za diplomasia. Na kwa kua tunao Wazanzibari tunaowatambua ambao ni *well qualified* katika mambo ya *International Relations or Conflicts Resolution* wapo katika vyuo vya kidiplomasia. Je, kwa kusema hivyo si kuwadharau vijana wetu wa Kizanzibari ambao wanayo taaluma hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza alisema kwa kuwa sasa ni nchi. Zanzibar ni nchi tokea asili si sasa, tokea mwanzo ni nchi. Kama nilivyosema ina haki yake kamili.

Mhe. Spika, tuliamua wenyewe kufanya Muungano na katika nchi yoyote ile duniani mnapofanya maamuzi mnayafanya na pale ambapo mnaona kuna kasoro mnarekebisha. Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo sasa suala la Muungano lipo Kikatiba na lipo Kisheria. Kwa hivyo ni haki ya kuheshimu Katiba na Sheria zilizopo. Hukatazwi kutoa maoni yako. Lakini cha msingi nafikiri utaratibu mzuri umekusudiwa kuwekwa kwa namna ambayo wananchi wangeweza kutoa mawazo yao. Utaratibu huo ni kupitia utaratibu wa Katiba mpya. Kila mmoja kuanza sasa kuenda mitaani na kufanya vurugu ya maneno kwa kila upande, inaweza kutuletea matatizo nchi yetu. Kwa sababu leo Uwamsho wanaweza kusema hili, kesho kinaweza kuzuka kikundi chengine kikasema vile.

Kwa hivyo kwa mujibu wa utaratibu vizuri ni kuyapanga haya mambo vizuri, tukatoa maoni yetu vizuri, mtu yeyote hakatazwi kutoa maoni yake, kwa sababu maoni ndio yatakayotusaidia kujenga nchi yetu. Kwa hivyo mimi nawaomba wale wote wasubiri karibuni hivi kutakua na utaratibu mzuri wa kutoa maoni vizuri na haki ya kila upande itapatikana.

Mhe. Spika, ningeomba kidogo arudie swali lake la (b)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Swali (b) Mhe. Spika, Mheshimiwa katika kujibu swali lake la msingi alisema kwamba SMT wanashindwa kuwapatia nafasi Wazanzibar kwa sababu taaluma hizi hawana yaani Wazanzibari waendelee kusoma kusudi Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano apate nafasi ya kuwateua kuwa mabalozi. Nasema kwamba Wazanzibari tayari wapo *well qualified* katika mambo ya *International Relations* au *Conflicts Resolution* na wapo wanasomesha katika vyuo vya diplomasia nje na ndani ya nchi hii.

Je, kwa kusema hivyo Mhe. Waziri si kuwadharau vijana wetu na kuwarudisha nyuma.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, mimi nafikiri kuwasisitiza wenzetu wasome si kudharau bali ni kujenga taifa zuri zaidi lenye maendeleo. Tunaposema watu wasome vizuri,

wajiendeleze, wapige hatua, sifikiri kama nitakua ninawadharau Wazanzibari zaidi ya kuwanasihi kwa ajili ya maslahi yao na maslahi ya nchi yetu.
Nilichosema hapa tutaendelea kuwasomesha, tutaendelea kutoa fursa na hivi sasa jitihada zinafanywa za kuchagua Wazanzibari wenye sifa ya kuwa mabalozi. Sijasema hata siku moja kwamba Wazanzibari hawapo ambao wana sifa. Wazanzibari wapo wengi wana sifa. Tunachokifanya ni kuzidi kuweka mkazo kwamba tuendelee kusoma ili tuweze kunawirika zaidi na kupata maendeleo zaidi katika nchi nchi yetu.

Nam. 140

Hatua Zilizochukuliwa Dhidi ya Waingizaji wa Mifuko ya Plastiki

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:

Baina ya tarehe 31/01/2011 na tarehe 3/2/2011 Askari wetu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) walikamata mashua 3 zikiwa na mifuko ya plastiki, jumla ya Bandal 714 ambayo hairuhusiwi kuingia nchini. Aidha, baada ya kukamata mifuko hiyo waliwakabidhi watu wa Idara ya Mazingira na Polisi.

(a) Je, kuna hatua gani zilizochukuliwa dhidi wa watu waliokamatwa wakidaiwa kuhusika na uingizaji huo na watu hao wako wapi.

(b) Je, mifuko iliyokamatwa iko wapi na imechukuliwa hatua zipi za kuangamizwa.

(c) Je, hatua gani zilichukuliwa kwa vyombo vilivyokamatwa na kudaiwa kuhusika katika kadhia hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 140 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo :-

Lakini kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo yafuatayo :-

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli siku ya tarehe 3/01/2011 Askari wa KMKM walifanikiwa kukamata mashua mbili zilizopakiwa mzigo wa mapolo 416 yakiwa na mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku kuingizwa hapa Zanzibar. Mashua hizo zilikamatwa eneo la Kisiwa cha Bawe, Wilaya ya Mjini zikiwa na jumla ya mabaharia 19.

Aidha siku ya tarehe 04/02/2011 Askari wa KMKM kwa mara nyengine tena walifanikiwa kukamata mashua moja iliyobeba mapolo 281 yakiwa na mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku kuingizwa Zanzibar. Mashua hiyo ilikamatwa eneo la Ras Shangani, Wilaya ya Mjini ikiwa na mabaharia 14.

Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako baada ya kutoa maelezo hayo naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

(a) Hatua zilizochukuliwa dhidi ya watu waliokamatwa wakidaiwa kuhusika na uingizaji huo ni kufunguliwa mashitaka katika vituo vya polisi na majalada ya upelelezi wa mashitaka hayo yalipelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua za Ofisi hiyo.

Hata hivyo, watuhumiwa wote waliachiwa huru kwa kua kosa la kuingiza mifuko ya plastiki hapa Zanzibar halikubainika kua lilitendeka.

(b) Mifuko yote iliyokamatwa ilikabidhiwa kwa watuhumiwa na Jeshi la Polisi kwa kua kosa la kuingiza mifuko hiyo halikufanyika.

(c) Hatua zilizochukuliwa kwa vyombo vilivyokamatwa ni kukabidhiwa kwa wenyewe kuendelea na safari zao kwa kua kosa halikuonekana kufanyika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi ya leo hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri suala la nyongeza.

Mhe. Waziri amekubali kwamba Kikosi cha KMKM wamekamata mifuko ambayo iliyoingizwa nchini kinyume cha sheria.

Je, Mhe. Waziri hao waliowakamata (Kikosi cha KMKM) amewapa tunza gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, Ofisi yangu ikiongozwa na mimi mwenyewe Waziri wa Nchi katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Ilifika katika Ofisi Kuu ya KMKM kwa ajili ya kupata mazungumzo ya pamoja na kuweza kuwapongeza ndugu zetu hawa ambao walifanikisha juhudi za kukamatwa mifuko hiyo.

Wenzetu walifurahi sana kwamba tulionesha imani kwao kwa kuweza kutekeleza sheria ambazo zimepangwa katika nchi yetu.

Nam. 163

Ujenzi wa Banda la Wavuvi Muyuni "B"

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabla ya yote kwa idhini yako na ruhusa yako naomba kumshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi alioufanya wa Baraza la Mawaziri hapo jana. Ukizingatia Mawaziri wetu wanapokwenda kuna kazi nzito kuliko huko wanapotokea kwa muda huu.

Mhe. Spika, wananchi wa Muyuni "B" kwa muda mrefu wamekua wakikabiliwa na tatizo la ukosefu wa banda katika shughuli zao za uvuvi (DIKO) na kuathiri shughuli zao, hasa wakati wa mvua.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo.

(b) Kwa kuzingatia kwamba wananchi kwa kushirikiana na Mwakilishi wao wameamua kuchangia baadhi ya gharama. Je, Serikali inaunga mkono vipi juhudi za wananchi.

(d) Gharama za ujenzi zinakaribia kufika Shs. 15, 000,000/=. Je, Serikali ipo tayari kuchangia kiasi gani baada ya wananchi na Mwakilishi kuonesha nia ya kweli ya kufanikisha mradi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 163 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kuondoa tatizo la banda kwa wavuvi wa Muyuni "B" kwa kufanya mpango wa kuwasaidia kuwajengea banda hilo.
b) Mhe. Spika, kwanza kabisa tunafuraha sana kusikia kwamba Mhe. Jaku Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Muyuni anawasaidia wapiga kura wake katika kuwapunguzia shida zinazowakabili wavuvi hao. Tunampongeza sana na kwa niaba ya Ofisi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunamuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nae ili kuhakikisha kwamba azma yake ya kuwaendeleza wavuvi wa jimbo la Muyuni inawezekana.

c) Serikali haitoweka mipaka katika kuwasaidia wananchi wake. Inasaidia katika kila nyanja kila inapowezekana na itaendelea kufanya hivyo kwa kiwango ambacho kitatolewa na Wizara kinategemea kiwango cha makusanyo yatakayopatikana na fursa nyengine zitakazojitokeza. Aidha kiwango ambacho

Mhe. Mwakilishi amekitoa kinathaminiwa sana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kwa mashirikiano na yeye bila ya kujali makundi kitatumika kusukuma mbele maendeleo ya wananchi wa jimbo la Muyuni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha nami nimepokea shukurani zako.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watu wanaochukua hatua za kuzorotesha ilani ya CCM ya kuwawekea mazingira magumu hasa kwa kuzingatia kwa sababu ya ubinafsi.

(b) Je, Serikali itatoa lini mchango wake wa kuendeleza mradi huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuhakikishia sana Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali haitawafumbia macho wapinga maendeleo na wanaozorotesha maendeleo ndani ya nchi yetu, sio tu wanaopinga ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini hata wale wanaopinga ilani ya Chama cha CUF, ambavyo vyama hivi viwili ndivyo vilivyounda Serikali ya nchi hii.

Lakini vile vile napenda nimuhakikishie kwamba hivi karibuni Wizara ya Mifugo na Uvuvi nafikiri baada ya kumaliza kipindi hichi cha Baraza itaonana na Mhe. Mwakilishi ili kuona ni kiasi gani kimebakia katika kukamilisha ujenzi wa banda hilo. Namuahidi kwamba banda hilo litamalizwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri mno ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kua si Chama cha Mapinduzi wala Chama cha Wananchi CUF kinachokusanya kodi katika diko lile la pale. Na kwa kua Halmashauri ya Wilaya ya kusini ndiyo inayokusanya mapato kwa wavuvi pamoja na wafanyabiashara katika diko lile. Je, Serikali ina mpango gani wa kuishawishi Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kutumia fedha za kodi zile kujenga hili banda na kumsaidia Mhe. Mwakilishi kumalizia jengo lile la banda la diko.
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli kwamba Halmashauri za Wilaya zinahusika katika kukusanya kodi kwa shughuli mbali mbali zinazofanyika ndani ya Wilaya hiyo. Lakini naomba kumuarifu Mhe. Saleh kwamba Halmashauri za Wilaya nazo zinakua na mipango yao na vipaumbele vyao vya jinsi gani vimejipangia katika mwaka ule kutekeleza shughuli zake za maendeleo ndani ya Wilaya. Si vibaya wakati wowote Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao kuchangia katika maendeleo haya. Kwa sababu juhudi za pamoja za Serikali za Wilaya pamoja na Serikali Kuu lakini vile vile juhudi za waheshimiwa Wawakilishi ndizo zitakazoleta maendeleo kwa pamoja.

Nam. 38

Ushukaji wa Thamani ya Shilingi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Kny Mhe. Rashid Seif Suleiman) - Aliuliza:

Baada ya kusherehekea miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika bado thamani ya shilingi inaendelea kuporomoka.

(a) Nini msimamo wa Serikali kuhusu athari ya kuporomoka kwa Shilingi ya Tanzania kwa Zanzibar.

(c) Kitu gani kinachochangia kushuka kwa thamani ya shilingi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa na idhini yako na kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi wa wananchi, lenye sehemu (a) na (b) naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, kuporomoka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunatokana na sababu nyingi. Naomba nizitaje baadhi ya sababu hizo, kama ifuatavyo:-

(i) Uzalishaji mdogo wa ndani ambao hauendani na mahitaji, hivyo kusababisha uagiziaji kutoka nje na hasa wa vyakula muhimu kua makubwa na kupelekea mahitaji ya fedha za kigeni kua makubwa.

(ii) Kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta duniani.

(iii) Kuchafuka kwa masoko ya fedha duniani kunakosababishwa hasa na matatizo ya kifedha yanayoendelea ndani ya Bara la Ulaya, kunapelekea thamani ya dola kuimarika dhidi ya sarafu nyengine duniani ikiwa ni pamoja na shilingi ya Tanzania.

(iv) Utegemezi mkubwa wa fedha zinazotoka kwa Wafadhili, hasa zile zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya kitaifa, zinapochelewa kunafanya mahitaji ya fedha za kigeni na hasa dola kua makubwa na hivyo kupelekea kushuka kwa thamani ya shilingi.

Mhe. Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunamuathiri sana mwananchi wa kawaida hasa kwa kutilia maanani kua bei za bidhaa mbali mbali na hasa vyakula pamoja na usafiri hupanda bila ya kujali vipato vya wananchi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, msimamo wa Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Zanzibar kuendelea kua ni Nchi ya amani na utulivu.
(ii) Kuendelea kua na sera nzuri za kuitangaza Zanzibar zitakazowavutia watalii zaidi. Kufanya hivyo, kutasaidia kupata fedha zaidi za kigeni.
(iii) Kuzalisha zaidi mazao ya vyakula pamoja na yale ya biashara kama karafuu, hiliki, pilipili n.k. kwa lengo la kupata fedha za kigeni.
(iv) Kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na wananchi kuanzisha mashamba ya samaki na majongoo ya baharini.
(v) Kuhakikisha vyakula vinavyozalishwa ndani haviuzwi nje ya nchi hadi pale tutakapokidhi soko la ndani.
(vi) Kupunguza viwango vya kodi kwa baadhi ya bidhaa muhimu hasa za vyakula.
(vii) Kupunguza manunuzi yasiyo ya lazima kwa bidhaa zinazotoka nje.

(b) Mhe. Spika, katika maelezo yangu ya awali, tayari nishaelezea baadhi ya sababu zinazochangia kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Namuomba Mhe. Mwakilishi akubali sababu hizo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kua athari ya kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania inachochea sana mfumko wa bei katika nchi yetu ya Zanzibar. Na kwa kua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina uwezo wa kudhibiti sera ya fedha. Je, Serikali yetu ina mpango gani kwa kushirikiana na Taasisi za Muungano kama vile BOT kuweza kudhibiti suala la athari hii.

b) Kwa kua matumizi ya ndani ya fedha ya Kimarekani ya dola inaathiri pia kuanguka kwa thamani ya shilingi yetu. Je, ni lini Serikali itakua na mpango wa kuzuia matumizi ya dola katika matumizi ya ndani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: (a) Mhe. Spika, kwanza nataka nimwambie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni m-bia wa BOT tunafanya kazi kwa karibu zaidi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na BOT katika masuala mazima ya Sera za Fedha.

(b) Mhe. Spika, matumizi ya dola sio halali, fedha halali ni shilingi ya Tanzania lakini Serikali zetu zote mbili zimeruhusu matumizi ya dola katika maeneo ya kitalii. Kwa mfano, mtalii anaweza akalipa kwa kutumia dola katika hoteli, lakini kulipa kwa kutumia dola kwa kununulia mchele na samaki si halali na hairuhusiwi kufanya hivyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri utakumbuka kipindi kilichopita cha bajeti ulisema kua Zanzibar imepanda uchumi wake kwa asilimia 6 na sasa hivi katika suala lako umesema kua kushuka kwa sarafu ya Tanzania kunatokana na uzalishaji.

Je, Mhe. Waziri ipi lugha sahihi ili wananchi wafahamu kwamba sasa hivi shilingi ya Tanzania imeporomoka.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli nilimueleza kwamba uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia 6, lakini haina uhusiano wa karibu wa kusema kwamba kukua kwa uchumi shilingi isishuke thamani. Shilingi ya Tanzania imeshuka thamani kutokana na sababu nilizozieleza, moja nimesema kwamba uzalishaji wetu ni mdogo kwa maana ya kwamba bidhaa ambazo tunazouza nje ni kidogo kuliko zile ambazo tunazoziagiza ndani. Hivyo, kumefanya mahitaji ya fedha za kigeni kua ni makubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuniona hatimae, hivyo naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni m-bia kwa BOT. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha BOT ya 1966 na hata ya hivi karibuni ya 1997, Zanzibar haitambuliwi kama ni m-bia katika BOT.

b) Mhe. Spika, kwa sababu hoja nyingi alizozielezea zilizopelekea kuporomoka kwa thamani ya shilingi zinahusu zaidi upande wa Tanganyika na ushahidi wa hayo ni kwamba nyingi katika athari kubwa za kimataifa ni kuzikumba chumi ndogo za visiwa kwa mfano Syschelles, Mouritius na hata ndugu zetu wa karibu wa Comoro. Mhe. Waziri haoni kwamba kuendelea kutumia thamani hii kutatuathiri na hivyo sasa wakati umefika wa Zanzibar kutumia historia yake ya kua nchi ya mwanzo kuanzisha sarafu yake katika eneo la ukanda wa Afrika Mashariki na Kati pamoja na Kusini kuendesha sarafu yake ambayo itasimamia vyema uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni m-bia katika BOT na kuthibitisha hili Serikali kila mwaka tunapata gawio ya faida iliyotokana na BOT. Huwezi ukapata gawio kama wewe sio m-bia.

Mhe. Spika, kuanzisha kwa sarafu yake Zanzibar mimi namuomba Mhe. Mwakilishi asubiri mchakato wa katiba utakapokua tayari basi achangie huko kama Watanzania au Wazanzibari wakikubaliana kwamba tuanzishe sarafu yetu, basi katiba mpya itasema kwamba tuanzishe sarafu yetu hivyo tutaanzisha sarafu yetu.

Nam. 86

Tofauti ya Maslahi Baina ya Watendaji wa Serikali

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilichukua hatua muhimu ya kurekebisha mishahara ya watendaji wake;

(a) Kwa hivi sasa kima cha juu kabisa cha mshahara anacholipwa mtendaji wa Serikali ni kiasi gani.
(b) Ni kwa namna gani marekebisho hayo yamewafaidisha watendaji wa sekta ya afya wakiwemo madaktari na madaktari bingwa pamoja na wauguzi.

(c) Ni vigezo gani vilitumika katika kutofautisha mishahara ya watendaji kwa mfano baina ya daktari bingwa mwenye shahada ya uzamivu (*Ph.D*) na hakimu wa Wilaya mwenye stashahada (Diploma).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa mishahara, Serikali inaweka kima cha chini cha mshahara na haiweki kima cha juu cha mshahara, bali inaweka ngazi za kupanda kwa mujibu wa ngazi za mishahara au cheo cha mfanyakazi.

(b) Kwa ngazi za mishahara za SMZ zinategemea elimu ya mfanyakazi. Kada ya afya ndio yenye malipo makubwa zaidi ukilinganisha na kada nyengine zote za watumishi wa umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(c) Madaktari wenye elimu inayolingana kwa mfano wenye *Ph.D* wote hawalipwi mshahara wa aina moja, inategemea ameipata lini na ameanza kazi lini. Mishahara mingi ya Mahakimu na Majaji ni "*fixed*" haina nyongeza ya kila mwaka na haitegemei sana kiwango cha elimu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kua nakumbuka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara moja iliwahi kutoa *circular* kwamba hata waajiri binafsi wazingatie kiwango cha chini cha waajiriwa wa Serikali na wao watumie hicho.

Je, Mhe. Waziri anajua kama kuna waajiri binafsi sasa hivi hawafuati agizo hilo la Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi, na Waziri anayehusika na ajira ndiye aliyetangaza kima hicho kwa niaba ya Serikali. Lakini ofisi yangu sina taarifa kwamba wapo baadhi ya waajiri hawajatekeleza hilo. Mhe. Spika, kwa kua Mhe. Mwakilishi ameuliza suala hilo hapa naomba awe mstahamilivu ili ofisi yangu iwasiliane na Wizara inayohusika na masuala ya ajira ili tuweze kumpatia jibu sahihi kama wapo ambao wanalipa na wapo ambao hawajatekeleza toleo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi amesema hivi karibuni Serikali ilichukua hatua muhimu ya kurekebisha mishahara kwa watendaji wake. Mhe. Spika, kuna sababu zipi hadi hii leo Shirika la Bandari wasizidishiwe mishahara hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwaka huu wa fedha imefanya marekebisho ya mishahara ya watumishi wote wa umma. Ni sababu zipi zilizosababisha watumishi wa Shirika la Bandari wasirekebishiwe mishahara yao.

Mhe. Spika, hiyo inatokana na kwamba Shirika la Bandari ni Shirika ambalo linajitegemea na linajiendesha kibiashara, na mishahara yao hutolewa kwa mujibu wa bajeti wanayoipanga au wanayoitoa Bodi ya Shirika la Bandari. Na kwa vile Shirika la Bandari mishahara yao au mwaka wao wa fedha huanzia mwezi wa Januari, na mwaka wa fedha kwa watumishi wote wa Serikali huanzia mwezi wa Julai. Mhe. Spika, wakati Serikali inafanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma, wao tayari Shirika la Bandari walishafanyiwa marekebisho ya mishahara yao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri ulipojibu hapa katika jibu lako mama ulisema mishahara ya Mahakimu hutegemea sana elimu ya mtu. Je, Mhe. Waziri kwa nini Mahakimu wa Mkoa wanapata pesa nyingi na Mahakimu wa Wilaya wanapata pesa kidogo, ni kigezo gani ambacho mmekitumia.

c) Kuna sehemu ambazo Wizara ya Afya ukianzia katika sehemu ya ufundi na makarani na sehemu nyengine mpaka leo hii hiyo nyongeza ambayo iliyotolewa na Serikali utakubaliana na mimi kama hawajaipata.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nilipokua nikijibu suala la msingi nilisema Mahakimu hulipwa mshahara kwa mujibu wa nafasi zao, ni kwa nini Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mikoa wanapata tofauti ya mishahara.
Mhe. Spika, ni kwamba unaposema Mkoa na Wilaya kuna tofauti, Mkoa ni ngazi kubwa na Wilaya ni ngazi ndogo. Hicho ndio kigezo ambacho kimetumika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mishahara ya Wizara ya Afya kwa nini kuna baadhi ya wafanyakazi wa vitengo vyengine hawajarekebishiwa mishahara yao, hilo mimi sikubaliani nalo kwa sababu ofisi yangu mpaka sasa hatujapokea malalamiko yanayohusiana na suala hilo. Mhe. Spika, kama nilivyosema katika vikao huko nyuma kwenye Baraza hili la Wawakilishi kwamba Wizara yangu ilitoa toleo maalum linalohusiana na marekebisho ya mishahara kupitia ngazi mbali mbali kwa mujibu wa taaluma na kazi watu wanazozifanya.

Mhe. Spika, pia kuna programu maalum ambayo tumeipeleka kwenye Wizara zote ili kuhakikisha kila mfanyakazi analipwa mshahara anaostahiki kulipwa. Kwa hivyo, kama wapo wafanyakazi mpaka leo ambao hawajarekebishiwa mishahara yao Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi ashirikiane na hao wafanyakazi ili waje wafuate taratibu zinazohusika wende Wizarani kwao na Wizara yangu itakapopata barua kwamba kuna watu hao hawajarekebishiwa mishara basi hatua za marekebisho zitafanyika mara moja.

Nam. 58

Kuzorota kwa Shirika la Umeme

Mhe. Hija Hassan Hija:

(Mheshimiwa aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 12

Mewata na Saratani

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: (Kny: Mhe. Mohammed Said Mohammed) - Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano (SMT) kupitia Wizara ya Afya na Jumuiya ya Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) imefanya kazi kubwa ya kuwachunguza akinamama wenye matatizo ya matiti ili kubaini dalili za ugonjwa wa saratani mapema.

(a) Je, mara ngapi madaktari wa MEWATA wametembelea Zanzibar kwa madhumuni ya kuchunguza dalili za saratani ya matiti hapa Zanzibar.

(b) Kama wametembelea na kuwachunguza wanawake wa Zanzibar, ni wangapi wamekutwa na matatizo ya saratani.

(c) Je, Serikali inafanya juhudi gani hapa Zanzibar kuwafanyia uchunguzi wanaume wenye umri mkubwa ili kubaini kama wamepata saratani ya kongosho dume ili kupatiwa matibabu mapema.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Madaktari wa MEWATA hawajawahi kutembelea Zanzibar kwa madhumuni ya kuchunguza dalili za saratani ya matiti hapa Zanzibar.

(b) Uchunguzi wa saratani ya matiti ulifanyika mara moja kwa ushirikiano wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Agakhan Hospital ambapo wanawake 1,000 walijitokeza kupima afya zao.

(c) Kati ya hao 4 walikua na dalili za *cancer* wakafanyiwa vipimo na upasuaji, na 6 walikua na *cancer* iliyokua imefika hatua kubwa na baadae wote walipewa rufaa na kupelekwa Ocean Road.

(d) Ni kweli kila mwanamme mwenye umri unaofikia miaka 40 na kuendelea anatakiwa afanyiwe uchunguzi wa kongosho dume angalau mara moja kwa mwaka. Neno kongosho si la kawaida linahusiana na mfumo

wa kwenda haja ndogo. Kwa hapa kwetu Zanzibar hakuna utaratibu maalum wa kuwachunguza wanaume kwa hiari yao, isipokua wale wanaokuja hospitali kwa matatizo ya kuziba njia ya mkojo ndio wanaopimwa kongosho dume na kwa sababu tu ni moja ya maradhi yanayofanya wanaume washindwe kupata haja ndogo. Si aghlabu, wanaume kukubali kupimwa kongosho kabla ya tatizo la kuziba mkojo halijajitokeza, na likijitokeza anapima kwa takhlifu kubwa na ni kwa sababu tu hana jinsi ya kufanya. Kinachowafanya wanaume kutopenda kupimwa kama haumwi ni aina ya kipimo chenyewe kinavofanyika.

Kwani vipimo vyovyote vya kidaktari, ili apate uhakika wa jambo ni lazima vianzie na mkono kwa kugusa sehemu husika. Baadae vipimo vya maabara na kufuatiwa na vipimo vyenginevyo vya kutumia vyombo maalum vya aina ya *x-ray*. Mhe. Spika, kipimo cha kongosho kinahitaji kupitia kwenye njia ya haja kubwa kwa sababu ndiko kongosho liliko. Mhe. Spika, wanaume wengi wakiambiwa hukimbia na kurudi kwa daktari pale tu hali inapokua mbaya. Pindipo mwanamme akikubali kupimwa mapema au kuchunguzwa kila mwaka anaweza kugunduliwa tatizo mapema, kutibiwa na hatimae akapona kabisa na pindipo akikataa tatizo hukuwa na mara nyingi huishia kuwa saratani ya kongosho kwa sababu ya mabadiliko yanayotokea ndani yake.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kua Mhe. Waziri amesema kwamba wanaume wanaofikia umri kuanzia miaka 40 mara nyingi ndio wanaopata saratani ya kongosho dume.

a) Je, Mhe. Waziri matatizo haya yanasababishwa na nini.

b) Mhe. Waziri katika jibu lako la msingi umesema kwamba wanaume wengi huwa wanaogopa kuangaliwa hii saratani ya kongosho kutokana na vipimo vyenyewe. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja sasa ya kuhamasisha katika vyombo mbali mbali vya habari ili hao wanaume wetu ambao wanaogopa kupima waweze kuja na wajitokeze kwa wingi kupima afya zao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni ukweli kwamba mimi sio daktari, lakini moja katika sababu ambayo nimeelezwa ni kwamba ile njia ya kupitia haja ndogo kila ukiwa mtu mzima lile kongosho hua linavimba na kila likivimba hua nguvu inapunguka ya kwenda haja ndogo. Mhe. Spika, ukitaka kujua hivyo mtizame mtoto mdogo anapokwenda haja mkojo wake ulivyokua na nguvu kubwa na wewe leo ukenda haja jitizame wako umepungua nguvu. Mhe. Spika, hiyo ndio moja katika dalili zake.

Mhe. Spika, hili ni suala la msingi na tunalipokea tutaendelea kuhamasisha wananchi. Lakini nakumbuka juzi kwenye mkutano wa *briefing* nilisema kwamba moja katika tatizo la jamii yetu ni kwamba tunaogopa kupima vipimo vyetu kabla hatujaugua. Juzi nikaambiwa niwalete madaktari, madaktari nimeshawaeleza na wamefurahi kweli na walisema badala ya kuja wakapima tu, pia wangepata na nafasi wakapewa angalau semina ya umuhimu wa kupima.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi alisema kama ni mara moja tu waliokuja madaktari hapa kwa kuja kuangalia saratani za matiti. Je, katika Wizara yako una mpango gani wa kujipanga vizuri ili ukaja ukaangalia tena afya hizi za kina mama kuhusu saratani ya matiti kwani ni tatizo sugu ndani ya nchi yetu.
Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kuna mipango ya aina mbili, moja ni kushirikiana na wenzetu kuja wakapima kina mama, hilo liko katika mfumo wa utekelezaji kazi. Lakini pili, tunategemea kua na kitengo maalum hapa Zanzibar ambacho kitachukua na kitashughulikia matatizo ya saratani muda wote. Kitengo hicho kinategemea kuwepo baada ya kumaliza ule mradi tuliouita wa *Orio* ambao utajenga lile jengo lilokua zamani la Kiwanda cha Madawa.

Mhe. Spika, lakini kwa taarifa tu kwamba hivi sasa kwa upande wa wanaume tayari tumepata msaada mdogo kutoka Serikali ya Misri katika kuwasaidia wale ambao wana matatizo ya mikojo. Kwa hivyo, mpango upo na utakapokua tayari tutawaeleza kina mama ili waweze kuja hapo tutakapowapata madaktari wenzetu kutoka Bara wakiwa tayari.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kua suala hili la maradhi ya wanaume ya kongosho, hili ni jina jipya na wananchi wengi hawalijui kongosho ni nini. Kwa faida ya wananchi wetu pamoja na Baraza lako naomba Mhe. Waziri atueleze zaidi ili tupate kufahamu kongosho ni nini.

Pili, chanzo cha maradhi haya ya kongosho dalili zake zinakuwa ni zipi?

Mhe.Waziri wa Afya: Mhe.Spika, nadhani Mhe. Amina Iddi aliuliza na nikaeleza kwa ufupi sababu moja ya dalili hizo ni kwanza umri, ukizidi miaka 40 mfumo wa kwenda haja ndogo unakuwa unaanza kuchoka na ile *system* ambayo iko inayosukuma mkojo katika mfumo ule wa kwenda haja ndogo huwa unavimba na kila ukivimba unapunguza zile nguvu za kusukuma mkojo nje.

Nimeeleza hapa kwamba dalili moja mtizame mtoto mdogo anavyokwenda haja mkojo wake unavyo nguvu zaidi kuliko wa kwako wewe mtu mzima. Narudia, ukiuona sasa haufiki kule, unakuja karibu ya miguu yako, basi ujue hali hiyo ni mbaya na uje tukutizame kongosho lako.

Sasa kongosho ni neno ambalo limetafsiriwa kwa Kiswahili linaitwa *prostate* na kwenye mfumo wa haja ndogo kuna mahali imewekwa hiyo na umbile la mwili kwamba hii iwe ndio sehemu inayosaidia kusukuma mkojo, ukiona dalili hizo matatizo yameanza. Sasa hakuna maelezo mengine isipokuwa niseme ni kongosho tu.

Nam. 101

Umiliki wa Duka la Vioo Darajani

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Wazanzibari wamekuwa wakilalamika juu ya uuzaji au ukodishaji wa mali za Serikali kinyume na utaratibu. Eneo la Darajani ipo nyumba (maarufu duka la vioo) ambayo inasemekana kuwa ni mali ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo wananchi hawajui hatima yake.

(a) Je, ni kweli jengo hilo ni mali ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

(b) Zipo taarifa kuwa jengo hilo limekodishwa kwa Kampuni ya Simu za Mikononi Vodacom. Je, taarifa hiyo ni kweli.

(c) Kama imekodishwa kwa Vodacom, Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapata kiasi gani kwa mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 101 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa kuanza na utangulizi ufuatao:-

Mhe.Spika, kwa taarifa zilizopo wizarani ni kwamba hakuna mali ya serikali au wizara iliyouzwa au kukodishwa kwa watu binafsi au kampuni bila ya kufuata utaratibu uliowekwa. Serikali ilifanya mageuzi ya kisera katika uendeshaji na usimamizi wa uchumi kwa kushirikisha sekta binafsi katikati ya miaka ya 1980.

Kwa hatua hiyo serikali iliondokana na Sera za Uchumi za uhodhi na kushughulikia zaidi na majukumu yake ya msingi ya ulinzi na usalama, usimamizi na uendelezaji wa miundombinu. Hatua hiyo ilisababisha kuziondoa baadhi ya mali zilizokuwa zinamilikiwa na serikali kwa njia ya kuziuza au kuzikodisha kwa sekta binafsi.

a) Ni kweli Mhe. Spika, jengo lililoko Darajani kwa umaarufu linaitwa Duka la vioo ni mali ya serikali chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

b) Taarifa hiyo Mhe. Spika, ni kweli kwamba jengo hilo limekodishwa kwa Kampuni ya simu ya mkononi yaani *Vodacom.*

c) Mhe. Spika, kutokana na ukodishwaji huo kwa Kampuni hiyo ya *Vodacom* Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata **US$ 1,100.00** kwa mwezi sawa na **US$ 13,200.00** kwa mwaka.

Mhe.Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, amekiri kwamba jengo hilo ni mali ya serikali chini ya wizara yake na kwamba limekodishwa kwa US$ 1,100.00 kwa mwezi. Kwa sababu limekodishwa je, anakusudia kunambia kwamba mkataba wa ukodishwaji jengo hili uko chini ya ofisi yake au ofisi ya Wizara ya Fedha. Na kama upo mkataba, wajumbe wako wakihitaji kuuona wanaweza kuuona.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni Wizara ya Biashara ndiyo iliyoingiana mkataba na Kampuni hii ya *Vodacom*. Mkataba huo Mhe. Spika, kama anataka kuuona Mhe. Hija afike wizarani na tutamuonesha.

Nam. 46

Tatizo la *Feeder Roads*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Kny: Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:

Njia ya Mgagadu ikiwa pamoja na njia zake za ndani (feeder roads) za Jimbo la Ziwani zinakatisha tamaa kwa uchakavu. Ili kuondoa tatizo hilo ni lini njia hizo zitajengwa. Wizara ina mkakati gani kupunguza kero hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Nam. 46 la Mhe. Rashid Seif Suleiman kama ifuatavyo. Kuhusu barabara ya Mgagadu/Kiwani. Mhe. Spika, barabara hii ina urefu wa kilomita saba na imetengewa shilingi mia tatu milioni katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Ujenzi wa barabara hii umeshaanza na unaendelea vizuri. Kuhusu njia za ndani (*feeder roads*) katika Jimbo la Ziwani, Mhe. Spika, hivi sasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeweka kipaumbele na hii ni kwa mujibu wa Zanzibar *Transport Master Plan.*

Kwa ujenzi wa barabara kuu kwa maana ya *Regional and District Roads* kama vile barabara sita za Mkoa wa Kusini Pemba ambazo zimeshafunguliwa katika Sherehe za Mapinduzi, barabara hiyo ya Mgagadu/Kiwani, zile zinazojengwa na *MECCO* Mfenesini/Bumbwini, Amani/Dunga, Wete/Gando, Wete/Konde, barabara sita zinazoendelea kujengwa sasa hivi chini ya mradi wa *MCC* na kama hizo. Huo ndio mkakati.

Kwa barabara za ndani kwa Jimbo la Ziwani kama vile Gombani/Kichuani, Mchanga wa Kwale/Pembeni, Huesa/Ndagoni mpaka Mkumbuu, hiyo ni mifano. Baraba hizo hatuna mpango maalum wa kuzijenga, kinachotokea ni kwamba zinajengwa kwa dharura ili zipitike wakati wa mvua na mara nyingi hakuna bajeti yake isipokuwa bajeti iliyopo ama ni Mwakilishi, Mbunge ama Mfadhili kusaidia mafuta kwa Wizara ya Miundombinu kwa sababu wizara hii ina gari, vifaa na vitu kama kifusi vinapatikana kirahisi. Kwa hivyo, ni pale ambapo utatoka msaada kwa kupitia *source* nyengine isiyokuwa ya bajeti ambayo haikupangwa ndivyo barabara hizo zinafanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, naomba kusema hayo katika swali hili la Mheshimiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza kwamba, kwa kuwa *feeder roads* za Ziwani ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya wananchi. Kwa sababu Ndagoni/Wesha ni barabara muhimu sana katika kutoa dagaa kule mpaka pale Wesha, Kichuwani Gomani ni muhimu sana kwa sababu zinapatikana kombe na kwa sababu wataalamu wa afya wanatueleza umuhimu wa vyakula vya bahari katika kujenga afya ya mwanadamu.

Je, haoni Mhe. Waziri kuendelea kuzidharau *feeder roads* hizo za Jimbo la Ziwani ni kudhalilisha afya za wananchi ambazo ni nguvu kazi kwa maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza niweke wazi kwamba hatuendelei kuzidharau wala hatuzidharau. Nimeeleza wizara hii inafanya kazi kwa mujibu wa bajeti iliyopangiwa, tuna mpango maalum na bila ya mpango huwezi kufanya kitu, na ni vizuri kufanya kitu kimalizike ndio ufanye kingine, sio

kwamba kingine usikifanye. Nilieleza vizuri sana kwamba kwa barabara zile ambazo haziko kwenye bajeti, bajeti yake Wabunge, Wawakilishi, wafadhili na hata wakati mwengine serikali yenyewe.

Kwa mfano, katika uvunaji wa karafuu *ZSTC* wamechangia zaidi ya shilingi milioni thalathini kwa ajili ya mafuta kwa barabara zile ambazo kuna karafuu nyingi ili gari ziende kuchukua karafuu.

Sasa hatuzidharau lakini ni mpango huwezi ukajenga *feeder roads* wakati hii *road* kubwa hujaijenga, hiyo *feeder road* haitakuwa na maana yoyote. Kwa hivyo hakuna dharau katika hili ni utaratibu ambao umewekwa, na bila ya utaratibu hatuwezi kwenda hivi hivi tu, lazima tufuate utaratibu ambao serikali imejiwekea.

Nam. 28

Kuingizwa Mtaala wa Uvuvi katika Elimu
ya Msingi na Sekondari

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Kwa kuzingatia kuwa dhamira kubwa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuwapa elimu wananchi wake ni kuwajengea misingi bora ili waweze kujikwamua kimaisha kwa kutumia rasilimali walizonazo.

(a) Ni kwanini hadi leo Serikali haijaingiza katika mtaala wa elimu hasa katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari masomo yanayohusiana na uvuvi ili kuwapa mbinu za uvuvi wa kisasa vijana wa kizanzibari hasa walio katika visiwa kama Kojani.

(b) Ni lini Serikali itaingiza masomo ya uvuvi katika mitaala ya elimu ili angalau wahitimu wa elimu ya sekondari hata wanaposhindwa kuendelea na elimu ya juu zaidi, wawe na taaluma ya kuweza kutumia rasilimali ya bahari iliyowazunguka ili kujiongezea kipata zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Nakushukuru sana Mhe. Spika, na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza, napenda kutoa maelezo ya Utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwapa elimu wananchi wake, ni kuwapatia ujuzi wa maarifa yatakayowasaidia kujikwamua kimaisha kwa kutumia rasilimali zilizopo nchini. Miongoni mwa rasilimali zetu ni bahari, na ardhi kwa ajili ya kilimo. Katika miaka ya 80, masomo ya kilimo na uvuvi yalikuwa yanafundishwa katika Skuli za Sekondari za Fidel Castro na Skuli ya Lumumba. Hata hivyo, masomo hayo baadae yalisitishwa kutokana na kufundishwa zaidi kinadharia kuliko vitendo kutokana na ukosefu wa zana muhimu za kufundishia, na hatimae faida iliyotarajiwa kupatikana kwa kuwaandaa wakulima na wavuvi kutopatikana.

Baada ya maelezo hayo Mhe.Spika, naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi inakusudia kujenga tena Chuo cha Uvuvi. Wizara inakusudia kufanya utafiti wa kina juu ya namna gani ya somo la uvuvi wa kisasa linaweza kuanzishwa katika skuli zetu na mahitaji ya zana zinazohitajika. Utafiti huo utatusaidia kuepuka makosa yaliyofanyika katika kipindi cha nyuma ambapo somo hili lilifundishwa zaidi kinadharia badala ya vitendo, na baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na mchepuo huo hawakupendelea kufanya hivyo.

b) Mhe. Spika, wizara itaanzisha somo hilo mara tu baada ya maandalizi yote yatakapokamilika, ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa mitaala, kupatikana kwa walimu wenye ujuzi, vifaa vya kufundishia na skuli mahsusi ya kuanzishia somo hilo. Wizara itajitahidi kuepuka kuanzishwa katika skuli zetu somo hilo bila ya maandalizi.

Mhe.Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe.Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe.Naibu waziri namshukuru kukiri kwamba somo hilo lilikuwepo kabla, lakini lilisimama kutokana na kukosa vitendea kazi vya kusomea somo hilo kwa vitendo.

Je, serikali imeshajipanga vizuri kuleta vitendea kazi vya somo hilo, au linaletwa kwa majaribio tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu mama kuwa, wizara itajitahidi sana kutofanya makosa ambayo ilifanya kipindi cha nyuma. Jambo la kwanza ambalo wizara tunaendelea nalo hivi sasa ni utafiti.

Mhe. Spika, kuna matatizo ambayo yalijitokeza kwa mfano, wanafunzi ambao tulikuwa tukiwachagua kipindi kile ni wale wanafunzi waliokuwa wakitoka katika michepuo, tunawapeleka katika skuli zetu hizo za Fiedel Castro na skuli nyengine ambazo tulikuwa tunazipangia, matokeo yake mwanafunzi akimaliza *Form VI* kumbe kichwani mwake hakuwa na mawazo kuwa yeye aende katika kada ya uvuvi au kilimo, wanafunzi hao walikuwa wakituacha mkono na hususan katika somo la uvuvi. Tulifanikiwa kidogo wataalamu kwa kwenye kilimo lakini kwenye uvuvi wanafunzi wengi walituacha mkono, na ndipo tuliposema pale kwamba, lazima tujipange kwanza wizara kwa kufanya utafiti juu ya namna gani masomo hayo tunaweza tukayaendesha. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini atakubaliana na mimi moja ya wanafunzi kuacha mkono ni kwa sababu hizo shughuli za uvuvi katika nchi yetu hazijaimarishwa.

Pili je, kwa kuwa Zanzibar ni kisiwa na kama ni kisiwa basi kimezungukwa na bahari, na serikali ina mpango wa kuelekea katika uvuvi wa Bahari Kuu, Haoni kama kuna haja ya kurejesha tena somo hili ili wananchi tukiingia katika hiyo awamu ya Uvuvi wa Bahari Kuu, iwe tayari wana ujuzi wa kutegemea na waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, haja ya kurudisha somo la uvuvi serikali inaona kuwa haja ipo, na ndio maana nikajibu kwenye jibu langu la msingikuwa haja ya kufanya hivyo ipo, na serikali inajipanga na tukishakuwa tayari Mhe. Spika, somo hilo litaanzishwa.

Lakini kwa taarifa tu Mhe. Spika, Chuo chetu Kikuu cha Zanzibar (*SUZA*) kinatarajia kuanzisha chuo kingine kule Pemba na kiwanja tayari tushapata sehemu za Mchangamdogo. Sasa chuo hiki kinafikiriwa kwa siku za mbele Mhe. Spika, kuanzisha pale skuli ya kilito. Skuli hii itakwenda sambamba na mifugo na uvuvi. Kwa hivyo, serikali imeliona hilo na namuomba Mhe. Subeit Khamis awe na subira na mambo mazuri hayahitaji haraka, tumo tunajitayarisha ili tukianza basi tusifanye makosa.

Nam. 88

Kurejeshwa Ligi ya Muungano

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kulifanyika mashindano ya *Mapinduzi Cup* yaliyoshirikisha Timu za Tanzania Bara na Zanzibar, na mashindano hayo kuleta msisimko mkubwa katika kushajihisha Sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu, na pia kuonesha kuwa mchezo wa Mpira wa Miguu bado unapendwa sana hapa Zanzibar.

Je, Wizara haioni kwamba sasa ipo haja ya kushirikiana na Wizara ya Michezo Tanzania Bara pamoja na vyama husika kurejesha mashindano ya Ligi ya Muungano ya Mpira wa Miguu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, ni kweli mashindano ya *Mapinduzi Cup* yalishirikisha timu za Tanzania Bara na Zanzibar, yalileta msisimko mkubwa na kuonesha kwamba mchezo wa mpira wa miguu bado unapendwa sana Zanzibar. Hata hivyo, kurejesha mashindano ya Ligi ya Muungano ya mpira wa miguu kuna athari zake. Athari kubwa ni timu zetu kutoweza kushiriki kama wawakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya *CAF*, kwani mashindano ya ligi ya nchi ndiyo yanayotoa wawakilishi wa nchi hizo katika michuano ya *CAF*.

Lakini kutokana na faida iliyopo ya timu zetu kupata uzoefu, ujuzi na kuongeza maarifa zinapambana na timu za Tanzania Bara, wizara inaona ipo haja kuandaliwa mashindano yatakayozikutanisha timu za pande hizo mbili. Hivyo kwa kutumia vikao vya mashirikiano tunapendekeza yawepo mashindano mengine zaidi ya *Mapinduzi Cup*.

Mhe.Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Spika, katika kudumisha Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar, michezo ni moja kati ya kuunganisha wananchi wa Tanganyika na Zanzibar. Je, haoni kwamba mbali na mchezo huu wa mpira wa miguu wizara kufanya mashindano mbali mbali katika kudumisha Muungano wetu kwa kupitia michezo ya mpira wa miguu, *net ball* pamoja na michezo mingine ya riadha.

Mhe.Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nashukuru Mhe. Spika, ni kweli kuna umuhimu mkubwa sana wa kuleta mashirikiano, lakini napenda kumjuilisha mjumbe tu kwamba, mara hii hatukufanya Kombe la Mapinduzi yaani kujumuisha mchezo wa mpira peke yake, lakini vile vile tumejumuisha na mchezo wa *netball.*

Hivi sasa tuna mpango wa kupanua wigo zaidi isiwe Tanzania peke yake lakini ziwe nchi za Afrika Mashariki na Kati vile vile. Kwa sababu tunaona kwamba kuna faida kubwa na kwa kweli imejenga mahusiano mazuri, na vile vile tumepata hamasa kubwa ya kunyanyua vipaji vyetu. Kwa hivyo, Mhe.Mjumbe kuwa na subira tunapanua wigo zaidi kwa *netball* na kwa michezo mingine zaidi mbali ya *football*, *netball* na michezo mingine vile vile kwa Afrika Mashariki na Kati. Ahsante sana.

Mhe.Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe.Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaashiria kwamba tutakuwa na mashirikiano ya kutosha katika mchezo huu wa mpira wa miguu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.Lakini katika mashindano haya ambayo Mhe. Mwakilishi kauliza swali, Chama kinachosimamia Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kimepinga kitendo cha wizara kuunda kamati ya kusimamia mashindano ya *Mapinduzi Cup* wakati chama kinachohusika na mchezo huo kipo.

Je, Mhe.Waziri serikali inatoa msimamo gani juu ya malalamiko hayo ya *ZFA*.
Mhe.Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba chama kinachosimamia ni Chama cha *ZFA*, lakini ni juzi tu, tumekaa pamoja na *ZFA* pamoja na wadau wa michezo yote ili kujaribu ku-*harmonize* yale matatizo yaliyopo hivi sasa, na kwa kweli tumefikia pahala pazuri.

Namhakikishia Mhe.Mjumbe kwamba ni karibuni tu hapa tutapata ufumbuzi mwengine mpya kabisa. Kwa sababu kwanza katika utaratibu wa kubadilisha ile katiba ya *ZFA* ili kupunguza ile migogoro.

Tumejaribu kukutana na wadau pamoja na *Mapinduzi Cup* pamoja na wale wachezaji wa zamani ili kutafuta njia mbadala nini cha kufanya ili tuhakikishe kwamba hakuna migogoro na mambo yetu yanakwenda vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi usiwe na wasiwasi tumefikia pahala pazuri sana.

Nam. 165

Mahabusu za Watoto

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Baraza la Wawakilishi mwezi Machi mwaka jana lilipitisha Sheria ya Kulinda Haki za Watoto.

(a) Kwanini Mahakama za Watoto Mahabusu hazijaanzishwa hadi sasa, na kusababisha watoto wenye umri mdogo kuendelea kusota gerezani kutokana na kesi zao kutosikilizwa kwa muda muafaka.

(a) Kwa kuwa serikali inazingatia haki za watoto, inakuwaje mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18 awekwe rumande kwa muda mrefu kwa kesi ya nazi 30 na kumnyima haki ya masomo na malezi ya wazazi wake.

(b) Serikali inatumia vigezo gani kabla ya kuwafungulia kesi kwa kupima uzito wa makosa, wakati makosa mengine yanaweza kutolewa adhabu na ikawa fundisho kwa watoto wengine.

(c) Mhe. Waziri huoni kwamba ucheleweshaji wa Mahakama ya Watoto na Mahabusu unavunja sheria ambayo tumeitunga wenyewe.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 165 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, si kweli kwamba Mahakama za Kitoto hazijaanzishwa hapa Zanzibar. Kwa mujibu wa sheria zetu Mahakama za Watoto zipo kwa muda mrefu na zinaendelea kufanya kazi zake katika kila Mkoa.

Kama nilivyosema Jana Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2011 kifungu cha 18 Mwenyekiti wa Mahakama hiyo ni Hakimu wa Mkoa akiwa na wajumbe wengine wasiopungua wawili ambao watachaguliwa na Mhe. Jaji Mkuu kama ilivyoainishwa katika kifungu Nam. 18(4).

Mhe. Spika, vile vile si kweli kwamba watoto wanasota gerezani kwa sababu hakuna Mahakama za Watoto. Kama nilivyosema Mahakama hizo zipo na wanapata huduma sawa na washtakiwa wengine, na pengine wanatoa huduma zaidi kwa sababu wao wana Mahakama zao peke yao.

Mhe. Spika, uhalifu ni uhalifu tu, na lazima hatua zichukuliwe za kukomesha uhalifu huo. Linalomsababisha mhalifu kubakia mahabusu kabla ya kesi yake ni mambo mengi, kama vile kukosa wadhamini, kutokamilika kwa uchunguzi, kuwa na wasiwasi kuwa mhalifu anaweza kutoroka na kadhalika.

Mhe. Spika, kila kosa lina vigezo vyake vya kisheria kabla ya mhalifu
hajapelekwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka. Kwa mfano wizi, ni lazima ionekane kuwa mtuhumiwa alikuwa na nia ya kuiba, kwamba kitu hicho alichokichukua sio chake na kwamba amekiondoa (kukichukua) kutoka mahala kilipo bila ya idhini ya mwenye mali hiyo.

Mhe. Spika, kila kosa vile vile lina adhabu yake na Hakimu anahitajiwa azingatie mambo mengi kabla ya kutoa adhabu kwa mkosaji.

Kwa mfano, Hakimu lazima azingatie uzito wa kosa lenyewe na kero lake kwa jamii, kama mkosaji ni mara ya mwanzo au ni mzoefu, umri wa mkosaji, afya ya mkosaji na kadhalika, na hapo ndio adhabu itolewe kwa kuyazingatia mambo yote hayo katika mtazamo mzima wa kuikinga jamii kutokana na uhalifu wa mhalifu huyo.

Mhe. Spika, jibu la swali la 165 (d) ni kuwa hakuna ucheleweshaji wa kesi za watoto kwa sababu Mahkama hizo zipo tokea zamani na sio kweli kwamba Mahkama hizo hazijaanzishwa kama alivyodai Mhe. Mwakilishi.

Nam. 149

Vituo vya Zimamoto na Uokozi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza**:**

Ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiweze kutekeleza vyema majukumu yake, suala la kuwa na vituo vya karibu na sehemu zinazotarajiwa kutokea majanga ya moto ikiwa ni pamoja na Bandarini, Uwanja wa Ndege na maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa Hoteli kama vile Nungwi ni jambo la msingi sana.

(a) Je, Kikosi cha Zimamoto kina vituo vingapi vinavyofanya kazi ukiacha vituo vya Bandarini na Uwanja wa Ndege.

(b) Kwa mujibu wa taratibu za Kimataifa, ni muda gani moto unatakiwa uwe umeshazimwa tangu kuanza kuwaka.

(c) Je, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kina wafanyakazi wangapi wenye ujuzi wa kuzima moto kitaalamu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi -Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 149 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kikosi kina jumla ya vituo vitano (5) vya zima moto ukiachilia mbali vile vituo vilioko katika viwanja vya ndege. Vituo hivyo ni pamoja na Mjini Unguja, Chanjaani Pemba, Mahonda, Kigunda Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, mipango inafanywa ya kuwa na vituo vyengine katika maeneo ya Mkoani na Wete kwa upande wa Pemba na Mwanakwerekwe na Uroa kwa upande wa Unguja.

b) Kwa mujibu wa taratibu za kimataifa moto unatakiwa uwe umeshadhibitiwa kwa asilima 90 ndani ya dakika tatu tangu kuanza kwake. Kinyume cha muda huo ndipo husababisha kazi za uzimaji moto kuwa kubwa zaidi kwa vile unakuwa umeshakuwa umetandawaa.

c) Kuna idadi ya kutosha ya wafanyakazi wenye ujuzi wa kuzima moto na uokozi. Wafanyakazi hao tayari wameshapatiwa elimu ya kitaaluma zaidi kwa viwango vya kimataifa katika nchi za Uingereza, Singapore, China na Japan.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa pumzi, uhai na uzima na kutuwezesha kukutana leo katika Baraza lako tukufu na mimi kunipa uwezo wa kuwasilisha mbele yenu Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe. Spika, pia sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango mbali mbali waliyoitoa wakati walipoujadili mswada huu. Nawahakikishia kuwa michango na mawazo yao nimeyapokea na yamenisaidia sana katika kuimarisha mswada huu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006 elimu ya lazima ni haki ya msingi kwa kila mtoto wa Zanzibar na itatolewa kwa muda wa miaka 12 kuanzia elimu ya maandalizi hadi sekondari ya kidato cha nne. Pia sera inaagiza kutolewa kwa elimu bora itakayowawezesha vijana wa Zanzibar kuweza kuitumia elimu watakayoipata kwa maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi na kuweza kuchangia maendeleo ya taifa.

Sera hiyo inatekelezwa kivitendo hatua kwa hatua na imetafsiriwa kwa kuangaliwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa mwaka 2007/2008 hadi 2015/2016. Nafasi za upatikanaji wa huduma ya elimu ya lazima katika ngazi zote zimeongezeka sana. Asilimia ya uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya maandalizi imefikia asilimia 37.1, elimu ya msingi asilimia 118.5 na elimu ya sekondari hadi kidato cha nne ni asilimia 67.2 mwaka 2011.

Sera ya Elimu pia imeelekeza katika kuinua kiwango cha ubora wa elimu. Mojawapo ya maelekezo ya sera hiyo ni kuundwa kwa chombo cha kufanya tathmini ya ubora wa elimu ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inalingana na viwango vya ubora kwa mujibu wa vigezo vya kitaifa na kimataifa. Hiyo inapatikana katika kitabu cha sera ukurasa wa 29 kifungu 5223.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikitunga na kusimamia ufanyaji wa mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili kwa lengo la kuchagua wanafunzi watakaoendelea na masomo katika skuli za sekondari za michepuo na kuingia kidato cha tatu.

Pia wizara imekuwa ikitunga na kusimamia kwa mitihani ya ualimu kwa ngazi ya cheti cha ualimu wa elimu mjumuisho *(inclusive education),* ualimu wa dini na kiarabu na stashahada ya ualimu wa msingi. Watahiniwa wanaofaulu wanapatiwa vyeti vinavyotolewa na wizara badala ya chombo huru kinachosimamia masuala hayo.

Hata hivyo, vyeti vinavyotolewa kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha pili vinatumiwa na wanafunzi wetu kwa ajili ya kukubaliwa kujisajili kufanya mitihani ya kidato cha nne bila ya kufanya mtihani wa maarifa *(qualifying test).* Pia vyeti hivyo vinawawezesha wanafunzi kukubaliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika nchi za nje au pia cheti hicho kinatumika kama hati rasmi ya kuombea kazi katika taasisi zetu za serikali na kampuni binafsi.

Mhe. Spika, matokeo ya mitihani hii mara nyingi yamekuwa yakitumiwa kwa madhumuni ya kuchagua wanafunzi watakaoendelea na masomo katika ngazi ya juu zaidi badala ya kutumiwa katika kufanya tathmini ya ubora wa elimu yetu. Matokeo yake baada ya kukamilika kwa shughuli za utoaji wa matokeo ni hatua za ufuatiliaji zinazofanyika ni chache mno.

Mbali ya mitihani hiyo wanafunzi wetu wanaoendelea na masomo wanafanya mitihani ya kidato cha nne na sita na wanafunzi wa mafunzo ya ualimu wa Zanzibar wanafanya mitihani inayotungwa na kusimamiwa na Baraza la Mitihani Tanzania *(NECTA)* na wanaofaulu wanatunukiwa cheti na stashahada za Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mhe. Spika, kwa vile wanafunzi wote watakuwa na haki ya kupata elimu ya lazima hadi kidato cha nne, kuna umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya wanafunzi hao kupimwa katika kipindi chao chote cha elimu badala ya kusubiri mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili ambayo ni ya mwisho.

Mojawapo ya majukumu ya bodi hii itakuwa ni kuandaa mbinu za kupima na kufanya tathmini juu ya uwezo wa kielimu wa wanafunzi katika ngazi mbali mbali kuanzia katika ngazi ya elimu ya maandalizi na kuendelea. Utaratibu huu utasaidia kuwa na vigezo vya kuweza kuwapima wanafunzi wetu katika hatua mbali mbali za masomo yao tokea katika elimu ya maandalizi. Upimaji huo utasaidia kufahamu dosari zitakazoonekana na kuweza kuzichukulia hatua kabla wanafunzi kufikia madarasa ya juu.

Vile vile kwa kuwa elimu ya lazima sio suala la Muungano Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina haki ya kuunda chombo chake cha kusimamia, kutunga na kutunuku vyeti na stashahada kwa wanafunzi wa ngazi ya elimu ya lazima na mafunzo ya walimu kwa ngazi ya elimu ya lazima ili kupima ubora wa wanafunzi wake. Chombo hiki kitakapoanzishwa kitakuwa ndicho kitakachokuwa kiungo cha mashirikiano na Baraza la Mitihani la Tanzania na vyombo kama hivi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na sehemu nyengine za dunia.

Mhe. Spika, hivi sasa Mkurugenzi wa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu ameshateuliwa na anafanya kazi zake ingawa bodi haijaundwa. Hivyo mapendekezo ya rasimu ya mswada wa sheria hii itawezesha bodi hiyo kuundwa na kufanya kazi zake rasmi.

Mhe. Spika, madhumuni makuu ya mswada wa sheria hii ni kuanzishwa kwa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar ambayo itasimamia shughuli zote zinazohusiana na mitihani ya ngazi ya elimu ya lazima ualimu cheti na stashahada kwa upande wa Zanzibar. Pia chombo hicho kitakuwa na majukumu ya kufanya tathmini ya elimu inayotolewa hapa Zanzibar. Tathmini hiyo itasaidia katika kurekebisha dosari mbali mbali zitakazoonekana katika elimu yetu.

Vile vile bodi hiyo itakuwa ni kiungo cha mashirikiano na Baraza la Mitihani la Tanzania na vyombo vyengine vyenye malengo kama hayo katika nchi za Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika na sehemu nyengine za dunia.

Mhe. Spika, kuundwa kwa chombo hiki kumekuja katika wakati muafaka ambao idadi ya wanafunzi wetu katika ngazi za maandalizi, msingi na sekondari inaongezeka hasa kutokana na sera kuelekeza kuwa wanafunzi wote watakuwa na haki ya kupata elimu ya lazima hadi kidato cha nne. Hivyo, wizara itapaswa kuelekeza nguvu zake zaidi katika uandaaji wa sera, mipango na usimamiaji wa utoaji wa elimu na kuwa chombo huru kitakachosimamia utungaji, usahihishaji na kutunuku vyeti na kufanya tathmini ya elimu kama zinavyofanya nchi nyengine.

Pia kwa vile chombo hiki kitakuwa kinajitegemea kitaweza kujiunga na mashirika yenye madhumuni kama yake na hivyo kuweza kunufaika sio tu kitaaluma na kitaalamu bali pia kupata misaada ya fedha za kuendesha shughuli zake. Aidha, chombo hiki kitafanya tathmini na tafiti mbali mbali zinazohusiana na kazi zake.

Mhe. Spika, mswada huu wa rasimu ya sheria umegawika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ikijumuisha jina fupi la rasimu ya sheria na tafsiri ya maneno mbali mbali yaliyotumika.

Sehemu ya pili inaelezea kuanzishwa kwa bodi, muundo wa bodi na wajumbe wake, uwezo wa bodi, vikao vya bodi na maamuzi ya bodi. Pia inaelezea muda wa wajumbe katika bodi hiyo na uanzishwaji wa kamati mbali mbali za bodi na majukumu yake na uwezo wa bodi katika uajiri wa wafanyakazi. Vile vile sehemu hiyo inazungumzia kuhusu mkurugenzi ambaye atateuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, sifa na kazi zake. Aidha, sehemu hiyo inapendekeza sifa za kielimu na uzoefu wa Mwenyekiti wa Bodi na Katibu wa Bodi. Rasimu hii inapendekeza Katibu wa Bodi awe mfanyakazi mwenye taaluma ya sheria.

Sehemu ya tatu inaelezea masharti ya fedha, vyanzo vya fedha vya bodi, utaratibu wa kufungua akaunti katika benki, namna ya kuweka kumbukumbu za matumizi, utaratibu wa ukaguzi wa akaunti ya bodi na utaratibu wa utoaji wa taarifa kwa Waziri anayehusika na Elimu na Baraza la Wawakilishi.

Sehemu ya nne inaelezea masharti mengineyo ikiwemo taratibu za kula kiapo kwa Maofisa wa Bodi na wafanyakazi watakapewa majukumu mbali mbali ya kutekeleza shughuli za bodi. Makosa mbali mbali yanaweza kufanyika chini ya sheria hii na adhabu zaidi. Pia inazungumzia kumpa uwezo waziri anayehusika na mambo ya elimu kutunga kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, wizara inapendekeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuyakubali mapendekezo yafuatayo:

(a) Kuundwa kwa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu kikiwa ni chombo kitakachojitegemea ambacho kitakuwa na majukumu ya kufanya upimaji na tathmini ya elimu katika ngazi ya elimu ya lazima na mafunzo ya ualimu ya cheti na stashahada.
(b) Kuwa na mamlaka kamili ya kutunuku vyeti vya wanafunzi watakaofaulu mitihani inayoandaliwa na bodi hii.
(c) Bodi kuwa na mamlaka ya kushirikiana na vyombo vyengine vyenye majukumu kama yake likiwemo Baraza la Mitihani la Tanzania na nchi nyengine.
(d) Bodi kuwa na mamlaka ya kufanya upimaji na tathmini ya elimu wa mara kwa mara kuanzia katika ngazi ya maandalizi hadi sekondari na kutoa taarifa juu ya ubora wa elimu.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa bodi hii kutasaidia sana katika kuimarisha shughuli za upimaji na tathmini ya elimu. Matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataujadili kwa kina mswada huu wa sheria na kuyakubali mapendekezo ya kuundwa kwa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu. Kwa niaba yangu na wizara yangu napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa dhati kwa kunisikiliza kwa makini na nasubiri michango yao. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya ili kuwasilisha mchango wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, aidha, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuweza kukutana leo hii ili kujadili na hatimae kupitisha mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziwafikie Wajumbe wa Kamati, watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wanasheria wetu wa Baraza na Serikali kwa mashirikiano ya kutosha kwa kutoa mchango na kutupa muongozo na ufafanuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe. Spika, **a**idha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii napenda kuchukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa ndugu na jamaa wote kwa kifo cha aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Bububu Marehemu Mhe. Salum Amour Mtondoo kilichotokea hivi karibuni.

Mwenyezi Mungu awajaalie subira familia, ndugu na jamaa wote wa marehemu pamoja na kuilaza roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mhe. Spika, ni vyema kuwatambua Wajumbe wa Kamati ambao walihusika katika kuupitia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar. Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2. Mhe Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6. Mhe Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7. Mhe Nassor Salim Ali	Mjumbe
8. Mhe Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9. Nd. Talib Enzi Talib	Katibu
10.Nd. Asha Said Mohammed	Katibu

Mhe. Spika, madhumuni makuu ya mswada huu kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ni kutunga sheria ya kuanzisha chombo cha kudumu kitakachojitegemea na kutambulikana katika kushughulikia masuala ya mitihani katika ngazi ya elimu ya lazima, ualimu cheti na stashahada pamoja na kufanya tathmini ya elimu inayotolewa Zanzibar.

Awali Mhe. Spika, jukumu hili lilikuwa likisimamiwa na wizara kwa ujumla kutokana na kutokuwepo kwa chombo hicho. Aidha Mhe. Spika, kumekuwa na kanuni kwa ajili ya madhumuni hayo ambazo pia imeonekana kuwa hazikidhi haja kwa madhumuni yaliyokusudiwa hivi sasa.

Mhe.Spika, kamati yetu inaiunga mkono serikali kwa kuona ipo haja ya kuwa na sheria maalum na vile vile chombo imara kwa ajili ya mafanikio na ufanisi katika utendaji.
Mhe.Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona kuwa kwa vile elimu ya lazima sio suala la Muungano, ina haki ya kuunda chombo chake cha kusimamia, kutunga na kutunuku vyeti na stashahada kwa wanafunzi wa ngazi ya elimu ya lazima na mafunzo ya ualimu ili kupima ubora wa wanafunzi wake.

Hilo ni jambo jema hasa katika kutathmini maendeleo ya elimu Zanzibar kwa hapa tulipo na hata baadae sambamba na changamoto zinazoikabili sekta ya elimu ulimwenguni.

Mhe.Spika, kwenda sambamba na hilo, kamati yetu inaona kuwa wakati umefika pia kwa Zanzibar kuanzisha mitihani yake ya darasa la kumi na mbili ili kwenda sambamba na sera yake ya elimu pamoja na kuweza kujitathmini kupitia chombo chake huru cha Bodi ya Upimaji na Tathmini kitakachoanzishwa. Tathmini hiyo itasaidia kurekebisha mapungufu yatakayojitokeza katika elimu yetu.

Mhe.Spika, Bodi ya Upimaji na Tathmini itakayoanzishwa iwe ni kiungo tu cha mashirikiano na vyombo vyengine vyenye malengo kama hayo, lakini hivyo vyombo vyengine visiendelee kutumika katika kusimamia mitihani ambayo usimamizi na uendeshaji wake unaweza kufanywa na Bodi yetu ya Tathmini itakayoanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kamati yetu imebaini kuwa miongoni mwa changamoto za msingi ambazo zinaikabili Bodi ya Upimaji na Tathmini ni kukabiliwa na gharama kubwa za uchapishaji wa mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili.

Katika kukabilina na hili kamati yetu inaishauri wizara husika kupitia bodi itakayoanzishwa kuona umuhimu wa kuanzisha kiwanda chake cha uchapishaji wa mitihani ili kuepuka kuendelea kutumia gharama kubwa za nje kwa ajili ya uchapishaji wa mitihani hiyo na hata kuwepo kwa wasi wasi wa uvujaji wa mitihani. Aidha Mhe.Spika, kamati yetu inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufanya marekebisho ya kanuni za Sheria ya Kuanzishwa kwa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar pamoja na mambo mengine izingatie kuainisha utaratibu maalum utakaotumika katika utoaji wa matokeo ya mitihani ili kuweza kuwarahisishia wanafunzi wetu kupata matokeo hayo. Pia kanuni hizo ziweke sifa zinazokubalika za watunzi wa mitihani pamoja na kueleza kuwa bodi kitakuwa ndio chombo cha mwisho katika suala la utoaji wa matokeo ya mitihani.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maoni hayo ya jumla naomba sasa niende katika mswada husika.

Mhe. Spika, kimsingi kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya Rasimu ya Mswada, hata hivyo imefanya marekebisho katika baadhi ya vifungu kwa lengo la kusaidia kuboresha mswada huo. Marekebisho hayo ni ya kimaandishi na yale ya msingi ambapo kamati yetu ilipendekeza kuongezwa baadhi ya vifungu.

Mhe. Spika, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo kamati yetu inaona yangefaa.

Mhe Spika, kwanza kamati imependekeza katika ukurasa wa 57 kuingizwa kifungu kipya cha 4(2) kitakachoeleza mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar ukiachia uteuzi wa Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Bodi hiyo ambao huteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Marekebisho mengine yaliyofanyika katika mswada huu ni kuongeza kifungu cha 4(1)(k) ambacho kinamjumuisha mwakilishi kutoka katika vyombo vya usalama kuwa pia ni mjumbe wa Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar. Kifungu hiki kiliachwa kwa makosa wakati ambapo kimo katika Rasimu ya Mswada ya Kiingereza.

Aidha, Mhe. Spika, kamati yetu ilipendekeza kuongezwa kifungu cha 6(1)(L) katika ukurasa wa 59 kitakachoipa bodi uwezo zaidi wa kuchunguza na kuthibitisha vyeti au tunuku nyengine zinazotolewa nje ya bodi iwe ndani au nje ya nchi. Hatua hiyo itasaidia kuwepo kwa vyeti vya kitaaluma vyenye hadhi na vilivyothibitishwa kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Mhe. Spika, kifungu cha 24(1) na (2) ambacho kimetajwa katika Rasimu ya Mswaada wa Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini kwa lengo la kufuta kanuni ya uendeshaji na taratibu za mitihani ya mwaka 1992 kimefutwa. Kamati imeona kuwa ipo haja ya kufutwa kifungu hicho kwa vile bado hakujafanyika marekebisho mapya ya kanuni za uendeshaji na taratibu za mitihani zitakazotumika kufuatia kuanzishwa kwa sheria mpya ya Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar. Na hoja nyengine ni kwamba kufanyiwa marekebisho kwa kanuni mpya moja kwa moja kunafuta kanuni zilizopo.

Mhe.Spika, mwisho, kamati yetu inaunga mkono mswada huu na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe waungane nasi kwa kutoa maoni kadri watakavyoona inafaa na hatimae kuunga mkono na kuupitisha mswada huu muhimu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru tena na tena Mwenyezi Mungu mtukufu kwa mara nyengine tena kutujaalia neema ya uhai na uzima wa afya tukaendelea kukutana katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuwa mtu wa kwanza kuchangia mswada huu muhimu sana wa maendeleo ya Zanzibar. Mhe. Spika, nasema ni mswada muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar kwa sababu roho ya maendeleo yoyote katika nchi yoyote ni elimu, ikiwa hatuko vizuri kielimu tusidanganyane hakuna maendeleo yoyote mengine yatakayokuja hata nchi yetu ikiwa na wingi wa rasilimali zai fedha kiasi gani.

Mhe. Spika, katika gazeti maarufu duniani la *New York Times* la tarehe 10 Machi, 2012 mwandishi mmoja maarufu sana duniani Thomas Friedman ameandika vitabu vingi huyu aliandika makala aliyoipa kichwa cha maneno *Pass the Books. Hold the oil*. Katika makala hii Mhe. Spika, mwandishi Friedman anaonesha kwamba tofauti na wengi wanavyodhania. Nchi zilizoendelea hasa ni zile ambazo zimetoa kipaumbele kwa elimu. Katika makala hii Mhe. Spika, ameonesha kwamba kuna upinzani wa dhahiri kati ya nchi ambazo zinazalisha mafuta kwa wingi labda zikategemewa zitapata mapato mengi na kupanda kwa maendeleo na zile ambazo zimewekeza zaidi katika elimu lakini ikawa safari nyingi.

Kwa faida ya Wajumbe Mhe. Spika, naomba ninukuu sehemu ndogo sana ya makala hii, kwa sababu ya muda sitoweza kuisoma yote. Anasema, *So hold the oil, and pass the books. According to Schleicher, in the latest PISA results, student in Singapore, Finland, South Korea, Hong Kong and Japan stand out as having high PISA scorse and few natural resources, while Qatar and Kazakhstan stand out as having the highest oil rents and the lowest*

PISA course. (Saudi Arabia, Kuwait, Oman, Algeria, Bahrain, Iran and Syria stood out the same way in a similar 2007 trend in International Mathematics and Science Study, or Timss, test, while, interestingly, students from Lebanon, Jordan and Turkey- also Middle East States with few natural resources- scored better.)

Mhe. Spika, ingependeza ningesoma zaidi lakini kwa sababu ya muda naomba niishie hapa. Nitampatia Mhe. Waziri aione makala hii kwa sababu ina mafunzo ya ajabu sana. Mhe. Spika, hii inaonesha kwamba unaweza ukawa tajiri wa rasilimali na ukawa tajiri wa fedha, lakini bado ukawa hukuekeza vizuri katika elimu basi maendeleo katika nchi yako yakawa ni kitu cha ajabu kabisa. Hata wanafunzi wako kufanya vizuri ikawa sio matokeo ya utajiri ulionao. Ndio maana imeoneshwa hata katika nchi za Mashariki ya Kati zinazotambulikana kwa uzalishaji wa mafuta zile nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi, wanafunzi wake wameshindwa kufanya vizuri ukilinganisha na nchi ambazo hazina mafuta kama hizi ambazo zimetajwa hapa nchi maskini ukilinganisha na nchi nyengine za Arabuni kama zile za Lebanon, Jordan na Turkey.

Pia makala hii imeonesha kwamba moja katika nchi tajiri duniani ambazo wastani wa pato la wananchi wake ni kubwa sana ni nchi ya Taiwan ameielezea humu kwamba ni nchi ambayo ni jiwe tu au ni jabali tu haina chochote, wanasema hata mchanga wake wa kujengea unatoka China. Lakini leo inapiga hatua kubwa kwa sababu imewekeza katika elimu.

Kwa hivyo, nimesema ninukuu Mhe. Spika, ili kuonesha kwamba kama tunataka kupiga hatua za maendeleo, basi ni muhimu sana maendeleo yetu, matumizi yetu na uwekezaji wetu ujikite katika sekta ya elimu.

Suala hili Mhe. Spika, niliunganishe na hoja nyengine vile vile kwamba tunasema siku zote, uchumi wa nchi yetu ya Zanzibar ni uchumi wa huduma, ni *services oriented* sio *resources oriented*, sisi hatuna rasilimali kubwa kama zilivyo nchi nyengine za mabara. Kwa hivyo, katika uchumi wa huduma hata nilipokua nachangia mswada wa Tume ya mipango nilisema kwamba ni muhimu mno kuekeza katika elimu kwa kuwapata watu ambao watakuwa wamebobea katika fani hizi kuweza kuhudumia uchumi wa huduma Mhe. Spika.

Hilo Mhe. Spika, ndio ndoto yetu siku zote, tunapoendelea kukariri wanasiasa kutoka vyama vyote, tunataka kuiona Zanzibar inakua Dubai ya Afrika Mashariki, inakua Hong Kong ya Afrika tunazungumzia uchumi wa huduma. Kwa hivyo, nalisisitiza sana Mhe. Spika, hili kwa sababu kama nilivyosema kama tunataka kulielekeza huko basi ni muhimu sana kuekeza katika sekta ya elimu.

Mhe. Spika, jengine katika maelezo ya jumla nilikua nataka kusema kabla sijachangia kwa vifungu. Mswada kwa jumla ni mzuri sana, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri mzee wangu, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na timu yake yote kwa kufanya kazi hii nzuri sana. Yako mapungufu ni kawaida tu za kibinadamu nitayatolea maoni. Nataka niseme kumwambia Mhe. Waziri naamini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali watakuwa na majonzi makubwa kwa kuondokewa na Mhe. Ramadhan Abdalla, kwa sababu wao kwa kipindi kifupi tulipozungumza nao walikua wanamsifu kwa mashirikiano ambayo alikua akiwapa. Ni matumaini yangu na *Inshaallah* isiwe vingine, kwamba Waziri mpya aliyekabidhiwa Wizara hii ataifanya kazi hii aliyoianza Mhe. Ramadhan ili yale mafanikio yaweze kuonekana.

Jambo la tatu Mhe. Spika, niseme pamoja na uzuri huo, yamekuwepo malalamiko kwamba na siku hizi imekua ni kawaida. Wananchi wetu siku hizi wamejifunza kua wasemaji zaidi. Wanasema kwamba kuna baadhi ya wadau ambao hawakushirikishwa katika kutoa maoni kwenye mswada huu, pengine kuna vyama mbali mbali huko na jumuiya za walimu na jumuiya za wazazi ambao hivi karibu wamekua na mawazo mengi juu ya masuala ya mitihani, hivyo wangependa washirikishwe.

La mwisho la jumla Mhe. Spika, nataka niipongeze Serikali kwa kuja na mswada huu, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwamba suala hili sio suala la Muungano na imefika Zanzibar ianzishe mkondo wake wenyewe wa kusimamia masuala haya kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, hivi karibuni tumepata mtikisiko mkubwa katika nchi kutokana na kufelishwa au kufutiwa matokeo kwa wanafunzi wengi wa Zanzibar katika mitihani ya taifa inayofanywa na Baraza la Mitihani la Taifa letu. Mhe. Spika, kati ya wanafunzi 3,303 kama sikosei waliofutiwa matokeo kwa jumla Tanzania. Wanafunzi 1,004

wanatokea Zanzibar. Ukitizama kwa wastani wa idadi ya watu na waliofanyiwa mitihani, basi utakuta uwiano huu haulingani kabisa.

Mimi Mhe. Spika, nashindwa kushawishika kukubali kwamba ati uvujaji wa mitihani uko zaidi Zanzibar kuliko ulivyo Tanzania Bara au Tanganyika. Lakini hapa ndio sababu watu wengi wakawa na wasi wasi kwamba je, kuna nia njema katika hili, maana yake kama unavyojua kuna kamati mbali mbali za wazazi zimeundwa kufuatia suala hili, naomba Serikali suala hili ilifuatilie kwa makini na ichukue hatua za kurekebisha ili mambo haya yasitokee. Mimi naamini hatua za kuleta mswada huu itakua ndio mwanzo kuelekea kua Zanzibar baadae kuwe na Baraza lake la Mitihani la Taifa la Zanzibar.

Mhe. Spika, haya mambo tusiyakwepe kama inafika pahala Zanzibar tunapoteza imani na wenzetu kwamba hawana nia njema basi ni lazima tuchukue mamlaka mikononi mwetu, kwa sababu kama ninavyosema kwamba katiba inaturuhusu kufanya hivyo, mamlaka ya kuendesha nchi kwa Zanzibar ni ya Wazanzibari na sisi Wawakilishi wao waliotuleta hapa tuna haki ya kuyatekeleza madaraka hayo kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Spika, sasa niende katika mswada. Maoni kwanza kuna mambo madogo madogo kwa sababu ya kuokoa muda, basi haya niruhusu niyachangie katika kupitisha vifungu, kwa sababu ni mambo ya maneno sahihi na si sahihi, lakini yale ambayo nayaona yanakwenda katika *content* nilikua naomba niyazungumze.

Mhe. Spika, la kwanza katika kifungu cha 2 kinachohusu tafsiri au ufafanuzi wa maneno. Katika mambo ambayo yameorodheshwa hapa tumeona kwamba kuna stashahada ambayo ukitizama kwa Kiingereza imetafsiriwa kutokana na neno diploma, lakini haikugusa ngazi ya shahada kwa maana digrii na kwenda juu. Mhe. Spika, Zanzibar tayari tumeanzisha vyuo vikuu vyetu hapa, kiko cha Serikali SUZA, lakini pia viko vya binafsi vilivyoanzishwa.

Nilikua najiuliza hii bodi ya upimaji kama ilivyorekebishwa na kamati, bodi ya upimaji na tathmini ya elimu Zanzibar, kwa nini tusiipe mamlaka hata ya kuangalia. Hata kama masuala haya ya elimu ya juu yako katika masuala ya Muungano kwa sasa, lakini ile haja ya kupima pia maendeleo ya elimu katika viwango hivyo, kwa nini tusitumbukize hapo katika tafsiri ili ikaonekana kwamba hatuzungumzi kutoa vyeti na shahada, lakini angalau tungefanya tathmini kwamba na hilo vile vile likawa limejumuishwa.

Jengine Mhe. Spika, katika huo huo ufafanuzi, kuna neno limetiwa pale limeitwa ‘vipimo’, lakini katika marekebisho ya kamati neno lile wamelikataa wametumia neno ‘upimaji’. Sasa nilikua nadhani kwenye ukurasa wa 56 pale kama unatumia neno ‘upimaji’ basi katika tafsiri vile vile lionekane neno hilo badala ya neno ‘vipimo’ ambalo liko pale.

Mhe. Spika, naomba sasa niende katika sehemu ya pili kuanzishwa kwa bodi kifungu cha 4 cha mswada, kifungu hiki kinazungumzia muundo wa bodi. Mhe. Spika, maoni yangu ni kwamba nchi yetu inafanya mabadiliko mengi na tunaelekea katika mfumo ambao unatoa uwakilishi mpana zaidi, ushiriki mkubwa zaidi. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu kuna baadhi ya wajumbe wa bodi ambao wanatoka katika jumuiya mbali mbali, hawa kwa mujibu wa kifungu hiki wote watateuliwa na Waziri. Mimi kwa maoni yangu nilikua nadhani na Waziri atukubalie.

Kwa mfano kifungu (f) mwakilishi kutoka katika jumuiya za walimu. Kifungu (h) mwakilishi kutoka katika jumuiya yoyote iliyosajiliwa, hapa imeandikwa ‘na’ nadhani imekusudiwa iliyosajiliwa ‘ya’ watu wenye ulemavu. Katika kifungu (j) mwakilishi kutoka katika jumuiya za skuli binafsi. Maeneo haya matatu Mhe. Spika, mimi maoni yangu ni kwamba Waziri akubali kwamba hizi jumuiya zenyewe zichague wawakilishi wao.

Nayasema haya kwa hoja Mhe. Spika, kwa sababu kimsingi tunapotaka uwakilishi wa jumuiya kama hizi katika bodi kama hizi, basi tunataka hawa wasimamie maslahi ya jumuiya zao. Sasa kuendelea kua na utaratibu tuliouzoea huu kwamba Serikali yenyewe ndio inayoteua kila kitu, basi tunaweza tukafika pahala ikajenga dhana kama vile hawa watakuja kulinda maslahi ya Serikali kuliko maslahi ya zile jumuiya ambazo zilipaswa kuwakilishwa.

Kwa hivyo, madamu zipo hizo jumuiya basi mimi naomba kupendekeza kwamba hapa tufanye marekebisho kwamba kwa jumuiya hizi wawe watachaguliwa na jumuiya zenyewe.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu hicho hicho kwenye kifungu cha (i) hapa pameandikwa Mwakilishi wa Baraza la Mitihani ya Taifa la Tanzania. Katika marekebisho ya kamati wamependekeza iongezwe aliyepo Zanzibar. Mimi

naona kusema aliyepo Zanzibar haitoshi. Unaweza ukawa na mjumbe au mwakilishi wa Baraza la Mitihani la Taifa anayetoka Bara, lakini kwa kazi fulani akaweko Zanzibar, hii sheria naona haijakaa sawa. Mimi nilikua nataka tupendekeze isomeke, mwakilishi wa Zanzibar katika Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania, nadhani ikikaa hivyo itakua imekaa vizuri zaidi ili kuainisha kwamba ni wale ambao wanaiwakilisha Zanzibar, waliochaguliwa na Zanzibar kuingia kule ndio mmoja wapo atakua mjumbe wa bodi hii.

Mhe. Spika, naomba niende katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki cha 4, imeandikwa mtu hatostahiki kuwa Mwenyekiti wa bodi isipokua angalau awe na shahada na uzoefu katika fani ya elimu. Huku katika marekebisho ya kamati, naomba Mhe. Spika, unistahamilie kidogo na inabidi nifanye hivyo nusu huku na huku. Katika marekebisho ya kamati wamependekeza kwamba kifungu hiki kisomeke, kimerekebishwa kwa kuongezwa maneno yasiyopungua miaka 5 baina ya anayeweza uzoefu na katika. Sasa hii miaka 5 Mhe. Spika, kule mbele kwenye Mkurugenzi pia utakuta kuna miaka 5.

Mhe. Spika, kwa Mwenyekiti wa Bodi, utaratibu ambao tumeuzoea katika Baraza lako mheshimiwa ni kwamba mara nyingi nafasi hizi tumeweka uzoefu wa miaka 7 katika fani nyingi sana. Kwa hivyo, nilikua nadhani kwa sababu ni mtu ambaye anaisimamia bodi nzima tumempa jukumu kubwa sana. Kwa hivyo, ni muhimu mbali ya kua na shahada katika fani ya elimu, lakini tumuongezee uzoefu angalau 7 kumtofautisha na yule Mkurugenzi ambaye tumemwambia angalau awe na uzoefu angalau wa miaka 5.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kabisa mapendekezo ya Kamati ya kuongeza kifungu (c) katika wajumbe cha kuwa na Mwakilishi kutoka katika vyombo vya usalama, kwa sababu hili nalo ni muhimu sana katika bodi kama hizi.

Mhe. Spika, kwanza niseme napongeza marekebisho yaliyofanywa katika kifungu kidogo cha (4) kinachohusu Kkatibu, kimeandikwa vizuri zaidi. Niende katika kifungu cha 5 kazi za bodi. Mhe. Spika, na hili bahati mbaya Kamati haikuliona. Kijifungu (a) cha kifungu cha 5, hiki ukikitizama kimeondoka kabisa katika lengo la mswada, nikisema lengo la mswada mimi naangalia la Kiingereza, kwa sababu baadae sheria itakua ya Kiingereza. Mhe. Spika, tafsiri hii iliyokuwepo hapa sio sahihi, naomba ili nieleweke niisome ile ya Kiingereza, inasema

The board shall perform the following functions:

(a) *To prescribed the procedures in which students in primary, secondary and teachers colleges shall be assessed and the standards to be achieved at each level.*

Mhe. Spika, hapa imetafsiriwa kuweka miongozo itakayoelekeza ni jinsi gani utapimwa utendaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyapata na viwango wanavyostahiki kufikia katika kila kiwango cha daraja ya elimu. Kwa mtazamo wangu Mhe. Spika, hii imekwenda nje kabisa, naomba niirekebishe kwa sababu tu thamira ya Baraza itakuja kutazamwa katika hii ya Kiswahili kwa sababu ndio lugha ya Baraza.

Mhe. Spika, nitampa Mhe. Waziri baadae kama akikubali aichukue, nadhani tafsiri sahihi ya 5(a) katika kipengele ingekua, kuweka taratibu na miongozo itakayotumika kupima uwezo na maendeleo ya wanafunzi katika elimu ya msingi na Sekondari na mafunzo ya ualimu na viwango vinavyopaswa kufikiwa katika kila ngazi. Nadhani hiyo Mhe. Spika, itakua na tafsiri sahihi kwa lile ambalo limekusudiwa hapa.

Mhe. Spika, naomba niende kifungu cha (c). Namuomba Mhe. Waziri akiangalie sana kifungu hiki kwa sababu hapa ndio panazungumziwa kazi za bodi katika kifungu cha 5, kwa sababu maneno mengi yalivyotafsiriwa hayaakisi kisawa sawa ile dhamira iliyokuwepo. Naomba nitaje kifungu cha (c). Mhe. Spika, kwa kuepusha muda sitosoma ile ya Kiingereza tena, lakini ukisoma vizuri kilichokusudiwa hapa badala ya kusema kuweka utaratibu maalum wa mitihani, hapa neno lililotumika ni *to formulate examination.* Kwa hivyo, nadhani tungesema, kutunga mitihani majaribio na aina nyengine za upimaji wa wanafunzi na maendeleo yao kwa mujibu wa mtaala wa Zanzibar.

Vile vile Mhe. Spika, kijifungu cha (d) naona pia haki yake sio sawa sawa ile iliyokuweko katika Kiingereza, nadhani tafsiri sahihi ingekuwa, kuendesha mitihani kwa elimu za msingi, sekondari na mafunzo ya ualimu na mitihani mingine katika Zanzibar kwa kadiri itakavyoonekana inafaa kwa maslahi ya umma. Mhe. Waziri, nadhani akikisoma atanielewa kuwa hii tafsiri kidogo haikukaa vizuri.

Pia katika kijifungu cha (e) cha kifungu cha 5. Kinasomeka, kusimamia, kukusanya na kuweka kumbukumbu za muendelezo wa upimaji wa wanafunzi, na sio utendaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyapata. Kwa sababu hapa panazungumziwa katika Kiingereza *continues assessment of candidate.* Nadhani itakuwa ni tafsiri sahihi zaidi.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu cha (f) naomba turekebishe kwa maoni yangu tuseme, kuweka na kuandaa miongozo kwa skuli na vyuo, inayohusu namna ya kufanya upimaji wa maendeleo ya wanafunzi, kuliko hivi kilivyokaa naona hakiwakilishi ipasavyo ile dhamira.

Kifungu cha (g) Mhe. Spika, neno lililotumika mwisho pale, mitihani inayofanywa na bodi, nadhani ni mitihani inayosimamiwa na bodi, kuliko inayofanywa na bodi.

Kifungu (i) Mhe. Spika, kimeandikwa Kiingereza kuwa, *To conduct research leading to improvement of testing, assessment and examinations at all levels.* Kamati wameirekebisha, lakini mimi kwa maoni yangu, vile walivyorekebisha Kamati wamekosea, vile ilivyokua katika mswada ndio sahihi. Kamati, inanipa kazi kweli Mhe. Spika, ya kwenda huku na huku. Kifungu cha 5(i) kamati imependekeza mstari wa pili neno 'na'iliopo baina ya neno 'wanayopata' tena lisomeke katika. Sasa ukilitia neno katika hapa Mhe. Spika, utaisoma kwamba kufanya tafiti zinazopelekea kuinua kiwango cha majaribio, upimaji wa utendaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyapata katika mitihani ya ngazi zote. Lakini hapa ilivyokusudiwa ni upimaji wa utendaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyapata na mitihani katika ngazi zote. Hivyo ndivyo ilivyo katika Kiingereza Mhe. Spika.

Vile vile Mhe. Spika, naomba tukirekebishe ikiwa maoni yangu yatakubaliwa kifungu cha (j) kisomeke vizuri katika kutathmini cha Kiingereza kwa kusema, kushirikiana na vyombo mbali mbali vya kitaaluma vya hapa nchini kikanda na za nchi za nje mamlaka za uratibu na usimamizi na wadau wengine husika katika kufanya utafiti, kuchapisha takwimu na taarifa nyengine ili kukuza utaratibu unaofaa wa mitihani na kiwango bora cha elimu Zanzibar. Hivyo hivyo Mhe. Spika, naomba kifungu cha (k) kisomeke kufanya tathmini ili kugundua na kuzifanyia kazi nguvu na mapungufu ya mipango ya elimu na kuinua kiwango cha wanafunzi katika kujifunza.

Kifungu cha (l) vile vile huku kimeandikwa, *to set rules for regulating the conduct of examinations.* Lakini Kiswahili imeandikwa kuweka miongozo, nadhani sahihi kutunga kanuni za uendeshaji wa mitihani na kwa mambo mengine yoyote yanayofaa kwa ajili hiyo.

Pia kifungu cha (m) Mhe. Spika, pale mwisho kufanya mambo mengine muhimu kwa kuharakisha utekelezaji mzima wa moja au zote kati ya kazi zilizoelekezwa, pamekosekana neno pale, kwa bodi chini ya sheria hii. Hivi ilivyoandikwa imeandikwa kwa mujibu wa sheria hii imekosa lile neno la bodi ambalo linajitokeza pale.

Mhe. Spika, naomba niende katika kifungu cha 6 cha mswada huu uwezo wa bodi. Yako maneno machache nitakuja kuyarekebisha, naomba ruhusa yako wakati wa kuja kupitisha vifungu ili niepushe muda, lakini makubwa ni moja (c) pale, imeandikwa kuonesha umuhimu wa kazi za bodi kwa kutumia muhuri wake. Mimi nadhani neno la kutumika la Kiingereza ni *to signify.* Kwa hivyo nadhani ni kuthibitisha kazi za bodi kwa kutumia muhuri wake. Lakini ambapo nilikua nataka nipate maoni hasa ni katika kifungu cha (f). hapa pamezungumzwa, kualikwa chombo au vyombo vyovyote nje ya Zanzibar kama itakavyoona inafaa kuendesha mitihani ya kitaaluma kifundi na mingineyo katika Zanzibar na kuendesha mitihani hii kwa pamoja na bodi na kutunuku vyeti au stashahada, kwa wanafunzi watakaofaulu katika mitihani hii.

Mbali ya marekebisho ya lugha Mhe. Spika, ambayo ningependekeza isomeke, kualika na kuingia makubaliano na vyombo vyovyote kutoka nje ya Zanzibar, kama itakavyoona inafaa kuendesha mitihani. Lakini nilikua nataka ku-*insists* pia juu ya *content* ya kifungu hiki. Mhe. Spika, nadhani wewe na wenzio wenye umri kama wako mnatuhadithia sana juu ya Zanzibar ilivyokua wakati mnafanya mitihani ya *cambidge* na jinsi ambavyo wakati fulani naambiwa hata mwanafunzi bora wa mitihani ya *cambridge* katika nchi zote za Jumuiya ya Madola, *Commonwealth* aliwahi kutokea Zanzibar.

Sasa katika hali kama hii ambapo kumekuwa kutokuaminiana katika uendeshaji wa mitihani ndani ya Jamhuri ya Muungano. Mimi nilikua nadhani kwa kutumia kifungu hiki Mhe. Waziri na uongozi wa Wizara wazingatie sana katika ile haja ya kupandisha viwango, kama nilivyosema mwanzo katika mchango wangu, kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yote, basi tusione kazi Mhe. Spika, kama tutapata nafasi ya kuingia makubaliano na

kualika taasisi za nje ambazo zinaheshimika duniani ambazo tukipata nafasi ya wao kukubali kuja kutufanyia mitihani vitapandisha hadhi elimu ya Zanzibar, basi tusione tabu kuwakaribisha, tukiamini kwamba hilo hatimaye litasaidia sana katika maendeleo ya elimu kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mengine ya lugha yako mengi, hivyo nitayawacha na kuja kuyachangia katika vifungu. Lakini katika kifungu cha 7(8) kinachohusu vikao na maamuzi ya bodi. Mhe. Spika, kifungu hiki kinazungumzia uhalali wa matendo au mwenendo wa uendeshaji bodi wowote hautoathirika kwa kutokuwepo kwa moja kati ya wajumbe au kwa kasoro kati ya uteuzi wa mmoja wa mmoja wao.

Sina tatizo Mhe. Spika, ya kwamba maamuzi ya bodi yasiathirike kwa kutokuwepo kwa mmoja kati ya wajumbe, lakini nina matatizo na hili la pili, au kwa kasoro katika uteuzi wa mmoja wao. Mhe. Spika, mimi nadhani kama kuna mjumbe taratibu za uteuzi wake umetokezea kasoro, basi huyo anapoteza sifa za kuwa mjumbe, sasa hatujui watakua wangapi katika orodha hii, binadamu anaweza akawa mmoja au wanaweza wakawepo zaidi ya mmoja. Sasa tukihalalisha maamuzi ya bodi hata panapotokezea kwamba kuna kasoro katika uteuzi wa wajumbe wa bodi, mimi nadhani hapa tutakua hatutungi sheria nzuri Mhe. Spika.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri hili akubali kuanzia yale maneno, au kwa kasoro katika uteuzi wa mmoja wao yaondoke, tumalizie tu pale kwamba uhalali wa matendo au mwenendo wa uendeshaji bodi wowote hautoathirika kwa kutokuwepo kwa mmoja kati ya wajumbe.

Vile vile Mhe. Spika, naomba niende katika kifungu cha 8(1) kinachofuata, muda wa mjumbe katika bodi. Imeandikwa, mjumbe wa bodi isipokuwa wale ambao wapo kutokana na nafasi zao za kazi utakua ni kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi, na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kama ambavyo Waziri ataona inafaa.

Sasa ukiwacha hivi hivi Mhe. Spika, kwamba anaweza kuteuliwa tena katika kipindi chengine, unaiwacha wazi, kwa hivyo anaweza kuteuliwa kwa vipindi vitatu au vinne. Lakini ukisoma Kiingereza neno lililotumika ni kwamba ni kwa kipindi chengine. Kwa hivyo, nilivyofahamu mimi kinachokusudiwa ni kipindi chengine kimoja. Hivyo ningependekeza kwamba tungeirekebisha ikasomeka, ataweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja chengine au kwa kipindi chengine kimoja kama ambavyo Waziri ataona inafaa, ili kutoa nafasi ya mtu kuingia sio zaidi ya mara mbili katika bodi hii.

Mhe. Spika, naomba niende katika kifungu cha (9) kueleza bayana maslahi na ili nieleweke naomba nikisome kinasema, mjumbe atakapokuwepo kwenye kikao cha bodi au kamati yoyote ambapo mjumbe huyo kwa kuzingatia kua atakua katika shauri ambalo lina maslahi ya moja kwa moja, au sio la moja kwa moja kwake yeye binafsi, mjumbe huyo atalazimika kwa kadiri iwezekanavyo mara tu baada ya kuanza kwa kikao, aeleze bayana maslahi hayo na ni marufuku kwake kushiriki katika mazingatio au mjadala wowote au kupiga kura katika jambo linalohusiana na shauri hilo, halafu ikamalizia, isipokua tu pale bodi itaelekeza vyenginevyo.

Mhe. Spika, haya maneno ya mwisho siyaungi mkono. Nadhani iishie pale na shauri hilo. Hoja yangu ni kwamba tukianza sheria kutoa mwanya kwa bodi kuruhusu mjumbe ambaye kesha *declare interest* halafu bado unamwambia asishiriki, lakini bodi ikimruhusu ashiriki katika maamuzi kuna uwezekano, mambo haya Mhe. Spika, tunayajua sote, wanaweza ndani ya bodi mule wakawa na maelewano fulani, akaja akaachiwa mjumbe, kwa sababu kuna nipe nikupe na yeye ikajakutokezea jengine na mwengine akaachiwa. Mimi nadhani kama mtu ana-*direct interest principle* ambayo tumeizowea ni kwamba mtu yule anakua hashiriki katika maamuzi ambayo yeye ana- *direct interest*. Kwa hivyo, nilikua naomba haya maneno ya mwisho, isipokua tu pale ambapo bodi itaelekeza vinginevyo tuyaondoe.

Mhe. Spika, naomba moja niseme kwa jumla. Katika vifungu vingi vilivyotajwa makosa katika faini inaandikwa shilingi za Kitanzania. Nadhani sio utaratibu wetu Mhe. Spika, inajulikana sheria imetungiwa Zanzibar ambapo pesa iliyotumika ni shilingi ya Tanzania, kwa hivyo faini ni kwa mujibu wa shilingi ya Tanzania na hatujawahi kutunga sheria tukasema shilingi za Kitanzania, tunaandika tu faini ni shilingi. Kwa hivyo, hili nalisema hapa nadhani kote iendelee hivyo hivyo. Hata katika Kiingereza inataja tu shillings, haisemi Tanzania shillings, nadhani utaratibu wa kawaida wa kutunga sheria tunasema shilingi tu. Kwa hivyo, haya maneno ya Kitanzania yamo katika vifungu vingi, naomba Mhe. Waziri akubali kwamba turekebishe.

Kifungu cha 5(9) Mhe. Spika, vile vile kule mwisho kwa hoja kama niliyoeleza katika kijifungu cha 9(1) kuna maneno, isipokua kama bodi itaelekeza vyenginevyo. Hapa ni vile vile kinasema kwamba iwapo mtu amehusishwa katika kuendesha mitihani au kufanya kazi zinazohusiana na mitihani na anayo maslahi binafsi ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja katika mitihani hiyo, au karatasi za mitihani au maelezo yanayohusiana na hayo, au ikiwa mke, kamati imeongeza mume, mtoto, naona wamesahau neno moja rafiki au jamaa wa mtu huyo ni mtahiniwa katika mitihani hiyo, atalazimika haraka iwezekanavyo kabla ya kuanza kutekeleza jukumu lake kuhusiana na mitihani hiyo, aweke bayana maslahi hayo kwa bodi au aliyemchagua kutekeleza jukumu hilo na atalazimika kuacha kutekeleza jukumu hilo, isipokua kama bodi itaelekeza vyenginevyo. Haya maneno Mhe. Spika, isipokua kama bodi itaelekeza vyenginevyo, mimi nilikua naomba tuyaondoe, kwamba mtu akiwa na *direct interest* basi huyo awe *disqualify* katika kutunga mtihani ule ambao atakuwa na *interest* ya moja kwa moja.

Mhe.Spika, kama nilivyosema mambo mengine ya shilingi za Kitanzania nimeyarekebisha kwa jumla.

Sasa naomba niende katika yale ambayo tunazungumzia moja kwa moja mambo ya maudhui ya mswada kuliko kurekebisha lugha kama nilivyosema kwamba nitarekebisha baadae.

Mhe.Spika, tukiangalia ukurasa wa 62 kifungu cha 13(5) naomba kunukuu.

Kifungu cha 13(5) kinaeleza hivi:-

> "Mtu ambaye atamzuia Ofisa mwenye mamlaka kutekeleza
> kazi zake kwa mujibu wa sheria hii, ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za Kitanzania laki mbili na nusu, au kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote viwili faini na kifungo".

Mhe.Spika, kamati imerekebisha kidogo hapa.Lakini naona kwamba hiki kijifungu cha 4 hapa juu kinachozungumzia kuhusu ofisa huyu kupewa kitambulisho katika muundo ambao utaainishwa kwenye kanuni, ili aweze kufanya kazi zake. Kwa hivyo, hapa panazungumzwa kwamba mtu atakayemzuia ofisa huyo atakuwa ametenda kosa, lakini hapakuelezwa na huyo ofisa naye akiwa ata-*breach* ile *trust* ya kutumia kitambulisho kile naye atakuwa ametenda kosa.

Kwa kweli nimeangalia huku mwisho ambako kumetajwa makosa ya jumla katika kijifungu cha 22, lakini nadhani na hapa kuna haja ya Mhe.Waziri kukaa na Mhe.Mwanasheria Mkuu wakaona haja ya kuweka kosa na wala si kwa atakayemzuia tu, lakini hata huyu mwenyewe ikiwa atatenda kosa.

Mhe.Spika, kama nilivyosema kwamba masuala ya lugha nitayarekebisha baadae, basi niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 19 kuhusu Fedha na Mapato ya Bodi, naomba kunukuu.

Kifungu cha 19(1) (a) kuhusu Fedha na Mapato ya Bodi kinaeleza hivi:-

> (a) "Fedha ambazo zinazotolewa na Baraza la Wawakilishi kwa Bodi".

Mhe.Spika, kamati imefanya marekebisho, lakini hili neno kimsingi zinazotolewa limeachwa. Mhe.Spika, nadhani Baraza la Wawakilishi hatutoi fedha, isipokuwa sisi tunaidhinisha na hapa neno lililotumika huko ni *prove by* sio *provided*, maana Baraza halina fedha lenye linakwenda kulia kwa kuomba fedha kwa ajili ya kuweza kufanya kazi zetu. Kwa hivyo, nafikiri turekebishe kwa kutumia neno zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa Bodi.

Kifungu cha 22 Mhe. Spika namalizia, pia kuna kitu ambacho kwa bahati mbaya wenzetu wa kamati hawakukiona kifungu cha 22(1) kuhusu Viapo, Makosa na Adhabu. Mhe. Spika, hapa kuna maneno hapa, kile kifungu kimemalizia Mkuu wa Viapo na halafu kuna kituo kikubwa, pia kuna maneno hapa Kiapo cha Kutunza Siri kwa mujibu wa Sheria Rasmi za Viapo, yananing'inia peke yake.

Kwa maana hiyo, haya yanapaswa yaje yaungane huku juu, kwamba isomeke Bodi inaweza kumtaka mtu yeyote anayefanyakazi za Bodi au ametakiwa kuendesha mitihani au kuchukua karatasi zote za mitihani kula kiapo mbele ya Mkuu wa Viapo, Kiapo cha Kutunza Siri kwa mujibu wa Sheria Rasmi ya Viapo, ndivyo ilivyo katika Kiingereza. Kwa hivyo, nadhani iunganishwe pale juu kwa sababu hili kamati haikuliona.

Mhe.Spika, kwenye kifungu hicho na sehemu nyengine imetumika, nimeona lugha mpya katika Kiswahili huku tunatumia katika kutamka kifungu kidogo cha kwanza. Lakini nafikiri katika utungaji wa sheria mara nyingi *consistency* ni jambo muhimu sana.

Sasa lugha tuliyoizoea humu ndani siku zote ni kwamba tunapofanya *reference* au marejeo kwa kifungu kidogo, neno tunalotumia ni kijifungu. Kwa mfano, hapa kwenye 2(a) anawajibika chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki ndio utaratibu unaotumika, kuliko kuandika kifungu kidogo cha kwanza na wala haisemi cha kifungu kipi na hayo yapo sehemu kadhaa, basi ni vyema tuyarekebishe, ili tuwe na *consistency* katika namna tunavyotunga sheria.

Mhe.Spika, nyengine katika kijifungu hicho cha 2(d) katika makosa imeandikwa atachapisha, atauza, atanunua, ataazima au kukopesha vyeti. Sasa haya maneno yametafsiriwa *literary* mno kutoka katika Kiingereza, kwa sababu neno lililotumika katika Kiingereza ni *lends*. Lakini *lends* si lazima uwe unakopesha kila wakati, hata kutoa pia na nafikiri ndilo neno ambalo ni sahihi zaidi, na zamani tulikuwa tukitafsiri neno hilo. Kwa hivyo, nadhani tuseme, atachapisha, atauza, atanunua, ataazima au atatoa vyeti au stashahada bila ya kupewa mamlaka ya bodi.

Halafu kifungu au kijifungu (f) kuna neno katika Kiingereza limetumika pale *false certificate* na hapa halionekani, isipokuwa imeandikwa iliyopatikana kwa njia ya udanganyifu. Kwa hivyo, nadhani *false* hasa ni iliyoghushiwa, kwa sababu inawezekana ikawa ni cheti halisi, lakini umekipata kwa njia ya udanganyifu, hivyo *false* ni kile ambacho kilichoghushiwa. Kutokana na hali hiyo, ni vyema yakaonekana yote hapa ikiwa mtu ameiba au aliyepata kwa njia ya udanganyifu au kilichoghushiwa, vyote itakuwa ni makosa.

Mhe.Spika, kifungu cha (i) nadhani lile neno kuwa ni Ofisa, basi ianzie akiwa ni Ofisa aliyeidhinishwa, na akatekeleza kazi alizopewa katika sheria hii kwa uzembe au dharau ndio itakuwa imekaa vizuri.

Mhe.Spika, baada ya kusema hayo, lakini kama nilivyosema yako mengi ya marekebisho ya lugha ya hapa na pale, pamoja na makosa ya uchapaji nitakuja kuyarekebisha wakati wa kupitisha vifungu na wala nisichukue muda mwingi.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba naomba ufafanuzi, lakini sijui niuombe kwa Mhe.Waziri au Kamati, kwa sababu kwenye mapendekezo ya kamati mwisho kabisa wamependekeza kifungu cha 24(1) na (2) kifutwe, yaani wamesema kifungu cha 24(1) na (2) kimefutwa.Sasa mimi nilivyosoma katika mswada huu kifungu cha 24 kinazungumzia kufuta na kubakiza, ambao ni utaratibu wa kawaida wa kutunga sheria. Mhe.Spika, naomba kunukuu

Kifungu cha 24(1) kinaeleza hivi:-

> 1 “Kanuni ya uendeshaji na taratibu za mitihani ya 1992 zinafutwa”

Halafu cha 24 (2) kikahalalisha naomba kunukuu Mhe.Spika.

Kifungu cha 24(2) kinaeleza hivi:-

> (2) “Jambo lolote halali lililofanywa chini ya kanuni zilizofutwa na kifungu cha (1) cha kifungu hiki, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya Sheria hii.

Mhe.Spika, huu ni utaratibu wa kawaida na kama tumetunga sheria hii, basi mimi nilivyofahamu hata kwenye maelezo ya madhumuni na sababu ya Mhe.Waziri yameeleza kwamba, kwa kutunga sheria hii tunaondokana na ule utaratibu wa zamani kuwa tulikuwa na kanuni tu. Sasa kamati kwa nini imekikataa kifungu hiki na kusema kifutwe, na wala sijafahamu. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi na sijui nani atanisaidia Mwenyekiti wa Kamati au Mhe.Waziri, lakini nadhani tusaidiwe zaidi Mhe.Spika.

Baada ya kusema hayo Mhe.Spika, nakushukuru sana kwa uvumilivu wako mkubwa, na kwa kunipa muda wa ziada ya ninaostahiki.Lakini naamini kwamba nimelisaidia Baraza lako katika kazi zetu tunazopaswa kufanya kutunga sheria zaidi. Kwa hivyo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nakushukuru sana Mhe.Spika. *(Makofi)*

Mhe.Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia mswada huu ambao umeletwa na Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini baada ya hapo hivi sasa amebadilika na kuwa Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza naomba unistahamilie kidogo kwa sababu lahaja yangu niiseme kwenye kiti chako Mhe.Spika, ili watu waweze kujua nini ninachokizungumza.

Mhe.Spika, siku zote mimi huwa ninasema kuwa katika hizi teuzi za Mhe.Rais, basi ndani ya nafsi yangu huwa ninao waziri ambao huweza kuwa Mhe.Rais hakutia mkono kizani, yaani siku zote ninao. *(Makofi)*

Kwa kweli nisifiche siri yangu Mhe.Spika, nimtaje wazi wazi akiwemo mwenyewe Mhe.Waziri wetu wa Elimu na Mafunzo ya Amali, basi Mhe. Rais hakutia mkono gizani katika kumteua na hata huko anakompeleka hali kadhalika.

Mhe.Spika, Wallahi wanavyokwenda vizuri na Naibu Waziri wake, yaani hata katika maswali na majibu angalia jinsi gani wanavyojibu na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanavyoridhika na majibu yao, na wala sijasikia hata siku moja watu hawa wakasemwa kwamba wanajibu vibaya Wajumbe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba nitoe dukuduku langu Mhe.Spika na likufike kwenye kiti chako na Mhe.Rais ajue kuwa nampa pongezi sana kwamba hakukosea na ataendelea kumchagua na sehemu nyengine kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mhe Spika, nini maana ya kusema hivyo. Kwa kweli mswada huu mimi tangu nianze katika Baraza hili, yaani katika miaka ya nyuma na wakati huu naingia kipindi cha pili, Mhe. Spika kila mtu Mwenyezi Mungu humpa akili yake, na kila mtu, mawaziri huangalia jinsi gani ya kuweza kuongeza hali ya ufanisi katika wizara yake. Sasa huleta vitu ambavyo vinakuwa vinatusaidia sana hasa sisi wawakilishi, kwa kupitia wananchi wetu ambao waliotupa kura, kwa ajili ya kupata ufafanuzi.

Hivi karibuni Mhe.Spika, kulikuwa na wimbi kubwa sana la uvujaji wa mitihani na wala hakuna asiyejua suala hili Mhe. Spika, watu walipiga kelele, wengine wakenda Bara, vyombo vya habari vilikuwa vinaeleza hapa na pale.Lakini Mhe.Waziri wetu amekaa kimya na kusema nitakutafutieni chombo ambacho kitaweza kusimamia masuala haya, pia tutaweka sheria kali sana, ili mambo kama haya yasiweze kuvuja.

Mhe.Spika, nakubaliana na mswada huu na mimi mara nyingi sana husema kwamba sitomsifu waziri ambaye mwenye kasoro zake, isipokuwa nitamsifu waziri ambaye mwenye kuleta vitu vyake.

Baada ya hayo, sasa nakwenda kwenye mswada kwenye ukurasa wa 56 kifungu cha 4(1)(a) kuhusu Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais. Mhe.Spika, naomba sana kuwa yeye huyo Mhe. Rais atakayemchagua asiwe na *interest* ya mambo ya kisiasa, isipokuwa awe na lake moja tu.

Lakini kama tutakwenda hivyo na kumchagua mtu ambaye yumo kwenye jopo la mambo ya kisiasa, basi huyo mtu hatufai na hapo lazima Mhe. Rais apaangalie sana, kwa sababu hivi sasa hii tunaifanya kama ndio roho ya elimu, ili vijana wetu wapate kuwa katika hali ya juu.

Kwa hivyo, hilo moja aliangalie, sifa lazima zieleweke na asiambatane na suala la siasa kabisa, kwa sababu hivi sasa siasa imekwisha na tumo katika kuijenga nchi yetu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nikiendelea kwenye ukurasa wa 56 kifungu cha 4(1)(b) kuhusu Mkurugenzi. Vile vile naomba sana kwamba Mkurugenzi naye awe na sifa ambazo ataweza kuiendesha ofisi yake, Mhe. Spika tunawajua Wakurugenzi wengine tunawajua wamechaguliwa, lakini *interest* ya zile ofisi zenyewe hawana, na ndio maana hawa wanawapa matatizo mawaziri katika utendaji wao, na ndipo pale tunapokuja kuwasakama.

Kwa kweli wakati mwengine masuala haya yanatokea huko, yaani wanavuruga tu, basi kwa kuwa mtu amechaguliwa na wengine wanajisifu kwamba hakuna wa kuweza kuniondoa ah! Ameshavurunda baada ya kukaa na kujisawazisha anachoambiwa nini, basi anaendelea na lugha ambazo si nzuri.

Mhe.Spika, naomba sana hapa huyo Mkurugenzi atakayeteuliwa hapa, basi lazima awe miongoni mwa watu waadilifu, na aipende ile sehemu ambayo aliyochaguliwa, kwa ajili ya kuleta ufanisi mzuri sana, ili ile dhana nzima hapa ielekee katika kuwasaidia wanafunzi wetu.

Nikiendelea na mchango wangu kuna hili jopo la Wakurugenzi kutoka Elimu ya Sekondari, Wakurugenzi wa Taasisi mbali mbali. Mhe.Spika, hapa kidogo ningeomba tuangalie hii Bodi iliyoundwa hapa, kuna mambo sijui yatakuwaje katika Mtihani wa "O" na "A" *level* hivi sijui itahusisha vipi katika usimamizi wake hapa, yaani hii bodi sijui itashirikishwa vipi. Kwa hivyo, namuomba Mhe.Waziri kupitia kwako Mhe.Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi ambao unaostahiki.

Mhe.Spika, ukurasa wa 57 kifungu cha 2, naomba kunukuu.

> Ukurasa wa 57 kifungu cha 4(2) kuhusu Muundo wa Bodi kinaeleza hivi:-
>
> > (2) "Mtu hatastahiki kuwa Mwenyekiti wa Bodi isipokuwa angalau awe na shahada ya uzoefu katika fani ya elimu".

Mhe.Spika, angalau basi tungetajiwa kutoka chuo gani, kwa sababu ndio shahada tunajua, lakini tunaangalia na ukubwa na vile vyuo vyenyewe ambavyo vitakavyoweza kusema kwamba hapa hakuna tatizo lolote, basi angalau tuambiwe chuo chenyewe ni kadhaa, na hapo tutasema kweli hakuna tatizo lolote na tutakwenda sambamba.

Suala jengine kwenye ukurasa wa 59 kifungu cha 8(1) naomba kunukuu Mhe.Spika.

> Ukurasa wa 59 kifungu cha 8(1) kuhusu muda wa wajumbe katika Bodi kinaeleza hivi:-
>
> > "Ujumbe wa Bodi isipokuwa wale ambao wapo kutokana na nafasi zao za kazi utakuwa ni kipindi cha miaka mitatu, kuanzia tarehe ya uteuzi, na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kama ambavyo Waziri ataona inafaa".

Mhe.Spika, kifungu hiki bado sijakubaliana nacho na ninazo sababu zangu, hivi kwa nini tutoe kwa muda wa miaka mitatu, na halafu pia kwa nini tuwarudie wale kwa wale, hatuoni kwamba huyu mtu akili imeshachoka. Mhe.Spika, hivi sasa kuna watu ambao akili tayari zimeshachoka na tunavyo vizazi vipya kwa nini hatuwapi.
Sasa matatizo haya ndiyo yanayotusababisha tunashindwa kupiga hatua, kwa sababu leo mtu unamuweka miaka mitatu, kwa *experience* ya mtu katika masuala ya akili kwa mambo ya Ki-*biology* tayari ile akili inaanza kukomaa. Kwa kweli suala hili Mhe.Spika, ninaomba sana hebu tukiangalie, na ndipo pale niliposema kwamba mimi sikikubali kifungu hiki.

Mhe.Spika, kwa taaluma ya Mhe.Waziri, maalim pamoja na mzee wangu, basi ataweza kunielimisha mpaka niweza kushawishika, kwa sababu ajue wazi amesema kuwa huyo mtu anaweza kuchaguliwa tena pale aa! Bora isomeke moja kwa moja kama tunampa miaka mitatu hakuna tena nafasi ya kuchaguliwa, na atafutwe mwengine na hiyo nakubaliana nayo kwa mujibu wa sheria, lakini tusikubaliane tena mtu yule arejeshwe tena pale.

Kwa kweli Mhe.Spika, hii kidogo sitaki nimpinge Mhe.Waziri, isipokuwa tuliangalie uzito wake wa hali halisi ilivyo, kwa sababu akili huwa zinachoka, na hasa kuwa tuna tabia moja ya kusema kwamba mtu kuanzia miaka ya juu ndio anaweza kuwa kwenye *post* kama hizi.

Lakini Mhe. Spika, kuna watoto wadogo ambao wenye maadili mazuri sana, na bado akili zao ni changa kabisa, na wanaweza kuendesha jambo hili na likawa zuri, kuliko kuongezwa mtu ambaye muda wake umeshapita. Mhe.Spika, kidogo hapo kwenye kifungu hiki kuna utata, hivyo namuomba Mhe.Waziri kupitia kwako Mhe.Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 60 kifungu cha 9, naomba kunukuu Mhe.Spika.

Ukurasa wa 60 kifungu cha 9 kuhusu kueleza bayana maslahi kinaeleza hivi:-

(1) "Mjumbe atakapokuwepo kwenye Kikao cha Bodi au
Kamati yoyote ambapo mjumbe huyo kwa kuzingatia kuwa atakuwa katika shauri ambalo lina maslahi ya moja kwa moja kwake yeye binafsi…"

Mhe.Spika, hapa ndipo ninapomsifu Mhe.Waziri wangu.Kwa mfano, tukisema hivi sasa Zanzibar bodi nyingi sana Mhe.Spika zinakuwa na *interest* ya mambo yao na ndio maana utakuta kuna mambo mengi tunaharibikiwa kutokana na mambo kama haya.

Lakini Mhe.Waziri ameanza ku-*defend* mapema, na ni vizuri kwa sababu ameliona hili jambo, kwamba inawezekana mtu akaweka kitu chake kwa mantarafu yake mwenyewe tu na kuweza kuharibu mzungumko mzima wa bodi kwa akili zake yeye. Kwa hivyo, ameliona na kuliwekea sheria ambayo sheria hiyo inasema kwenye kifungu cha 4. Sasa mimi nasema hapa ah! Shilingi 500,000/= hivi sasa sio fedha Mhe. Spika, hebu jaribu kwenda kwa SUMA kama kweli utarudi na shilingi 500,000/=.

Kwa maana hiyo, tuweke kitu ambacho kitashtusha na kuweka msimamo pamoja, na msisitizo na wala sio kitu cha mas-hara Mhe. Spika, kwa sababu watoto wetu wanakesha usiku na mchana kwa ajili ya kutafuta elimu. Lakini mtu anakuja kwa *interest* zake na kuja kupenyeza mambo kwa kweli kitu hiki Mhe. Spika, sikubaliani nacho, kwani shilingi 500,000/= ni ndogo sana. Vile vile na hicho kifungo chake ni miezi mitatu ah! Miezi mitatu si kumpeleka mtu pikiniki kule gerezani, hebu tuwe sheria ambayo itatisha na kupelekea mtu kushindwa kufanya jambo hilo.

Mhe.Spika, miezi mitatu kule, kwa sababu kuna zile sheria kuhusu siku za Jumamosi na Jumapili zinaondoshwa na wanasheria watanisaidia na sijui mpaka leo, kwani kila siku hapa tunazileta sheria zile kwa zile, yaani tunazungumza mule mule. Lakini ninavyojua mimi kwamba siku za *holidays*, basi na wao wenzetu wanakuwa na *holidays* siku zile.

Mhe.Spika, naomba sana suala hili kwamba ni miezi mitatu naona aa! Au sikutizama vizuri, labda nivae miwani kwa sababu wakati mwengine nakuwa sioni vizuri, ndio Mhe.Spika ni miezi mitatu, hapana naona bado hatujajenga mustakabali.

Kwa hivyo, Mhe.Spika akione hiki kitu na wala asimuonee haya au huruma mtu, kwa sababu hali halisi tunaiona Mhe. Spika hivi sasa inavyotokea, yaani watoto wetu wameshavunjika moyo na hali halisi. Kwa kweli watoto wetu hivi sasa walivyokuwa wanaijua hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa nguvu zake kwa kupitia wawakilishi.

Mhe.Spika, mimi mmoja *number* one hivi sasa nimeikubali kabisa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu ni mambo mazuri sana. Mhe.Spika, huyo he, Waziri anayesema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk haipendi Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni muongo sana. Kwa kweli mimi naipenda sana, kwani nimepata elimu yake nzuri na ndio maana tunachangia vizuri hivi sasa, kweli zamani tofauti, lakini leo ninao uwezo wa kusema hiyo siitaki na Mhe.Spika unaona. Kwa hivyo, lazima tuseme ukweli Mhe.Spika, jinsi hali halisi ilivyo, *message* imefika.

Nikiendelea kwenye ukurasa wa 61 kifungu hiki cha 5 na 6 navyo viangaliwe hii faini bado, kwa sababu ni shilingi 500,000/- na hiki sitaki nikieleze sana. Lakini naona hapa kidogo, ili twende vizuri Mhe.Spika, basi tuongeze tena. Kifungu cha 11 Mhe.Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 11 kuhusu posho na malipo ya Bodi kinaeleza hivi:-

"Wajumbe wa Bodi watapaswa kulipwa posho na malipo kama itakavyopendekezwa na Bodi na kukubaliwa na Waziri".

Mhe.Spika, kifungu hiki hebu tuweke bayana, kwa sababu mara nyingi sana bodi huwa wanalipana fedha nyingi sana kuliko ule wakati wa vikao vyenyewe, na halafu wanapokwenda kujadili hakuna kitu ambacho hakileti mfumo mwengine, yaani siku zote ndio yale kwa yale. Kwa hivyo, ni vyema Mhe.Waziri kuweka bayana kwamba posho hili watapewa kiasi gani kwa kila kikao, yaani tuwe wazi na kusema ukweli ulivyo.

Kwa mfano, ukiweka shilingi 200,000/= weka bayana kabisa na wala usione tabu na wakati atakapokuja kufanya majumuisho Mhe.Waziri, basi anijibu tu kwamba kikao kile tumeamua kuweka shilingi 500,000/= *per day* kwa ajili ya kikao. Mhe.Spika, jambo la msingi ni kuangalia uzito wa zile shilingi 300,000/= au 500,000/= kwa siku wanachokizungumza nini na kitaleta faida gani. Kwa hivyo, naomba sana Mhe.Spika kuangaliwa vizuri kifungu hicho.

Mhe.Spika, kwa kumuogopa Mhe.Waziri wangu, kwa sababu nilianza kumpa sifa nyingi sana, sasa naona kila nikiendelea nadhani nitakuja kukosea na baadae nikaja kumtoa makosa na yale yote niliyosema ikawa *nothing*.

Kwa hayo, machache kwa hili naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope.Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuchangia mswada uliopo mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa, pamoja na wizara husika kwa kutuletea kuundwa kwa chombo hiki, ambalo ni jambo la maana tena la msingi kabisa.

Mhe.Spika, ni hivi karibuni tu kulikuwa na vilio vya watoto wetu pamoja na wanafunzi wetu kutokana na kufutiwa mitihani, basi angalau leo tunazungumzia jambo hili watajisikia vyema kuwa na chombo chao.Kwa kweli watajisikia vyema, kwa sababu nyingi sana ambazo zilizojitokeza.

Kutokana na hali hiyo, takribani watoto wengi walikuwa wamekwishakata tamaa. Kwa mfano, ndani ya jimbo langu kulikuwa na watoto wawili wa kike walisema umri tulionao ni watoto, lakini wanakuja waume tunawakataa, na tukiendelea na masomo tunakatishwa tamaa namna kama hii. Kwa kweli hili ni jambo ambalo liliwarudisha nyuma watoto wetu. Kwa hivyo, kuundwa kwa chombo hiki ni faraja kubwa kwa Zanzibar nzima, na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tuwe imara na tutapata mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mhe.Spika, tukiangalia kifungu cha 6(1)(e) na (f) kuhusu Uwezo wa Bodi naomba kunukuu Mhe.Spika.

Kifungu cha 6(1) kinaeleza hivi:-

(e) “Kuendesha mitihani ya kitaaluma na kiufundi na mitihani mengine katika Zanzibar kama itakavyoonekana inastahiki
kwa maslahi ya umma”.

Mhe.Spika, kifungu hiki nikipongeze tu, kwa sababu kimezungumzia jambo la maslahi ya umma tena kwa Wazanzibari ni jambo la neema, kwani jambo zuri lolote lile huungwa mkono na baya nalo hukataliwa, kwa hapa nakipongeza kifungu hiki.

Lakini tuangalie tulikotoka huko ni wapi, tulikuwa na Baraza la Kutunga Mitihani ambalo ni *National Examination Council of Tanzania* (*NECTA)*. Mhe.Spika, hili ni Baraza la Kutunga Mitihani, lakini mimi kidogo napata wasi wasi hivi tunajitoa huko au vipi, kwa sababu za msingi pengine mitihani inayotungwa kule hayendi sambamba na masomo ya kwetu Zanzibar na kuwapa tabu watu wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe.Waziri kupitia kwako Mhe.Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi anipe ufafanuzi mzuri ili niweze kufahamu.

Vile vile kifungu cha 6(1) (f) naomba kunukuu Mhe.Spika.

Kifungu cha 6(1) kinaeleza hivi:-

(f) “Kualika chombo au vyombo vyovyote nje ya Zanzibar
kama itakavyoona inafaa, kuendesha mitihani ya kitaaluma, kiufundi na mengineyo katika Zanzibar na kuendesha mitihani hii kwa pamoja na Bodi na kutunuku vyeti na stashahada kwa wanafunzi watakaofanya mitihani hii”.

Mhe.Spika, na hili ni jambo jema kwa sababu imedhamiria vizuri kutoa vyeti kwa wanafunzi watakaohitimu katika masomo yao, hivyo hili ni jambo jema, tena la faraja na linafaa kuungwa mkono. Lakini ipo haja kama nilivyosema kuunda chombo hicho kwa ajili ya kusimamia elimu ya Zanzibar na wala sio kwa mripuko tu, kwa sababu limejitokeza jambo, basi na sisi tukafanya jambo kwa mripuko tu.

Kwa hivyo, lazima iwe serikali pamoja na wizara husika imejipanga vizuri kuhusiana na jambo hili, kwa sababu masuala ya elimu ndio mambo ya maendeleo kama Mhe.Ismail Jussa Ladhu alivyotoa mfano hapa, kwani bila ya elimu hakuna maendeleo. Kutokana na hali hiyo, basi ni vyema tusiwe tunaripuka tu na lazima tuwe na msimamo thabiti na wala sio kwa kutaja tu hapa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu ni kwamba, tutakuwa na changamoto nyingi ambazo zinazoweza kujitokeza kutoka kwa wenzetu Tanzania Bara, pengine tu kwa kutoitambua Bodi yetu hii. Kwa mfano, inawezekana wenzetu wasiitambue bodi yetu hii, sasa hapa itakuwa tumejipanga vipi. Mhe.Spika, ni vyema kuweka mambo mazuri yenye misingi madhubuti.

Mhe.Spika, pia kutoikubali mitihani yetu inayosimamiwa na Bodi yetu, inawezekana kujitokeza changamoto kama hizo za kutoikubali mitihani inayosimamiwa na bodi yetu. Vile vile inawezekana kujitokeza migogoro ya hapa na pale baina ya bodi na *NECTA*. Kutokana na hali hiyo, lazima tuwe tumejipanga vizuri kwa jambo hili. Kwa mfano, yatatokea hayo Mhe.Spika tumejipanga vipi kukabiliana na kero mbali mbali zinazoweza kujitokeza, basi ni vyema tujipange vizuri bila ya kutetereka. Maana yake tuwe na msimamo thabiti bila ya kuogopa na kujali mambo yatakayojitokeza na hili litakuwa jambo jema.

Mhe.Spika, mimi sikuwa na mchango mkubwa, isipokuwa nilikuwa natoa maoni yangu kwa kuangalia huko tunakokwenda. Lakini hili ni jambo la faraja na nafikiri katika kuzungumza kwetu huku wananchi ambao ni watoto wetu, yaani wanafunzi watakuwa wanafurahia sana. Kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nami nikaweza kuchangia na kutoa mawazo yangu kwa mswada huu wa sheria uliopo mbele yetu, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa wazima na kuweza kushiriki hapa katika baraza lako tukufu. Lakini nimpongeze Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwa kuteuliwa nafasi mpya ya Wizara nyengine, lakini pia niwape pole wale wa Wizara ya Elimu kwa kuondokewa na waziri wao.

Mhe. Spika, madhumuni na sababu za mswada huu kama alivyotueleza Mhe. Waziri ni kutunga sheria ambayo inakusudia kuanzisha chombo cha kudumu kitakachotambulikana na imara, kushughulikia masuala yanayohusiana na mitihani katika Zanzibar hayo ndio madhumuni na sababu. Ambapo ametwambia hapo kabla masuala haya ya mitihani yalikua yakishughulikiwa na Wizara, lakini kulikua hakuna chombo chochote mahsusi kwa ajili ya kushughulikia masuala hayo, kulikua na kijikanuni ambacho kilikua kimetungwa kwa ajili ya madhumuni hayo lakini imeonekana sasa haki kukidhi haja hasa kwa wakati huu.

Lakini akatwambia kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona kwamba ipo haja sasa ya kutunga sheria maalum na vile vile chombo imara kwa ajili ya mafanikio na ufanisi katika utendaji, mimi nampongeza Mhe. Waziri baada ya kuona kwamba ipo haja ya kuona mambo haya.

Mhe, Spika, ni hivi karibuni tu wananchi wa Zanzibar walikua wakisikika, wakisononeka, wakilia, wakipata mfadhaiko juu ya matokeo ya mitihani ya watoto wao ambayo imefutwa kwa sababu mbali mbali, lakini kwa bahati nzuri chombo tunachotunga hapa sasa hivi sicho chombo ambacho kilisimamia matokeo yale ambayo yaliyojitokeza hivi karibuni. Nadhani Mhe. Waziri ili kuepukana na kama hayo yaliyokuwa yametokea basi kiharaka haraka basi ameona atayarishe hichi chombo kitakachosimamia kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa kweli kile ni kilio kikubwa na kama mwenzangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu alivyotangulia kusema jambo lile ambalo limetokea kwa kiwango kile ambacho kwa Zanzibar kimetokea lile ni janga, serikali inatakiwa ilitafakari sana na ilitafakari kwa njia moja pamoja na makoseo yaliyokua yamejitokeza au matatizo yaliyojitokeza, lakini kitendo cha kuwafutia matokeo au kuwapa adhabu watoto wasifanye mitihani ile ya taifa kwa miaka mitatu inahitaji kuangaliwa upya. Kwa sababu watoto wale ni wetu wanahitaji uangalizi na wale bado ni watoto, kwa hivyo ni lazima busara Mhe. Spika, itumike.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa nije kwenye mswada wenyewe ambao uko mbele yetu. Katika kifungu cha kwanza cha mswada huu ambapo kumeeleza jina fupi na kuanza kutumika, naomba kunukuu.

Kifungu hiki kinasema

> "Sheria hii itajulikana kama sheria ya kuanzisha bodi ya vipimo na tathmini ya elimu Zanzibar mwaka 2012 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika gazeti rasmi la serikali".

Wenzetu wa Kamati wamesema badala ya kutumia neno vipimo sasa tubadilishe litumike neno upimaji, mimi naona bado hatujapata jina la mswada huu, kwa sababu ukisema upimaji, vipimo na nahisi tumekua tuna wasi wasi katika kuandaa sheria hii. Mimi nimuombe Mhe. Waziri tubadilishe jina hili badala ya kuanzisha sheria ya kuanzisha bodi ya vipimo kwa nini tusianzishe sheria ya Baraza la Mitihani la Zanzibar. Wala hatuanzishi baraza la Taifa aaa? Tukaja tukaonekana tumekiuka katiba, lakini tuite baraza la mitihani la Zanzibar ambalo litafanya hiyo shughuli ya kutathmini, kupima, vipimo na mambo mengine ambayo yataelezwa kwenye sheria hii *(Makofi).*

Kwa hivyo Mhe. Waziri nadhani usiingie hofu ukaanza kuzunguruka sijui upimaji, vipimo ukaja ukaonekana umekiuka katiba laa hasha, sema tu Baraza la Mitihani la Zanzibar wala sio la taifa hili ni baraza letu ambalo litashughulikia mambo mbali mbali yanayohusu upimaji vipimo na mambo mengine yaliyokua mengi, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hebu libadilishe hili jina tusizunguruke, mara vipimo, mara upimaji mara hivi itakuja kua bodi ya ardhi hilo moja.

Lakini katika kifungu cha pili kuna mtiririko kidogo wa mambo yamejitokeza mara mbili sijui kama wenzetu wa kamati hawakuliona au sijaiona mimi kwenye marekebisho yao lililozungumzwa "jopo", nasema maana yake ni kikundi cha wataalam wa masomo ambao hufanya kazi za ushauri wa bodi, lakini imejitokeza kama mara mbili. Kwa hivyo hili moja tulitoe libakie moja kwa sababu yote yana maelezo ya aina moja.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya mswada ambayo inasema kunaanzishwa bodi, inasema kunaanzishwa baraza la mitihani, hapa kwenye kifungu cha 3(1) kinasema kutakua na bodi ambayo itajulikana kama bodi ya vipimo na tathmini ya elimu ya juu. Mimi nasema tunaanzisha badala ya kwamba kutakua iwe tunaanzisha hapa, kama utakubaliana na mimi neno la Baraza basi lisomeke hilo kwamba tunaanzisha baraza la mitihani kama itakavyojulikana kama baraza la mitihani Zanzibar na mambo mengine ambayo utayapanga wewe mwenyewe.

Jengine ambalo Mhe. Spika, nimeliona katika sheria hii katika muundo wa bodi, katika muundo wa bodi kifungu cha nne kifungu kidogo ambacho wenzetu wa kamati wamejaribu kukifanyia masahihisho eneo la katibu, ambapo hapa mswada umezungumza tu kwamba kifungu cha nne afisa wa sheria atakua katibu wa bodi na maelezo ambayo yapo pale. Lakini wenzetu wa kamati niwapongeze wameiona hii kasoro na wakasema kwamba kifungu hicho sasa kisomeke kwamba kutakua na Katibu wa bodi mwenye shahada ya sheria inayotambulikana na uzoefu usiopungua miaka mitano.

Lakini kifungu kidogo cha tano mbili nacho kinaandikwa upya kisomeke kuwa Katibu wa Bodi atateuliwa na bodi, lakini kifungu chengine cha nne tano cha tatu kinaandikwa upya na kitasomeka katibu wa bodi hatokua na kura katika maamuzi ya bodi mimi sina matatizo ya marekebisho haya ambayo wenzetu wameyaweka.

Lakini tatizo langu ni kwamba katibu huyu sasa hajaoneshwa kazi zake kwa mujibu wa sheria, sasa ningemuomba Mhe. Waziri huyu katibu ambaye tunamzungumza hapa basi sheria imueleze kazi zake na kikawaida makatibu hawa hua ndio wanaoitisha vikao vya bodi kwa kushauriana na mwenyekiti, lakini pia hua ndio wanaotunza kumbu kumbu za mikutano na mambo mengine. Kwa hivyo kuna kasoro hapa kwa kazi za katibu ambazo hazikuainishwa. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri basi atuainishie hizo kazi za katibu huyu ambaye tunasema hapa ni mwanasheria anayetambulika na uzoefu, lakini hatokua na kura kwa hivyo eneo hili lionekane.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni kifungu cha 7 kifungu kidogo cha 3 kinasema hivi naomba kunukuu. "*Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano maalum wakati wowote itakapoombwa na wingi zaidi ya nusu ya wajumbe".* Sijui mswada wetu wa kiingereza unasemaje, lakini hili neno anaweza linamhiyarisha lakini kiwepo kitu ambacho kinamlazimisha. Mwenyekiti ataitisha mkutano maalum wakati wowote itakapoombwa kwa wingi wa zaidi ya nusu ya wajumbe watakaokuwepo aitishe, sio anaweza kwa sababu tukisema anaweza ana hiyari hata kama wajumbe wamekua wengi akisema *OK*. Lakini Mwenyekiti aitishe mkutano ikiwa hiyo idadi ya nusu ya wajumbe

watakaokuwepo ataombwa kufanya hivyo, kwa hivyo hili neno ataweza Mhe. Waziri naona libadilike hili. Mhe. Ismail Jussa Ladhu anasema kwenye kiingereza imeandikwa *may* kwa hivyo tubadilishe sasa iwe *shall*.

Mhe. Mwenyekiti eneo jengine ambalo nimeliona linahitaji masawazisho pamoja na masawazisho mengine ambayo tayari kamati imeyapitia ni kifungu cha 19 kifungu kidogo cha 2 pana neno hapa limeandikwa muhuri maalum, kwa nini iwe muhuri maalum ina maana kuwa na mihuri miwili. Kutakua na ule muhuri wa kwanza uliotajwa kwenye kifungu cha kwanza lakini kutakua na muhuri maalum, sasa kidogo hapa nipate ufafanuzi, muhuri maalum huu unaokusudiwa ni upi *official* sio ule wa kawaida.

Kwa sababu katika kifungu cha kwanza kifungu kidogo cha 2(a) kinasema ni chombo kinachojitegemea chenye uwezo wa kuridhiwa na chenye muhuri wake unaotambulikana, sasa hapa tumesema muhuri maalum sasa huu ni tofauti na muhuri huu, kwa hivyo kutakua na muhuri maalum na muhuri wa kawaida kama ndivyo na muhuri ndio huo huo , laa kama tumekusudia muhuri maalum basi na hata kwenye kifungu cha tatu basi neno maalum lijitokeze, chenye muhuri wake maalum unaotambulika.

Kifungu chengine cha 11 nacho ningeliomba Mhe. Mwenyekiti, kiongezwe neno kwenye kifungu cha 11 maposho na malipo ya bodi ambapo kifungu kinasema kwamba. “Wajumbe wa bodi watapaswa kulipwa maposho na malipo kama inavyopendekezwa na bodi na kukubaliwa na Waziri, paongezwe neno jengine kati ya malipo na kama, ambapo itasomeka kwamba wajumbe wa bodi watapaswa kulipwa maposho na malipo mengine kama ilivyopendekezwa na bodi na ilivyokubaliwa na waziri.

Mhe. Spika, kifungu cha 13 kinasema. “Afisa mwenye mamlaka”. *Statement* inasema kwamba bodi itachagua watu watakaokua maofisa wenye mamlaka kwa mujibu wa madhumuni ya sheria hii. Mimi ningeomba hii watu watakaokua tuliondoe na badala yake paandikwe kwamba bodi itachagua maafisa wenye mamlaka kwa mujibu wa madhumuni ya sheria hii, kwa sababu hawa moja kwa moja watakuwa ni watu watakaokua. Bodi itachagua maafisa wenye mamlaka kwa mujibu wa madhumuni ya sheria hii.

Eneo jengine Mhe. Spika, ambalo kidogo ningependa nipate ufafanuzi ni katika hiki kifungu cha 13(3) b kimeandikwa hivi. “Afisa mwenye mamlaka pia atafanya yafuatayo, (a) imetajwa hatuna matatizo nayo lakini (b) kuandika ripoti alipoingia kwenye chumba cha mitihani kwa mujibu wa kifungu kidogo cha pili amegundua aina Fulani ya uvunjaji wa kanuni za mitihani. Sasa nilipokua napitia mswada huu nilikua najiuliza atamuandikia nani huyu Afisa kuandika ripoti ataiwasilisha wapi kwenye bodi au kwa mkurugenzi.

Kwa hivyo hebu Mhe. Waziri njoo utupe ufafanuzi hii ripoti, au ataandika ripoti halafu akae nayo sasa ningeomba sheria ionyeshe huyu afisa maalum atakapokwenda pale akikuta mambo kama haya yaliyozungumzwa ataandika ripoti sasa ripoti ile ataiwasilisha wapi, kwa hivyo ioneshe atakapopeleka hiyo ripoti yake.

Mhe. Spika, kifungu cha 14 kuanzishwa kwa kamati kinasema hivi naomba kunukuu. “Bodi inaweza kuanzisha kamaati kwa madhumuni ya kusaidia utekelezaji wa kazi zake.” Kamati zenyewe itakua kama ifuatavyo sasa hatuilazimishi hapa kusema bodi inaweza, wakati hizi kamati zilizokuwepo ni kamati ambazo lazima ziwepo na kwa sababu zimeshatajwa. Kwa hivyo ningeomba kuwe na mabadiliko hapa kwamba badala ya kuandika bodi inaweza inasema bodi itaanzisha kamati, hiyo bodi hiyo ikishaundwa itaanzisha kamati kwa madhumuni ya kusaidia katika utekelezaji wa kazi zake na kamati zenyewe zitakua kama ifuatavyo.

1) KAMATI TENDAJI
2) KAMATI YA MITIHANI

Sasa hizi Mhe. Spika, iwe ni kifungu cha 14(1) lakini kuwe na kifungu cha 14(2) kinachosema bodi inaweza kuanzisha kamati nyengine kama ambavyo itaona inafaa kila baada ya muda. Kifungu cha pili kinaipa mamlaka bodi sasa hivi za mwanzo ni kamati ambazo za lazima ambazo zitaanzishwa na bodi, lakini kifungu chengine cha pili hiki sasa bodi inaweza kuanzisha kamati nyengine kama ambavyo itaona inafaa kila baada ya muda ihiyarishwe sasa.

Lakini kutakua tena na kifungu chengine cha 3 ambacho kinasema wajumbe wa kamati watateuliwa na bodi, lakini kinajirejea kwa sababu huku tumeshasema, kifungu cha tatu ndio wajumbe wa kamati watateuliwa na bodi hiki kitafaa. Kwa hivyo kifungu cha 14 kitakua na 1,2 na cha 3.

Mhe. Spika, kifungu cha 15 (a) kuna neno hapa usimamizi nahitaji kidogo Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe kidogo tafsiri ya hili lililokusudiwa kwenye kifungu cha 15 (a). Kamati tendaji zitakua na kazi zifuatazo. Kufanya kazi za kawaida za kiutendaji katika usimamizi wa bodi sasa hili kidogo limenipa mashaka katika usimamizi wa bodi kidogo hii *statement* naona haijakaa sawa, sijui sheria iliyoandikwa kwa kizungu iko sawa au tafsiri imekosewa, uendeshaji kwa hivyo kidogo sio usimamizi na libadilishwe neno uendeshaji badala ya usimamizi.

Mhe. Spika, kifungu cha 17 ambacho kinazungumzia Mkurugenzi wa bodi kuna neno ningeomba liongezwe kwenye kifungu cha 17 kifungu kidogo cha pili (a) ambacho kinasema mtu hatoteuliwa kuwa Mkurugenzi isipokua awe ni mwenye angalau shahada ya pili katika fani ya elimu na uzoefu wa angalau miaka mitano katika fani. Sasa paongezwe neno fani hiyo isiishie fani tu miaka mitano katika fani hiyo kwa hivyo liongezwe neno hiyo halafu iendelee. Mimi hivi vigezo vya kielimu sina mashaka navyo pamoja na kwamba wenzangu wamejaribu kuuliza lakini mimi sina mashaka navyo.

Lakini kifungu cha 18(1) Mswada unasema kwamba kwa mujibu wa masharti ya sheria hii atawajibika kufanya kazi za kila siku za bodi, mimi kidogo sikuona kama imekaa vizuri. Mimi ningeomba ikae hivi lakini pia niongeze na kifungu kidogo cha pili, kwa mujibu wa masharti ya sheria hii Mkurugenzi atawajibika kwa bodi. Lakini kuwe na kifungu cha pili kidogo kitakachosema mbali ya kazi zake za kawaida Mkurugenzi atawajibika na kufanya kazi za kila siku za bodi.

Hiki kifungu cha 2 kilichokuwepo hapa Mhe. Waziri nakiona hakina maana tukifute hiki kilichokua kimetangulia ambacho kinasema hivi, Mkurugenzi atakua ni mjumbe wa bodi na atashiriki katika mijadala ya bodi na atawajibika kupiga kura kwenye maamuzi ya bodi au kwenye masuala yote yanayohusiana na bodi, haya tayari tumeshamtaja kwenye wajumbe wa bodi mmoja ni Mkurugenzi kwa hivyo akishakua mjumbe mle maana yake yeye atakua na haki ya kujadili, kupiga kura na mambo mengine yote ya bodi.

Sasa tukiweka kifungu hiki maana yake tunarudia rudia tumeshamteua kule Mkurugenzi kwamba ni mjumbe wa bodi kwa hivyo haki hizi ambazo tumezitaja pale zipo kwa mujibu wa sheria hii kwa hivyo kifungu hiki tukifute, badala yake tuongeze hicho kifungu cha pili hicho ambacho nimekipendekeza.

Kwamba kwanza mkurugenzi ajue moja kwa moja anawajibika kwa bodi kwa mujibu wa sheria, pamoja na kwamba anateuliwa na Rais na sheria kama hizo zipo kwetu hapa watu wanateuliwa na Rais lakini wanawajibika kwenye vyombo vyengine hasa kwa shughuli hizi za bodi. Kwa hivyo Mkurugenzi kwanza ajue kwamba moja kwa moja anawajibika kwa bodi na atakapojua anaweza kufanya kazi zake vizuri.

Lakini kifungu cha pili ambacho kitamueleza kwamba mbali ya kazi zake hizo za kawaida pia atatakiwa kufanya kazi za kila siku za bodi ambazo atapewa na bodi.

Mhe. Spika, kifungu cha 18(4) cha mwisho ambacho kinazungumzia timu ya uongozi inajumuisha Mkurugenzi na maofisa wengine wa bodi, kifungu hiki nakiona kama kinaning'inia kama kimechomekwa na kama hakina mshiko namuomba Mhe. Waziri kifutwe, hichi ambacho kinazungumzia timu ya uongozi inajumuisha Mkurugenzi na maofisa wengine wa bodi ambapo kwenye sheria nzima humu hakuna panapozungumzia timu ya uongozi na *composition* zake. Kwa hivyo nakihisi kama kinaning'inia laa kama utakuja kuona kina manufaa basi utatupa au utakipanga vyengine basi utatueleza.

Eneo jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 21(4) kama wenzetu wa Kamati wamekiona watanieleza, lakini mimi nimekiona kidogo kuna neno linahitaji kuongezwa naomba kukinukuu.

Kifungu cha 21 "(4) Bodi italazimika kwa muda ambao si zaidi ya miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha kuwasilisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa Bodi, ikijumuisha ripoti ya ukaguzi kwa kuhusiana na mwaka wa fedha pamoja na kuwasilisha mizania ya hesabu ya bodi kwa mwaka wa fedha."

Sasa itawasilishwa wapi. Naomba kuongezwe neno kwa "Waziri" na mwisho kuongezeke neno "mwaka wa fedha unapofika" na isomeke hivi:

"Bodi italazimika kwa muda ambao si zaidi ya miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha kuwasilisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa Bodi kwa Waziri ikijumuisha ripoti ya ukaguzi kwa kuhusiana na mwaka wa fedha, pamoja na kuwasilisha mizania ya hesabu ya bodi kwa mwaka wa fedha unaohusika"

Nadhani itakuwa inasomeka vizuri. Kwa sababu hapa imesema itawasilisha ripoti, lakini haijulikani wapi.

Mhe.Spika, eneo jengine ni Sehemu ya Nne Masharti Mengineyo, kifungu cha 22(i) naomba kukinukuu,

Kifungu cha 22(1) "Bodi inaweza kumtaka mtu yoyote anayefanya kazi za Bodi au ametakiwa kuendesha mitihani au kuchukua karatasi zozote za mitihani, kula kiapo mbele ya Mkuu wa viapo."

Mhe.Spika, tumeshuhudia hapa huko nyuma, tusilie kilio matangani kwamba kumekuwa na mambo yanayofanyika ya wizi wa mitihani, tunasema ukopiaji wa mitihani na mambo mengine ambayo yote haya chanzo chake kikubwa kinatokana na watu wa aina hii, ama wanaochapisha mitihani au wanaosafirisha mitihani au wanaohusika na kuivujisha mitihani. Sasa pasiwe na kitu ni kwamba unaweza, hawa wanatakiwa wale viapo wote. Kwa sababu hii kazi imeshakuwa pevu, kwa hivyo kwanza tuwalishe viapo hawa ndio tutakapowashtaki vizuri. Sasa badala ya hivi naomba sasa isomeke hivi,

Bodi itamtaka kila mtu anayefanya kazi za bodi, itamtaka kila mtu anayefanya kazi za bodi.

Sijui kama itakuwa pamoja na wao, maana na wao wanafanya kazi za bodi na wao walishwe viapo vile vile wote kuanzia bodi, kamati za utendaji, kamati za mitihani, wote wanaohusika na masuala ya mitihani wale viapo mbele ya mkuu wa kiapo.

Tujiridhishe katika hilo, pengine itakuwa ni dawa tutaogopa kuapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuvujisha, pengine itasaidia.

Kwa hivyo badala ya kuwambia bodi inaweza kumtaka mtu yeyote. Bodi itamtaka kila mtu ale kiapo pengine huenda ikasaidia. Tena na haya mengine mimi nakubaliana nayo yaliyoandikwa sina wasi wasi.
Jengine katika kifungu hiki cha 22(3) naomba kunukuu kinasema hivi:

Kifungu cha 22 "(3) Bodi itakaporidhika kuwa kumetumika utaratibu ambao sio wa kawaida unaotakiwa katika mitihani, Bodi inaweza kusimamisha au kuikataa mitihani hiyo au sehemu inayohusika na hilo."

Mimi nasema Mhe.Mwenyekiti, sheria yetu isiseme inaweza badala ya kuona yameshatendeka haya, badala ya kwamba itaweza isomeke kwamba bodi itasimamisha au kuikataa mitihani ile au sehemu inayohusika na hilo. Tuhiyarishe bodi hapa kama anavyosema Mhe. Jussa hapa tusitoe *lop hole* ya kisheria. Bodi ikishaona tu mambo haya yametendeka basi hatua zichukuliwe, kuwe na hatua za moja kwa moja zichukuliwe.

Lakini pia hata kifungu kidogo cha (4), nacho kuna neno hili limetumika kwamba Bodi inaweza kukataza kituo hicho, kupanga, kusimamia. Ni vyema bodi ikataze kabisa ambapo itakapotokea zaidi ya theluthi moja ya watihaniwa katika kituo cha mtihani kufanya mambo kinyume na masharti, bodi kukataza kituo hicho kupanga maeneo yake. Tusiseme inaweza, ikataze hasa kwa sababu kuna mambo ambayo yamekwenda kinyume na kanuni za utungaji na usimamizi wa mitihani yetu.

Mhe.Spika, mwisho ningeomba kifungu cha 23 Mhe.Waziri aje atupe ufafanuzi ambacho naomba kukinukuu.

Kifungu cha 23 "(1) Katika kutekeleza majukumu yake na kufanya kazi zake bodi inaweza kwa idhini ya waziri kuweka kanuni kuelezea kitu chochote kwa mujibu wa Sheria hii ambacho kinahitaji maelezo au ni muhimu au chenye kupasa …"

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla chini ya kifungu kidogo (1) Kanuni zinaweza kutungwa kuelezea mambo yafuatayo…"

Mhe.Spika, haya yanahitaji lazima kuwa na kanuni katika kuyaendeleza. Nilikuwa najiuliza Kanuni hizi za sheria hizi zitatungwa na bodi. Mara nyingi tunapopitisha sheria ili kanuni ziwe na nguvu, basi kanuni huwa zinatungwa na Mhe.Waziri. Lakini hapa tunasema kwa idhini bodi inaanza kwa idhini, ina maana Waziri anapowambia undeni kanuni kwa hivyo kama kuna marekebisho basi turekebishe, isiwe kwa idhini ya waziri, lakini kanuni zitungwe na bodi. Kanuni zote za sheria hii zitungwe na Mhe.Waziri anayehusika na wizara hii, sio waziri atoe idhini kwamba tungeni kanuni. Kuwe na maelezo kwamba waziri atatunga kanuni kwa ajili ya uendeshaji bora wa sheria hii.
Mhe.Spika, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono mia kwa mia Mswada huu wa sheria. Namuomba Mhe.Waziri mapendekezo ambayo nimeyapendekeza basi atakayokuwa hakuyachukua basi aje anipe maelezo au ufafanuzi zaidi, ili tuone sheria hii inakuwa ni bora na inaweza kusimamia zaidi masuala ya mitihani ya kwetu hapa Zanzibar, ambayo siku hizi imekuwa inalalamikiwa sana.

Mhe.Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mhe.Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe.Spika, na mimi kwa kupata fursa hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria wa Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe.Spika, niipongeze kamati kwa yale yote ambayo waliyoyaona na ikapendekeza, kwa hivyo ni jambo la msingi kwa sababu hii ni kamati yetu ya Baraza la Wawakilishi ni kamati za kudumu ambayo ni moja katika wajibu wa kisheria na kikatiba, ni lazima tuwe na kamati hizi ili kufanikisha shughuli za Baraza letu. Haya yote ambayo ilitoa kama ni mapendekezo, kwa hivyo Mhe.Spika, naomba Mhe.Waziri ayaone ni katika moja ya kuweza kuyasaidia katika majukumu yao ya kila siku.

Mhe.Spika, vile vile niwashukuru kama walivyoendelea wenzangu na Waziri na Naibu Waziri, kukaa pamoja na kujibu maswali hapa kwa ufasaha zaidi nawashukuru kwa hilo. Pia nitoe masikitiko yangu kwa Waziri kwa muda mfupi kwa kupata uhamisho na kwenda kuendelea na majukumu kwengine. Lakini yote ni kazi ambayo kama kawaida unapokuwa mtendaji mzuri, basi utapata sehemu nyengine pengine pale alipokwenda, pengine patakuwa na matatizo zaidi basi anaweza akayaondoa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie akafanya kazi vyema na huko.

Mhe.Spika, nikianza sehemu ya kwanza ambayo kuna jina fupi ya sheria hii. Niseme kama wenzangu walivyosema kwamba Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu ya Zanzibar lisizunguke sana hili jina tuliite tu “Bodi ya Elimu ya Zanzibar” badala ya kusema ya “Tathmini, vipimo” bora twende tu moja kwa moja kwamba ni Bodi ya Elimu Zanzibar.

Vile vile kwenye ufafanuzi kama walivyopita wenzangu niende kwenye mjumbe wa nafasi maalum. Hapa imeelezwa maana yake ni mtu ambaye kwa mujibu wa sheria hii, anatarajiwa kuhudhuria mikutano kutokana na nafasi yake katika Ofisi anayofanya kazi katika taasisi ya umma. Hapa Mhe. Waziri pananitatanisha sijaelewa huyu mjumbe kwa nafasi maalum atatoka wapi, au atakuwa ni muajiriwa wa moja kwa moja vipi, hapa sijapaelewa vizuri.

Mhe.Spika, niende sehemu ya hii ya kuanzishwa kwa bodi, nimeona hapa kuna kazi za bodi katika kusimamia na kukusanya na kuweka kumbukumbu za muendelezo wa utendaji wa wanafunzi. Maendeleo wanayopata wanafunzi kuhusiana na mitihani inayofanywa na bodi. Hili ni jambo la msingi kwamba bodi yenyewe itakuwa inapata kujua maendeleo ya wanafunzi wake.

Hili naliunga mkono na nasema Mhe.Waziri amefanya kazi kubwa kuona hili. Kwa sababu tunathamini hasa pale wanapokaa pamoja na taasisi mbali mbali kuona kuna haja sasa ya kuwa na bodi hii ili tuone kama Zanzibar tunakuwa na vyombo kama hivi vya maamuzi kuweza kujitegemea sisi wenyewe na kupandisha ile *grade* ya elimu yetu. Kwa sababu elimu ni kitu cha msingi na kwa kuwa tunakwenda katika mambo ya teknolojia ni lazima tuende na wakati ambao wenzetu sasa hivi wameshabadilika. Bodi hii itashughulika na mambo ya elimu ya lazima kwa hivyo si vibaya hata kutafuta chombo chengine cha juu zaidi ambacho kitashughulika na elimu ya juu.

Mhe.Spika, nikariri maneno ya mwanasiasa mkongwe kabisa aliyesema *education is a good weapon*, kwa hivyo ni lazima tuone elimu ni jambo la msingi kabisa. Elimu ni ufunguo wa maisha, kwa hivyo ni lazima tuwe na wasomi wengi na Wizara ya Elimu ndio yenye juhudi ya kusomesha, kwa hivyo wataalamu ni kuanzisha zile tafiti na kuona kwamba sasa tuna haja ya kuwa na vyuo vikuu ambavyo tutavisimamia wenyewe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe.Spika, niende kifungu cha 3 katika sehemu ya kuanzishwa kwa bodi kinachosema, itakapotokea mjumbe wa bodi kutohudhuria kikao, kwa sababu ya kutokuwepo Zanzibar au ugonjwa au kwa sababu nyengine inayokubalika. Kutoweza kutekeleza majukumu yale mamlaka inayohusika na uteuzi, inaweza kumteua mjumbe wa muda kushika nafasi yake, na mjumbe huyo kwa muda atachukua nafasi hiyo hadi atakaporejea, jukumu hilo kwa mjumbe husika na hadi pale ambapo muda wa utumishi wa mjumbe huyo katika bodi utakapokwisha au lolote kati ya hayo litakapotokea mwanzo.

Mhe.Spika, ni kweli unapokuwa katika bodi kwa sababu bodi itakuwa na mambo yake mbali mbali, kwa sababu kunakuwa na *koram* maalum ya wajumbe wa bodi, basi ni vizuri tukatizama ule uzito wa yule mtu ambaye hakuwepo na hakuweza kuweka mtu mwengine.

Kueleza bayana maslahi, ni vizuri vile vile kama sisi ni wanasheria ambao tunapitisha sheria hii, basi si vizuri kubana bana mambo ni vyema kuyaweka bayana ili tukaweza kujua ni kitu gani ambacho kinaendelea. Pale ambapo patakuwa hapakustahiki basi ni kazi yetu wajumbe, ili tuweze kuona ni namna gani ya kuwasaidia hawa ili kuwe na ufanisi zaidi wa bodi yetu, ili tuone namna gani tunajikwamua juu ya suala hili la elimu.

Mhe.Spika, kifungu 10(2), muhuri maalumu wa bodi hautowekwa popote kwenye maandishi, au hati yoyote iliyofanywa au kutolewa au kutekelezwa na bodi au kwa niaba ya bodi isipokuwa kuwepo Mwenyekiti, Katibu au mjumbe mwengine wa bodi, au muajiriwa mwengine wa bodi atakayeteuliwa kwa ajili hiyo.

Hapa vile vile sijafahamu muhuri wa aina gani, kuna mihuri ambayo tumeizoea wanasema *stempu* ya kawaida kwa mfano muhuri unaandikwa jina la mtu na akabandika. Huu muhuri mimi nimefikiria ni ule muhuri kama kwenye nembo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unamkuta Adam na Hawa. Basi kama vile basi ule muhuri uendane na ile hali yenyewe, ya kwamba bodi ni ya elimu, basi kuwa na angalau picha zinazoonesha kwamba ni mwanafunzi au kitabu au kitu chengine kinachohusu mambo ya elimu.

Mhe.Spika, niende kwenye kifungu cha 14 ambacho kinasema kuanzishwa kwa kamati. Kamati (a) itakuwepo Kamati ya Mitihani, Kamati Tendaji na kamati nyengine kama ambavyo bodi itaona inafaa kila baada ya muda. Hili ni jambo la msingi vile vile na kwa sababu nia na madhumuni ni ile ile ya kukuza elimu. Kwa hivyo, ni lazima kamati zenyewe ziwe ni zenye kufuata misingi ya utawala bora, ziwe wazi, ziwe na uwajibikaji na ziwe wazi zaidi.

Mhe.Spika, niende na suala jengine la hesabu za bodi za ukaguzi. Bodi itasimamia uwekaji wa hesabu sahihi za fedha na kumbukumbu zilizo sahihi, kuhusiana na hesabu sahihi za fedha na kumbukumbu ambazo zinawekwa kwa mujibu wa miongozo inayotolewa na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hili ni jambo la msingi kabisa, pahala pakiwa na pesa ni lazima kuwe na taratibu na ziwe zinafuatwa.

Vile vile ziwepo taratibu za matumizi ya fedha za serikali, bila ya hilo kutakuwa na udhaifu, na pesa zitapotea bila ya malengo ambayo yamekusudiwa.Kwa muda huu hata mdhibiti mwenyewe ameshabadilisha namna ya ukaguzi. Kuna ukaguzi mpya ambao tunakwenda kwamba nayo Zanzibar ni sehemu ya dunia kwa hivyo ni lazima tuende na mabadiliko ambayo yanatokea ulimwenguni, tusibakie nyuma. Sasa hivi mdhibiti yupo katika ukaguzi wa kukagua kwa njia ya *value for money* na mambo ya kutumia kompyuta, kwa hivyo ni lazima tufuate masharti ya serikali.

Mhe.Spika, kwa niaba ya jimbo langu la Amani naunga mkono mswada huu na sisi kama wawakilishi tuuchangie mswada huu, na naomba tuupitishe kwa faida ya nchi yetu na faida ya watoto wetu ambao ndio wajenzi wa taifa hili hapo baadae.Nakushukuru sana Mhe.Spika.

Mhe.Aballa Moh'd Ali: Ahsante Mhe.Spika, na mimi mchana huu kunipatia fursa ya kusema machache kuhusu Mswada uliokuwepo mbele yetu.

Mhe.Spika, nilifurahi nilipopata gazeti la serikali na nikajenga imani kwamba sasa tumeanza kubadilika. Lakini kinachonisikitisha yule muasisi wa mambo haya anaondoka, sasa sijui utekelezaji wake utafanikiwa kiasi gani.

Mhe.Spika, hivi sasa kilio cha Wazanzibari au midomo yote mingi inazungumzia masuala ya elimu hasa baada ya matokeo. Sasa sijui Mhe.Waziri aliyaona hayo, na sijui Mswada huu utanyamazisha masuala ya wananchi wanayotuuliza. Ningependa au ningeshukuru kwamba mwaka unaofuata nitakuta katika gazeti la serikali Mswada kamili utakaotuwezesha kuwa na mitihani yetu, labda hapo ndio tutakapomaliza vilio vya wananchi wetu.

Mhe.Spika, baada ya kuusoma kidogo nilipata wasi wasi.Kwa sababu miezi mitatu tu iliyopita nyuma tulipata hoja binafsi. Hoja hii ilikuwa ni ya wanafunzi ambao walishindwa kupata mkopo kwa ajili ya maendeleo ya Elimu ya Juu. Nikapata wasi wasi kwamba je, Mswada huu haukuja kwa sababu ya kuwawekea vikwazo wanafunzi wetu? Kwa sababu hii ni kama TBS elimu itapimwa, lakini kwa kipimo gani? Labda ni kikwazo cha kuwafanya wanafunzi wasiwe na uwezo wa kupasi na kuwa wengi, kwamba Wizara haitoweza kuwalipia kuendelea na masomo yao ya juu. Sasa tuweke vipimo hapa kati kati ili wengi wasite site huku nyuma, ili watakapokuja juu wawe kidogo, ili wizara tupate kuwasomesha. Sasa mimi nina wasi wasi na suala hili, sasa sijui ndio nia ya wizara hiyo au labda nia ni kuboresha elimu.

Mhe.Spika, elimu kila mmoja anajua umuhimu wake katika nchi.Sisi Zanzibar nafikiri tupo katika watu ambao wa mstari wa chini sana kwa kiwango chetu cha elimu. Ili tuwe na kiwango kizuri, na hivyo vipimo viweze kufanya kazi kuna mambo mengi sana ambayo tunahitajika tuyaangalie. Hivi sasa wenzetu nchini Kenya, ambao nafikiri kwa kanda ya Afrika Mashariki kiwango chao cha elimu kipo juu, tayari wameshaanza kuangalia mfumo wao ukoje.Naona wataubadilisha wakati wowote. Sisi mfumo wetu upo muda mrefu, nafikiri nao unahitajika kufanyiwa marekebisho ili kuongeza kiwango cha elimu.

Nasikitika katika wanafunzi waliopata *disco* Chuo Kikuu cha Kiislamu pale Morogoro wengi ni Wazanzibari. Labda naweza kusema karibu wanafunzi 200 na sisi tumo katika kundi hilo. Hii inatokana na kuwa kiwango chetu ni kidogo. La msingi mswada huu uwe na nia hiyo, kwamba tunatafuta kiwango chetu cha elimu kiwe kizuri zaidi na zaidi, na sio kuja kuweka tu. Kipimo tunacho na naomba wizara wawe na malengo zaidi kulikoni kuweka mabodi ambayo kiwango cha elimu kitakuwa kipo pale pale.

Mhe.Spika, najua muda ni mdogo lakini sina mengi ya kusema. Katika kifungu cha 5 Mswada huu unasema:

Kifungu cha 5 “kazi za bodi ni kuweka utaratibu maalum wa mitihani, majaribio na upimaji, lakini kwa mujibu wa mitaala ya Zanzibar.”

Sisi tutakuwa bado tunaendelea kuwa katika mitaala ya NECTA ambayo inatungwa Tanzania Bara.Lakini huku tutakuwa tuna mitihani yetu ambayo itakuwa inafuata mitaala yake. Nahofia kwamba sisi tukiwa na mitaala yetu hapa Zanzibar peke yetu, lakini tutakapoingia elimu ya juu tutakuwa na mitaala mengine ambayo itatungwa mitihani yake na watu wengine. Sasa sijui tutawawezesha wanafunzi wetu kuwa na ufahamu kiasi gain, au tutakuwa na kipimo kiasi gani cha kuweza kujua mitaala ile itasaidia vipi katika kukuza kiwango hicho cha elimu cha wanafunzi wetu wa Zanzibar. Ningependa Mhe.Waziri atakapokuja hao walioleta sera hii labda wangetueleza.

Pia kifungu cha 5(f) pia kimezungumza muundo. Katika kifungu hicho kinasema kuandaa miongozo kwa skuli na vyuo. Vyuo ni neno ambalo Waarabu wanasema liko *shaamil,* limechukua mambo mengi sana.Lakini Mswada huu unakusudia elimu ya msingi.Sasa je, wanaposema vyuo wanakusudia chuo gani. Wanakusudia vyuo mpaka vya qur-an navyo vitakuwemo, ukisema chuo na Chuo Kikuu pia huwa tunaki *consider* katika mpango wa vyuo au vyuo vya elimu fulani tu Mbweni labda ya Chuo cha Kiislamu.

Naomba watakapokuja watueleze kidogo nini wamekusudia hapa vyuo, kwa sababu Mswada huu tunajikita zaidi na elimu ya msingi na vyuo vya Zanzibar.Lakini vyuo pia tunaingia katika vyuo vikuu.

Mhe.Spika, katika kipengele cha 17 kumeelezwa Mkurugenzi, kwamba kutakuwa na mkurugenzi, lakini mkurugenzi huyu awe na shahada ya pili na uzoefu wa miaka mitano. Lakini (2) awe na shahada ya kwanza na uzoefu usiopungua miaka kumi. Mimi lugha za kisheria sizifahamu, lakini najenga imani kwamba hapa tushaipa hii shahada ya kwanza na uzoefu wa miaka miwili kama tumeifananisha ni sawa sawa kuwa na shahada ya pili, vyenginevyo isingekuwa hivyo.
Mimi ningeomba kipengele hichi kikasomeka mara moja tu.Kama ni shahada ya pili iwe ni shahada ya pili, kama ni shahada ya kwanza iwe ni shahada ya kwanza. Tusihalalishe mtu kuwa uzoefu wa miaka kumi akawa tayari ndio akawa na shahada ya pili, kwa ninavyofahamu mimi.Lakini lugha za kisheria kila mmoja anakuwa na tafsiri yake.

Mhe.Spika, labda niulize tena Mswada huu uliokuja hapa je, katika kupima na kutathmini skuli za binafsi nazo zitaingia katika mfumo huu, au wao hawatokuwemo katika mfumo huo.Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono.

Mhe.Spika: Waheshimiwa wajumbe muda uliobaki ni mchache, nafikiri hautotosha kwa mjumbe kumuomba achangie.Kuna tangazo moja kabla ya kuakhirisha kikao.Ndugu zetu AZAKI ambao wanafanya maonesho yao hapo nje, wanatuomba kwamba jioni mnamo saa 10 wanategemea maonesho hayo yafungwe.Kwa hiyo Wajumbe tunaombwa tuhudhurie katika ufungaji huo ambapo mgeni rasmi atakuwa Mhe.Ramadhani Abdalla Shaaban.Kwa hiyo tumuunge mkono katika shughuli hiyo ya kufunga maonesho ya AZAKI.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe kikao nakiakhirisha hadi saa 11 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi yakuweza kuchangia angalau japo kidogo katika Mswada wa Marekebisho ya Elimu ambayo na mimi nitajitahidi kutoa mawazo yangu katika suala hili.

Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru Mhe. Waziri katika kuandaa mswada huu ambao ni mzuri ingawa ni mrefu, lakini una mantiki ndani yake na una mambo mengi yaliyoelezwa ndani yake na unaweza kukidhi haja.

Mhe. Spika, ni vyema kama vile walivyosema wao kwamba inaonesha kua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa miaka mingi ya nyuma iliyopita, Wizara kidogo ilikua imejisahau kua wana wajibu wa kuweka marekebisho au kupitia baadhi ya mambo ya sheria katika kuleta ufanisi wa elimu. Inaonesha katika shughuli zote za Wizara ya Elimu kwa muda mrefu ilikua hakuna jambo maalum la kuweza kuwaongoza katika suala zima la mambo ya mitihani.

Mhe. Spika, hata hivyo mitihani itakua inakwenda kutokana na mtaala wenyewe ambao tayari kwa wakati ule umetayarishwa, ingawa tunajua kwamba mitaala ni baada ya kila miaka 10 wanatengeneza ili kuboresha ile mitaala na kuifanya iwe kwa mujibu wa wakati ulivyo. Ndio maana kwa muda huu wakaona hawana namna yoyote Wizara ya Elimu wawache kufuata zile kanuni za zamani ambazo wakiziwacha na wakaona kwamba kanuni walizokua nazo hazikuweza kukidhi ile haja. Mhe. Spika, kutokana na hayo ndio wakatayarisha hiki chombo, chombo ambacho tumeletewa hivi sasa cha kisheria ili kiweze kudhibiti mambo yote ya kitaaluma na wataalamu wake.

Mhe. Spika, mimi niseme Wizara ya Elimu imefikiria jambo muhimu ni zuri na ni jambo la msingi katika kuifanya elimu hii iwe bora. Lakini katika yote hayo huwezi kufanya kitu bila ya kuweka sheria, na huwezi kuweka sheria bila ya kua na kanuni. Ningelimuomba Mhe. Waziri aweke kanuni ambazo zitaweza kukidhi mswada huu.

Mhe. Spika, suala zima linalozungumzwa hapa ni hiki chombo, chombo hiki ni hii bodi tunasema kwamba ni bodi inayoweza kupima na kutoa tathmini yote. Kwa kweli Mhe. Spika, tumeiona hali ya Bodi ya Elimu mimi nasema ni lazima iwe na watu wa kuweza kuisimamia kwani ni chombo kikubwa sana, na ni lazima kiwe na wataalamu wengi. Mhe. Spika, hapa tumeona hali halisi kwamba chombo hiki kimepangiwa Mwenyekiti wake, ambaye Mwenyekiti huyu atakua amechaguliwa na Rais. Vile vile tumeona katika chombo hiki ni lazima kiwe na Wakurugenzi na hapa wamejitahidi kuona wameingiza aina mbili za Wakurugenzi. Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari na Mkurugenzi vile vile wa taasisi za elimu. Mhe. Spika, hawa watu wawili ni muhimu sana kuwemo katika chombo hiki, na umuhimu wake unaojuulikana kutokana na taaluma na elimu waliyonayo hawa wanaweza kulifanikisha suala hili likawa bora zaidi.

Mhe. Spika, vile vile utaona katika muundo huu haukua mbaya wameweza kumshirikisha na mkaguzi mkuu ambaye atakua ni mtu ambaye ana uelewa mkubwa wa shughuli zote za elimu. Kwa sababu yeye ndiye anayepita akikagua chini ya wakaguzi wake wanaokagua na kuona hali halisi ya muundo mzima wa shughuli za maendeleo ya elimu pamoja na shughuli nzima za mitihani ambayo inafanywa na inavyopimwa na matokeo yake. Kwa hivyo, hapa hawakukosea kumuweka mkaguzi na yeye ataweza kutoa mchango wake mkubwa katika suala zima la chombo hiki chenye muundo wa bodi.

Mhe. Spika, vile vile wameweza kujali jumuiya mbali mbali jambo ambalo mimi nalifurahia kwamba hizi jumuiya siku zote zinaanza kupiga kelele, kwamba mnapofanya mambo sisi hamtushirikishi. Lakini hapa mimi nimshukuru Mhe. Waziri kaweza kufikiria jambo la muhimu na kuweza kukiunda hiki chombo ambacho mbali wale walioko katika Wizara, lakini pia kuingiza watu ambao wako katika jumuiya mbali mbali. Mhe. Spika, hapa tumeona jumuiya za walimu, jumuiya iliyosajiliwa na watu wenye ulemavu bahati nzuri na wao wameingizwa kwani kila siku wanasema hawapatiwi nafasi. Mhe. Spika, hata hivyo baada ya jumuiya mbali mbali ambazo zimetajwa hapa pia ni muhimu na wao kuweza kutoa mchango wao, hilo ni jambo zuri sana.

Mhe. Spika, pia hawakuwasahau wawakilishi katika sehemu ya Baraza la Mitihani la Taifa lakini la Zanzibar, ningemwambia Mhe. Waziri hapa umesahau huyu wa Unguja na yeye hayumo, naona wa Bara tumemuona hapa panasema mwakilishi wa Bara wa Baraza la Mitihani la Taifa. Mhe. Spika, mimi naomba na huyu wa Unguja na yeye awepo asiwe peke yake huyu, kwa sababu bwana huyu mwakilishi wa hapa wa Baraza la Mitihani la Zanzibar ni mtu muhimu hivyo ni lazima awemo katika chombo hiki.

Mhe. Spika, hapa imetajwa kwamba pamoja na hayo kuna hizi *private school* pia na wao wanapata nafasi ya kuingia kuunda chombo hiki na kuweza kutoa mawazo yao, kwa sababu kule katika skuli za binafsi kuna walimu, wanafunzi na mitihani pia inayofanywa. Lakini hapa ingawa hatujaambiwa katika maelezo haya kwamba hizi skuli za binafsi je, katika suala hili la chombo juu ya kudhibiti au kusimamia mitihani na wao watakuwemo au ni skuli za Serikali peke yake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie pamoja na hili tunaloliandaa lakini pamoja na skuli za binafsi pia watashirikishwa. Mhe. Spika, katika hilo tumeona uzuri wake na mimi nafikiri bodi hii itakua ni bodi iliyokua ni nzuri na ambayo itaweza kuleta faida.

Mhe. Spika, vile vile hapa tunaambiwa patachaguliwa watu wengine kwa mfano hapa imetajwa Mwenyekiti. Mhe. Spika, ufafanuzi hapana hapa katika masuala haya kifungu cha 3 wajumbe wa bodi watamteuwa mjumbe mmoja miongoni mwa wajumbe kua Mwenyekiti. Hapa kidogo haijajieleza vizuri ningelimuomba Mhe. Waziri huyu Mwenyekiti ni nani, huyu anataka kuunda kamati ndogo katika bodi hii, kwa sababu huku tayari Mwenyekiti yupo. Lakini huyu mwengine ambaye anasema wajumbe wa bodi watamteuwa mmoja kuwa ni Mwenyekiti miongoni mwao.

Mhe. Spika, hapa kuna kamati ndogo ndani yake inataka kuundwa lakini hapa haikuelezwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie zaidi. Vile vile afisa wa sheria atakua ndie katibu wa bodi na uwezo wake umeshatajwa kwamba lazima uwe mkubwa mwenye shahada ya sheria katika chuo chochote kinachotambulika, hapa Mhe. Spika, sio mbaya.

Mhe. Spika, pia imeelezea kwamba afisa wa sheria huyo hatokua na kura katika maamuzi ya bodi. Mhe. Spika, hapa ningelimuomba kwa nini huyu hana kura na yeye huyu ni katibu kuna kitu cha msingi hapa cha kumzuia huyu katibu asipige kura. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri akija atueleze kwa nini huyu hatokua na kura.

Mhe. Spika, bodi hii ambayo ina hawa viongozi ni muhimu sana, na tunategemea kwamba hawa ndio watakaokua wasimamizi wa kuiendesha hii bodi. Lakini ningelimuomba Mhe. Waziri aangalie kwamba huu mchanganyiko uliomo humu ndani wa viongozi mbali mbali pawe na *coordination* nzuri miongoni mwao. Kwa sababu humu mnakua na Wakurugenzi na watu mbali mbali kwa hiyo katika ile michango ambayo inayotolewa kwenye bodi pawe na *coordination* nzuri isije ikaleta matatizo ndani ya ile bodi kuonekana mmoja ana elimu zaidi na mmoja hana elimu kama ile ambayo imetajwa hapa. Kwa hivyo, ni lazima papatikane mashirikiano ya kutosha ili kuweza kufanikisha yale madhumuni hasa ya bodi hii.

Mhe. Spika, katika kazi ya bodi tumeelezwa hapa kwamba bodi hii itakua na kazi kubwa ya kuweza kusimamia shughuli nzima za uongozi au kuwafanyia mazuri wanafunzi ili waweze kupata maendeleo, katika suala la upimaji kwa mambo ya mitihani utendaji wao na viwango vyao vya elimu.

Mhe. Spika, pia tumeona katika muundo huu Wizara ya Elimu hapa imejipa majukumu makubwa sana, na tunapenda Wizara ya Elimu ihakikishe kwanza katika muundo huu wameweza kuthibisha kama vile wanavyotueleza katika maelezo yao kua suala hili litakua ni la msingi, suala hili litakua ni la sekondari, suala hili litakua ni la vyuo. Kwa hivyo, hapa ni kazi kubwa sana kutengeneza mambo haya mpaka yakatulia sawa sawa na ikawa ile tuliokusudia lengo letu ni kuleta ufanisi katika upimaji na katika taaluma za kujifunza zionekane nzuri. Hapa pana kazi kubwa sana.

Mhe. Spika, mitaala yao ya msingi iko tofauti na mitaala ya sekondari ni tofauti na elimu ya juu. Lakini inavyoonesha katika utaratibu huu wa bodi hii tuliyopewa hapa mara hii, inaonesha haya ni mambo ya *internal* kwa Unguja, ingawa imetaja ni elimu ya juu. Hapa Mhe. Waziri akija aje atueleze hili suala la kurekebisha haya dhamira hasa ni ya ndani tu au mpaka dhamira hii ni ya nje, hapa tunataka maelezo kidogo hali itakua vipi.

Mhe. Spika, ninachofikiria mimi kitu kikubwa ni kwamba utaratibu utakua vipi katika vyuo hapa hatujaelezwa. Je, utaratibu huu katika kupima ukapatikana ufanisi baada ya mitihani yao utakua mpaka katika vyuo?

Mhe. Spika, mitaala ni kitu muhimu sana pia nataka nimuulize Mhe. Waziri katika hii mitaala ina muda gani, ni ile ambayo ilioko katika kipindi cha miaka kumi au imeshapitiwa na miaka kumi au ndio tuseme badala ya kuona tunataka tuende haraka katika mambo yetu tuweke mitaala baada ya kila miaka mitano. Mhe. Spika, mimi nafikiri hata mtu tuseme kwa mfano aliyesoma mambo ya *chemistry*, *physics* na *biology* miaka ya nyuma ya 50 haiwezekani sasa hivi ukamwambia nakuletea *paper* ya mtihani ifanye, basi haifanyi hata kidogo. Mhe. Spika, kwa sababu kila siku kuna mabadiliko katika elimu na binadamu yeyote ni maendeleo, hivyo kama binadamu sio maendeleo haiwezekani kumpa mtaala ambao una umri mkubwa. Je, Wizara bado inaendelea kusimamia kwenye miaka 10 ya kila mtaala au itapunguza itaweka mitaala ya miaka mitano mitano ili iwe bora zaidi. Mhe. Spika, hilo bila shaka Waziri atakapokuja aweze kutueleza bado wangali na msimamo ule ule wa miaka 10 au wataendelea kufanya miaka 5 au watafanya vyovyote watakavyofanya.

Mhe. Spika, katika suala hili la mitihani ni *corruption* ndani ya nchi naweza kusema hivyo, *corruption* hii inaweza kua *internal corruption* kwa sababu mtihani ni mtihani, vipimo ni vipimo katika kumpima mwanafunzi kutokana mafanikio yake. Mhe. Spika, tunaamini kwamba wanafunzi hawako na akili za namna mmoja, kila mwanafunzi hua anakua na akili yake. Kuna wanafunzi ambao ni wa pole katika kufahamu, kuna wanafunzi kati na kati, kuna wanafunzi ambao mwalimu akiingia darasani akisomesha na anapotoa mitihani wengine wanafahamu haraka haraka. Je, hili suala limewekwa vipi ndani ya skuli zetu za msingi, skuli zetu za sekondari na vyuo.

Mhe. Spika, tuangalie muundo au msimamo wa Wizara ya Elimu mpaka hivi sasa, elimu ya sasa hivi labda ni elimu ya kusema ndani ya Wizara hii ni kumpata mtu akajua kusoma na kuandika. Sawa kama nia ndio hiyo ya kusoma na kuandika basi tunajua kusoma na kuandika, lakini nafikiri sio mwisho wa lengo. Mhe. Spika, tuna malengo sasa hivi ya kutaka wanafunzi wetu waweze kua mafundi wakubwa katika elimu ya sayansi. Hivyo, je katika Wizara ya Elimu imeweka huo muundo wa kuwafanya wanafunzi kwenye vipimo hivi vya mitihani ikaanza kuwabagua mbali mbali kuwaweka kama ilivyosema akifika darasa la saba anampeleka michipuo, akifika darasa fulani anampeleka darasa fulani. Hicho ni kipimo cha kuona wale ambao wanapata nafasi za juu.

Mhe. Spika, je wale ambao Mhe. Waziri wanapata nafasi za kati kati ambao hawakwenda katika michipuo na sehemu nyengine hapa mtakwenda vipi katika kuwapima wanafunzi. Lengo hasa ni nini? Ni kutaka kuonekana tu kwamba tunafanya, tunawapima wanafunzi yanapatikana matokeo au kutakua na *assessment* maalum kwamba kwenye mitihani ya mara hii tumeweza kuona kwamba tuna mategemeo baada ya miaka ijayo tutapata wanafunzi wengi wa somo la sayansi, au tutapata wanafunzi wengi wa somo la *art*. Kwa sababu sasa hivi *competition* Mhe. Waziri nataka nikupe hiyo taarifa kama hunayo sio ndio tulioko huku tunaojua na tunafahamu kwamba katika mitihani yote ambayo inafanywa hivi sasa sehemu kubwa ya watoto wetu wanapasi katika masomo ya *art* kuliko masomo ya sayansi.

Mategemeo yenu katika Wizara mnawaweka kidogo hamtaki kuwavunja moyo na mnajua sehemu kubwa ya wanafunzi ni wale wa *art*, kuliko wale wa sayansi. Kwa hivyo, huku kupima tunatathmini nini? Hivyo, watoto wapate maksi za juu au kuna lengo maalum mnafuatilia, hebu twambieni hapa hili lengo la kutathmini mnatathmini kitu gani. Mnatathmini muwaweke wanafunzi kwa *groups* zao kwamba hawa ni wa sayansi, hawa ndio watakaokuja baadae sekondari na chuo kikuu. Kwa sababu katika kuandaa kitu lazima uwe na malengo ambayo yanajuulikana malengo yake hasa ni nini.

Mhe. Spika, unajua kuwapima wanafunzi katika mitihani, kuna mtihani wa darasa wa kuweka *assessment* mwanafunzi amefanya kazi katika darasa unampa tano juu ya kumi, ile ni tathmini tayari uwezo wake ni tano, unampa nne juu ya kumi ile ni tathmini tayari ya mwanafunzi uwezo wake ni nne juu ya kumi au kumi juu ya kumi. Mhe. Spika, katika lengo la kufanya hivyo nini hasa dhamira, dhamira ni kuonesha kwa mwanafunzi anapata maksi za juu au kuna lengo katika Wizara kwamba inakusudia mwaka huu katika kuwapima tunataka tujue angalau

mafanikio ya baadae kwamba sekondari zetu na vyuo vyetu tuwatayarishe tupate wana sayansi wengi zaidi. Mhe. Spika, mimi nasema meli bila ya kua na rada haiwezi kuona mbele, hakuna hiyo. Kwa hivyo, nataka tujue hasa tunakusudia nini, tunalenga wapi katika kutathmini. Mhe. Spika, mimi nataka tuambiwe hasa lengo la kuwapima wanafunzi tunawapima kwa ajili gani, hili tuambiwe ili tuweze kuelewa.

Mhe. Spika, suala la mitihani nilisema zamani, kama suala la mitihani ni *corruption* katika nchi, hasa hii mitihani ambayo tunaifanya hapa, hili ni suala la ndani ya Zanzibar sio nje ya Zanzibar. Lakini kama hili linafanywa ndani ya Zanzibar pia linaleta *corruption* kwa wazee jinsi wanavyofanya mitihani na wanavyopasi mitihani yao. Lakini hata hivyo watoto hao watafikia kiwango wanafanya mitihani ya *form four* ambayo ni mitihani ya kitaifa wanafanya kutoka nje na matokeo yake yanakuja kutoka nje.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri mara hii matokeo ya mitihani ya wanafunzi tumeona matokeo yake ni kilio kikubwa kwa wazee na mmewaweka katika giza au njia panda hawajui nini la kufanya, pia hakuna maelezo kwa wananchi yaliyotolewa. Mhe. Spika, kwa kweli mitihani ya safari hii imeleta kilio kikubwa sana, tumezisikia skuli nyingi hapa zimefutiwa matokeo ya mtihani tena kwa mujibu wa taratibu zao labda walikua na *by-laws* kwakusema kwamba mwanafunzi akigunduliwa amekopia basi atawekwa nje kwa muda miaka mitatu ndio afanye tena mtihani. Mhe. Waziri suala hili la kuwaambia watoto wetu mtihani huu unafanywa huko na wao ndio wanaotoa majibu ya watoto wetu, kwa kweli kile kimekua kilio kikubwa sana na wazee mpaka hii leo hawako radhi kwenye suala hili na skuli nyingi zimekua *disappointed* kwenye suala hili. Mhe. Spika, ina maana labda Wizara ya Elimu pengine haikufuatilia au imelikubali hili suala moja kwa moja bila ya kufuatilia au imechukua kwamba samaki akioza mmoja ndio wameoza wote.

Mhe. Spika, jaalia mtoto mwanamke ambaye sasa hivi ana umri wa miaka 15 au 16 unamwambia akae miaka mitatu baadae, haya mtoto huyo miaka mitatu si atakua ameshaolewa huyo kweli ndio atasoma tena. Hebu mimi naomba hizi *by-laws* zirudiwe angalau unamwambia mtoto nakufutia matokeo mara hii basi mwaka ujao ufanye mtihani tena.

Mhe. Spika, naona unanitizama sana kwa muda wako na mimi nina mengi lakini nakushukuru Mhe. Spika, kwa kweli mimi naunga mkono kwa sababu mswada huu tayari umeshapitiwa pitiwa na taarifa nyingi zishachambuliwa kipengele baada ya kipengele, isipokua mimi nilikua natoa mawazo au fikra za jumla jumla kuhusu masuala haya. Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi naunga mkono mswada huu mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia machache juu ya mswada huu ulioko mbele yetu. Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kuweza kusimama hapa mbele yenu, pia natoa mkono wa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha swahiba wangu mpenzi aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu (Mhe. Salim Amour Mtondoo).

Mhe. Spika, moja kwa moja sasa niingie katika mswada huu kwa kuanzia kabisa naanza katika sababu na madhumuni. Tukiangalia sababu na madhumuni ya mswada huu ni kutunga sheria ambayo itaanzisha chombo cha kudumu kinachotambulikana na imara cha kushughulikia masuala yanayohusiana na mitihani Zanzibar. Kwa hivyo, kutokana na maelezo hayo ya madhumuni na sababu basi nianze moja kwa moja katika kifungu cha 1 cha mswada huu.

Mhe. Spika, kifungu cha 1 cha mswada huu kinasomeka kama ifuatavyo:-

“Sheria hii itajuulikana kama Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar 2012 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika gazeti rasmi la Serikali”.

Mhe. Spika, kifungu hiki mimi ndio nina mashaka nacho sana, hapa moja kwa moja ilikua mswada useme wazi kwamba sheria hii itajuulikana kama Baraza la Mitihani la Zanzibar. Hapa hapana kificho Mhe. Spika, tangu juzi wananchi wanasema Baraza la Mitihani la Zanzibar linaanzishwa sasa, kila mtu anasema tutaokoka sasa hivi. Kwa hivyo, mheshimiwa mimi naomba sana kwamba hapa hakuna kificho kwa sasa wakati umefika kua na Baraza letu la Mitihani la Zanzibar. Mhe. Spika, naomba kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na sheria hii ibadilishwe jina moja kwa moja iitwe Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile nije kwenye kifungu cha 5 kazi za bodi kinasomeka kama ifuatavyo:-

“Kuweka utaratibu maalum wa mitihani, majaribio, upimaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyafanya kwa mujibu wa mtaala wa Zanzibar”.

Mhe. Spika, hapa kifungu hiki kina matatizo kidogo, na matatizo yake makubwa kwamba kuna tofauti kubwa sana ya wanafunzi ambao wa madarasa ya chini ya msingi wa Tanzania Bara na wale wa Zanzibar. Tukiangalia mtaala wetu wa elimu wa hapa katika kiwango cha msingi mpaka darasa la saba, basi Tanzania Bara wanatumia mtaala wao wa elimu na hapa Zanzibar tunatumia mtaala wetu wenyewe. Mhe. Spika, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa uchunguzi uliofanywa kwamba uwezo wa wanafunzi wetu wanapoanza kuingia darasa la 9 unakua mdogo sana.

Kwa hivyo, Mhe.Spika, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri hapa, tukapaangalia zaidi na tukaangalia tunakwenda na mtaala upi, ikiwa tutakwenda na ule wa Tanzania Bara moja kwa moja katika elimu ya msingi, ama tutakuwa na huu huu, lakini tunataka vile vile ufanane na ule kutokana na kwamba tukiingia daraza la tisa wanafunzi wetu hapa kunakuwa na tofauti kubwa sana ya ufahamu juu ya masuala yanayohusiana na elimu.

Mhe.Spika, pia tuangalie kifungu cha 14 kuanzishwa kwa kamati na wajumbe wa kamati. Hapa mimi nina swali dogo tu niulize. Katika wajumbe wa bodi moja kwa moja wameoneshwa watatoka wapi, lakini hizi kamati tatu wajumbe wake sijui watatoka wapi. Pia Mhe.Spika, hili Mhe.Waziri atakapokuja atueleze kwamba wajumbe hawa watakaoteuliwa watakuwa na sifa zipi.

Vile vile Mhe.Spika, kifungu cha 22(1) kinachohusiana na masuala ya viapo, makosa na adhabu. Kwa mujibu wa kifungu hiki kuna makosa mengi ambayo yameainishwa hapa yanahusiana na ukiukwaji wa taratibu za mitihani, na adhabu iliyowekwa endapo mtu atathibitishwa kutenda kosa, basi atafungwa mwaka mmoja jela ama faidi ya shilingi milioni moja ama zote mbili. Sasa tukiangalia hapa mitihani ni miongoni mwa siri za serikali na tukiangalia katika sheria nyengine ambazo zinazungumzia juu ya masuala ya siri za serikali adhabu hii ya mwaka mmoja hii ni ndogo sana, kwanza kutokana na ule uzito wa jambo lenyewe.

Mtihani kwa mfano unapovuja tu unaweza kuitia serikali hasara kubwa sana, kwa hivyo hasara yote ya mamilioni ya pesa halafu mtu pengine afungwe jela mwaka mmoja kwa jambo ambalo amelifanya, adhabu hii mimi nahisi kwamba iongezwe ya kifungo, kwa sababu haihitaji gharama. Mtu anaweza kushindwa kutoa shilingi milioni moja faini kwa sababu pesa nyingi lakini uwezo wa serikali kumfunga mtu miaka mitano au sita huu rahisi mtu anaweza kutumikia. Kwa hivyo hapa masuala ya adhabu kutokana na uzito wa jambo hili mimi nahisi kwamba iongezwe.

Baada ya hayo Mhe.Spika, naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe.Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe.Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) ambaye ametujaalia jioni hii tukaweza kukutana hapa tukiwa katika hali ya uzima na salama.

Lakini pia Mhe.Spika, nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kuweza kunipatia fursa hii nikaweza kutoa mchango wangu mdogo katika mswada huu ambao ni muhimu sana kwetu.

Mhe.Spika, pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe.Waziri na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu kututuliza kilio chetu Wazanzibari. Mhe.Spika, kwanza na mimi nataka nianze kwa kwenda katika madhumuni na sababu ya mswada huu na naomba ninukuu.

> “Madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria ambayo itaanzisha chombo cha kudumu kinachotambulika na imara kushughulikia masuala yanayohusiana na mitihani katika Zanzibar”.

Mhe.Spika, chombo hiki kama kitaamua kutusaidia kweli kweli basi naamini Wazanzibari tunaweza tukafikia mahala pazuri kwa wanafunzi wetu na serikali kwa ujumla. Kwa sababu Mhe.Spika, tumeumia sana kwa matokeo ya watoto wetu kuzuiliwa kufanya mitihani. Hili Mhe.Waziri ni tatizo kubwa kwetu, kwa sababu kama tujuavyo wananchi wetu ni wanyonge sana wameshajishughulisha kusomesha watoto wao mpaka wanakaribia kupata matumaini linakuja sakata kubwa la kuwavunja moyo wanafunzi, lakini si wanafunzi tu peke yao bali hata wazazi wao.

Mhe.Spika, kama wanavyoumia wanafunzi kwa kupata matokeo mabaya, vile vile ndivyo wanavyoumia wazazi kwa kuona juhudi zao zote walizozichukua miaka yote zimegonga ukuta. Kufungiwa wanafunzi mitihani kwa muda wa miaka mitatu ili wasifanye mitihani, tatizo hili Mhe. Waziri nikuombe ulishughulikie kwa kina sana.

Tuangalie mfano mdogo tu, timu ya mpira kwa mfano. Timu ya Yanga ifungiwe mchezaji wake kucheza kiasi cha mwezi tu utaona watu wanavyoshughulika kukata rufaa ya kuona mchezaji huyu atadumaa kimchezo. Mhe.Spika, mwanafunzi kumfungia kwa muda wa miaka mitatu bila ya kushiriki katika mitihani, ni kumdumaza na kumkatisha tamaa kabisa.

Mhe.Spika, niende katika kifungu cha 22(b) cha mswada huu naomba ninukuu kinasema hivi:

> "Kwa kujuwa au kwa uzembe atatoa nje mambo yaliyomo kwenye vifaa vya mitihani, au taarifa yoyote inayohusiana na mambo yaliyomo katika karatasi yoyote ya mitihani kwa mtu aliyehusika awe ni mtahiniwa au si mtahiniwa".

Mhe.Spika, hili ndilo jambo ambalo lazima bodi iangalie sana kifungu hiki, kwani juhudi za wanafunzi hapa ndipo zinapopotea kwa makusudi kuvujishwa mitihani, na wanafunzi hupoteza kila kitu, juhudi zote za kwenda *tuition*, kufanya *discussion* na vitu mbali mbali walivyoweka kwenye vichwa vyao wanaviacha na kutegemea mitihani iliyovujishwa, hatimae mwanafunzi anakosa kila kitu, anakosa kaa na gando.

Mhe.Spika, kitendo hiki cha kuvujishwa mitihani si kama kinaathiri wanafunzi tu, lakini kinadhoofisha elimu yenyewe kushuka hadhi yake, na hatimae elimu inaposhuka hadhi tutakosa wataalamu wa fani mbali mbali, kwa sababu mitihani waliyoifanya hawakufanya kwa akili zao. Hivyo watashindwa kumudu wanapopewa kazi za kufanya, watakuwa si wabunifu kwa vile mitihani wamefanya kwa kukopia watakuwa hawana uwezo. Hili Mhe. Spika, litakuwa ni tatizo kwa wanafunzi lakini hatimae litakuwa kwa taifa zima.

Sheria hii imepanga adhabu kwa mwenye kupatikana na hatia, na mimi namuomba Mhe. Waziri adhabu hizi zitumike kama zilivyopangwa bila ya kumuonea aibu mtu yeyote. Mhe.Spika, naomba ruhusa yako ninukuu ubeti mmoja wa mshairi unaosema:

"Kifungo kitu kibaya wala hakina kifani,
Hakuna anoridhia kwa hiari asiliani,
Hili ametuumbia rahimu mola manani".

Mhe.Spika, mwisho wa kunukuu.
Kwa maana hiyo adhabu hizi zikichukuliwa hakuna mtu hata mmoja kati yetu anayeweza kusema mimi nipelekwe jela angalau siku mbili, kwa sababu jela si pahala pa masihara. Kwa hivyo, adhabu hizi zikichukuliwa kweli bila ya kufanya mchezo nadhani tatizo hili linaweza kuondoka.

Mhe.Spika, mimi sina mchango mkubwa nilitaka tu na mimi niunge mkono hoja hii kwa sababu ni muhimu sana mswada huu, ambao nimesema utatuliza kilio chetu. Pia nilikuwa nataka niungane na Mhe.Salmin Awadh Salmin kuhusu lile jina la huu mswada. Naungana naye kwamba mswada huu uwe na jina la Baraza la Mitihani Zanzibar.
Mhe.Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe.Spika.

Mhe.Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutujaalia uhai na uzima na kuhudhuria katika kikao chako. Mhe.Spika, baada ya hapo nakushukuru kunipa nafasi hii kuchangia machache kuhusiana na mswada huu, kabla sijafika mwisho, huu mswada ulinipa faraja kubwa kwamba sasa tumefikia pahala pazuri Zanzibar pa kuanza kuweka tathmini na vipimo vya elimu yetu na upimaji.

Kwa hivyo, fikira zangu nyingi sana kabla sijaufikia mwisho mswada huu ilikuwa sasa nianze kwenda kwenye skuli zetu na kuzitizama majengo yake, namna wanafunzi wanavyokaa, maabara zake, je vitabu vinapatikana, wanafunzi wanapata *tuition* ya kutosha, walimu wapo, yote ni tathmini ya elimu, lakini kumbe lililokusudiwa liko mwisho kabisa. Kwa hivyo, mwanzo niliona mswada huu utakuwa mkubwa sana, kwa sababu itabidi mambo yote hayo tuyaangalie, tutakuwa na watu wangapi wa kuweza kwenda kuangalia yale mabanda yanayoning'inia mapaa, ni lini Mhe.Waziri atakwenda kuyaezeka.

Kwa bahati nzuri leo nilikuwa sipo asubuhi lakini kwa hamu ya Baraza yale maelezo ya Mhe. Salmin Awadh mimi niliyapata. Nashukuru sana na nilimpongeza nilipoingia tu namna alivyoweza kupitia pitia katika mswada huu. Kwa hivyo, niunge mkono basi kwamba isingepaswa chombo hiki kuitwa Bodi ya Tathmini au ya Vipimo au ya Upimaji, hapa isitumike lugha ya kutafuna wanayosema watu siku hizi, twende moja kwa moja tulikokusudia.

Mhe.Spika, ikiwa katiba na sheria zinaturuhusu tuseme hasa si lazima kutumia neno Baraza au nini lile liliopo, lakini tukitaje ni chombo cha mitihani *finish*. Kwa hivyo, kama wale waliopendekeza inaruhusiwa kikatiba na kisheria kusema Baraza la Mitihani Zanzibar basi tuliite hivyo kila mmoja alijue, hapo Mwanasheria Mkuu kabla ya majumuisho atakuja kutufafanulia.

Lakini mimi kidogo Mhe. Spika, nina wasi wasi zaidi wa hili neno Bodi kulitumia hapa, kwa sababu katika sheria nyingi tunazopitisha hapa Bodi, inatumika zaidi ni chombo cha kusimamia taasisi na sio taasisi kuna Bodi ya Shirika la Bandari, Bodi ya Shirika la *ZSTC*, kuna Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu, sasa hii bodi katika sheria zetu tunazopitisha hapa ina maana ni chombo kinachosimamia taasisi na sio taasisi yenyewe, lakini kwa mantiki ya hapa, bodi hiyo hiyo inatumika kwamba ndio taasisi. Sasa ikiwa hii taasisi inataka kusimamiwa, hicho chombo kitakachosimamiwa kitaitwa vipi, Bodi ya Bodi?

Kwa hivyo, hili neno bodi Mhe.Spika, hata kwa lugha zetu za kawaida tunazotumia hapa Barazani lisingestahiki kuwepo hapa. Hilo ndilo la mwanzo nililosema mimi. Kwa hivyo, ninaunga mkono ile *idea* ya kusema kwamba hiki chombo kingeitwa Baraza la Mitihani la Zanzibar moja kwa moja bila ya kutafuta maneno.

Halafu Mhe. Spika, moja katika nilimopitia kama nilivyosema mimi nilimsikia Mhe. Salmin Awadh na nikamsikia anam-*quote* Mhe. Ismail Jussa Ladhu naamini wamepitia sana. Lakini mimi nimeona jambo hili, katika mambo yote ya kazi na wajibu wa hii bodi kitu kimoja sikukiona, ambacho mimi binafsi nilikuwa nakipigia kelele sana Mhe.Spika.

Mimi nimekuwa nikisomesha kwa muda wa miaka 20, lakini sikupatapo kuyaona matokeo ya *Form II* hata siku moja, vile wanafunzi wanapofanya mitihani matokeo yakaletwa skuli kwamba hawa wanaendelea kwenda *Form III* hatujapatapo kuyaona sisi walimu. Mara nyingi nilikuwa nikisema hapa kwamba, haya matokeo vyovyote yatakavyokuwa wapelekewe walimu kwa sababu ndio watakaowarekebisha wale wanafunzi, lakini wanatangazwa wanafunzi majina tu hawa ndio waliopasi, Haile-Selassie, Haile- Selassie mpaka wanamaliza ,lakini walimu hawapelekewi matokeo halisi ya wale wanafunzi na wao ndio wanaambiwa wamepasi.

Sasa chombo hiki hakikuandikwa pahali kwamba kitachapisha rasmi matokeo ya wanafunzi, na hiyo lazima itokeze kwamba hatuwezi kuona chombo matokeo yako siri, lazima kichapishe rasmi matokeo ya wanafunzi yajulikane. Hilo ndilo jambo moja nililoliona kwamba lina kasoro katika mswada huu.

Mhe.Spika, hii ni nini? Ni kwa sababu wale wanafunzi ni *continous* akitoka *Form II* anakwenda *Form III*, akitoka *Form IV* anakwenda *Form V* na *Form VI* au anaendelea na Diploma na mambo mengine. Kwa hivyo, wale walimu na watu wengine wanataka kuona, lile neno kapasi tu Haile- Selassie mkururo mzima toka matokeo yanasomwa siku moja mpaka sasa yanasomwa siku tatu aa basi tena, kompyuta zote hizi zilizoenea.

Halafu Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 Muundo wa Bodi. Hiki kifungu cha 4(1) (a) katika mswada huu kinapingana na kifungu cha 4(3), kifungu cha 4(1) (a) kinasema hivi, "Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao: Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais, lakini chini yake hapo kifungu cha 4(3) Wajumbe wa Bodi watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti, *coalition* hapo. Kama kamati ilirekebisha nashukuru, kwa hivyo, hilo nafuta kama kamati ilirekebisha, lakini na mimi nilikiona kwamba kuna *coalition*.

Mhe.Spika, ile niliyosema kuchapisha rasmi basi itokeze katika kazi za kamati, pia itokeze katika uwezo wa bodi. Kwa sababu lazima ipewe uwezo wa kuchapisha, pengine ile kanuni iliyokuwepo ya kuandaa mitihani na kusahihisha ilikuwa haina uwezo wa kuchapisha. Kwa hivyo bodi inatakiwa ndani ya kazi zake ipewe ule uwezo wa kuchapisha haya matokeo.

Kifungu cha 8 Mhe.Spika, ikiwa tunaunda hiki chombo cha kitaalamu kama hiki, na ndio maana nikasema kwamba, kulitumia hili neno bodi linaweza kuwa-*confuse* wao wenyewe ndio kilichotokea katika kifungu nambari 8. Kama

kamati imeliona kidogo, mimi nilikuwa mbali na haya masahihisho ya kamati, Mjumbe wa Bodi isipokuwa wale ambao wapo kutokana na nafasi zao za kazi itakuwa ni kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi.

Sasa hii ni taasisi ya mitihani, ni taasisi inayoongeza ule ujuzi wake kila wakifanya lile jambo, sasa vipi tena unamuwekea miaka mitatu kama kulitizama. Ndio nasema hii kwa sababu unaita bodi sawa sawa na ile Bodi ya kusimamia taasisi, hii ndio hatari ya kutumia majina ambayo siyo.

Kwa hivyo, hapa kidogo pana wasiwasi, hawa wasingestahiki kuondoshwa mpaka kwa yale makosa ambayo yamo katika sheria hii, au mtu anajiuzulu mwenyewe, lakini kwa miaka mitatu keshajua kwamba mimi mwakani ninamaliza kwa nini asiibe mtihani na yeye anamaliza muda wake, atafanya purukushani tu.

Kwa hivyo, wajumbe watakaoingia katika taasisi hii wawe ni wa kudumu, kwa mujibu wa kazi zao na elimu zao. Suala la anaweza nafikiri sina haja ya kulizungumza, naunga mkono pale alipokuwa akisisitiza Mhe. Salmin kwamba kila ambapo taasisi hii imepewa uwezo, *ile anaweza*, *anaweza* iondoke na iwe *itakuwa na uwezo* huu mpaka pale itakapokuwa ni lazima tu kuwa anao uweza.

Halafu Mhe. Spika, hiki ni chombo cha mitihani kweli, lakini ukitizama mwanzo wake mimi nakubaliana kwamba Bodi ya Vipimo na Tathmini katika skuli Mhe.Spika, hususan za Sekondari kuna vitu vinaitwa *daily assessments* zinafanyika, yaani vipimo vya majaribio ya wanafunzi kwa *term* nzima kwa mwaka mzima, na yale yanakwenda katika Baraza la Mitihani la Tanzania hivi sasa. Kwa hivyo, katika uundaji wa kamati, kuna Kamati Tendaji na Kamati ya Mitihani, lazima iwepo Kamati ya Tathmini ndio itakayofuatilia kule skuli kunakwendwa vipi kila siku, kabla hajatahiniwa yule mtoto mwisho wa mwaka kule skuli kunakwendwa vipi.

Nilieleza siku moja Mhe.Spika, naomba niirudie tena, nilipokuwa mimi ni mkaguzi wa skuli tulikuwa na *work shop* moja Beit el Ras, alikuja *lecturer* mmoja tena huyu alikuwa ni mkubwa kwa sababu anatoka New York, Marekani lakini asili yake ni South Africa.

Mhe.Spika, yeye alituomba *experiment* moja tu, akatutaka tuchukue kipande cha *sponji* tukiingize ndani ya maji, tukakiingiza ndani ya maji. Halafu akasema hebu kitoe ukitizame, kikatolewa kikitizamwa uzito wake hakichukuliki, lakini akasema hebu likamuwe, lilipokamuliwa unamrushia mwenzako bila ya yeye kukereka, akasema hivi ndio wanafunzi wenu mnavyowafanya, mnawanywesha nyinyi kwa ajili ya mtihani hata akimaliza mtihani hajui chochote, siku ya mtihani anasema fatiha na yeye hana kitu.

Sasa ili kuzuia hayo, ndio ikawekwa ile kazi za kila siku iwe mwanafunzi hasomi kwa ajili ya ule mtihani tu, anasoma kwa ajili ya kujua na kutambua ile elimu. Sasa haiwezekani kuwa na kitengo cha Kamati ya Mitihani tu, lazima kuwe na Kamati ya Tathmini ili kuonekana kwamba kweli walimu wanafanya kazi zao kule, kweli wanafunzi wanapata ile taaluma. Kwa hivyo, iongezwe Kamati ya Tathmini hii ndio itakwenda maskulini kuona hasa kwamba kweli wanafunzi wanafanyiwa yale majaribio, na madaftari yao yako sahihi na kila kitu, hawa sio wakaguzi.

Mwisho kabisa Mhe.Spika, nasema kwamba huu mswada ni mzuri na unastahiki kuwepo, lakini iwe tumedhamiria kweli. Kudhamiria kweli kwanza ni kufuata mashauri ambayo yametolewa, kwamba chombo chetu tukiite moja kwa moja chombo cha mitihani, itakavyoitwa vyovyote Baraza, sebule vyovyote vile lakini iwe chombo cha mitihani.

Mhe. Spika, la pili usimamizi wa chombo hichi unahitaji kuwe na uangalifu mkubwa, usimamizi wa chombo hichi si hizi sheria za kubanana kwamba atafungwa miaka mitano, sita au kumi huu usimamizi. Usimamizi ni uwezo wa chombo chenyewe wa kuweza kuamua, kuweza kujipangia mipango yake hichi ndio muhimu. Kwa hivyo, tukisema tunaunda chombo kisiwe tena leo anawekwa huyu, kesho huyu, akiwekwa mtu anajulikana kwamba amewekwa na ana uwezo wa kuamua. Mhe. Spika, kwa haya machache mimi naunga mkono hoja kwa masharti kwamba haitakwenda hivi hivi kificho ficho, tutaliweka hili jambo bayana kwa mujibu wa sheria na katiba itakavyoturuhusu. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza jambo ambalo kwa mujibu wa mchango wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu asubuhi ni jambo muhimu sana. Mhe. Spika, labda kwanza kama kawaida yangu niipongeze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kutekeleza matakwa ya Sera yetu ya Elimu. Suala la kuunda chombo hichi limo katika Sera ya Elimu kama alivyolitaja Mhe. Waziri asubuhi hapa na ni

chombo muhimu na nafikiri kimekuja wakati muafaka sana hata kama kimechelewa kidogo. Lakini pia niipongeze Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kutusaidia kazi, wamejitahidi sana kufanya marekebisho ambayo tungelazimika kuchukua wakati mwingi kidogo kuyaeleza lakini tunawashukuru sana kufanya kazi hii.

Mhe. Spika, nafikiri kabla sijenda mbali nataka niungane na hii naomba sana Mhe. Waziri aichukulie kama angalizo maalum. Kila mjumbe aliyesimama hapa alitaka jina hili la bodi libadilishwe badala ya kuitwa bodi basi tuseme moja kwa moja kama hili ni Baraza la Mitihani la Zanzibar. Hoja hii aliizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu akaifafanua vizuri sana Mhe. Salmin Awadh Salmin na bila ya kutafuna maneno Mhe. Rashid Seif Suleiman nae kaizungumza na mimi natilia mkazo.

Mhe. Spika, natilia mkazo kwa sababu wakati umeshafika sasa Wazanzibari tubadilike na njia moja ya kubadilika basi sasa ni kusema kweli na yale maneno ya muhali ya kubabaisha mimi nafikiri tuyaweke kando. Jamii ya Wazanzibari inatutazama sisi tulioko humu, ni sisi ambao tukisimama imara tutaweza kuwatoa kule kwenye *angle* waliyowekwa. Maana Wazanzibari wako kwenye kona sasa hivi hawafurukuti, sasa kama sio sisi nadhani hakuna mwengine. Kwa hivyo, tujitahidi kila tunapoona hapa pana haja ya kurekebishwa basi tuseme wazi wazi kama hapa tufanyeni hivi. Hivi watakavyosema wawakilishi basi mimi nadhani serikali ina wajibu wa kufuata kwa sababu mimi hapa nawasemea watu zaidi ya 30,000 kutoka jimboni kwangu na kila mmoja ana idadi kama hiyo. Kwa hivyo, kauli zetu Mhe. Spika, ni kauli za Wazanzibari wote. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri hilo alizingatie.

Mhe. Spika, bodi hii au kama Mhe. Waziri atakapofuata mashauri yetu akalibadilisha likawa Baraza ni jambo muhimu sana na nilipokuwa naangalia kazi zake ndio hasa unaweza kuona sasa umuhimu wa hichi chombo.

Mhe. Spika, taasisi hii tunayoiunda ina kazi muhimu sana za kushughulikia masuala mazima ya elimu. Nilikuwa naangalia pale kifungu cha 5 Kazi za Bodi ukikisoma kifungu kidogo (b) naomba ninukuu kinasema “Ni kupima ni kwa kiwango gani skuli zimefanikiwa kufikia malengo ya elimu na kurekebisha miongozo sahihi ya utendaji kazi ambayo yatapelekea kuinua kiwango cha kujifunza.”
Sasa hii ni kazi muhimu sana kwa sababu nafikiri wengi wetu tumekuwa tukisema wazi kwamba kiwango cha elimu kimeshuka sana Zanzibar. Tumefanikiwa Zanzibar sana kumfanya kila mtoto wa Kizanzibari kupata a, b, c ya elimu lakini hatujafanikiwa kuweka ubora wa elimu ambayo itawasaidia Wazanzibari kuweza kuingia katika soko la ajira.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba mtoto anasoma mpaka anafika kidato cha nne lakini hana uwezo wa kukabili mitihani ya kidato cha nne. Ndio sasa hivi imekuwa kama ni dili kwa vijana wetu ikifika siku ya mtihani kama mtoto hana simu atakuazima simu yako usiku usiku, baba niazime simu hata ukisikia hivyo ni wiki ya mitihani hiyo.

Usiku kucha mtoto halali anapiga simu anauliza haya lipi lililovuja na matokeo yake ndio hayo yaliyojitokeza mwaka huu ambayo kwa kweli si mazuri hata kuyataja. Kwa sababu mtoto ameshasota miaka 12 halafu unakuja kuifanya kazi yake yote haina maana tena ni jambo baya sana.

Kwa hivyo, ile Mhe. Spika, inakuja kwa sababu watoto hawajiamini kufanya mitihani na hawajiamini kwa kuwa kiwango cha elimu walichonacho ni kidogo kulingana na mitihani inayokuja. Sasa ndio nikasema ni muhimu sana hii taasisi iwepo ili iweze ku-*monitor* kwa karibu sana elimu inayotolewa inafikia viwango.

Mhe. Spika, mimi mara nyengine nilikuwa naona tuna tatizo la mitaala katika nchi yetu kuna haja kubwa sana bodi hii ikishaundwa ikaangalia sana kurekebisha mitaala ya elimu. Mhe. Spika, watoto wengi wanafeli sasa hivi kwa sababu hawajui Kiingereza. Mtoto wa kidato cha nne hawezi kujieleza hata kwa ile *half full scap* kama atapewa swali
La Kiingereza ajieleze. Kwa mfano, swali la Biology ni suala la kujieleza hamna jawabu ya mkato kama hesabu mle. Sasa pengine anajua nimeulizwa hichi na anajua jawabu yake ni hii lakini kujieleza kwa Kiingereza anashindwa na badala yake anafeli.

Sasa hii inatokana na kwamba mitaala haijakaa sawa somo la Kiingereza ni muhimu, sina hakika kwa wiki wanafunzi wanasoma vipindi vingapi vya Kiingereza lakini sidhani kama vitazidi vinne. Kuna masomo lazima yaongezwe vipindi kutokana na umuhimu wake moja ni hili la Kiingereza, somo la Hesabu, Sayansi haya ni masomo lazima wizara iangalie kuyapa vipindi vingi katika wiki kuliko masomo mengine. Kwanza mimi nahisi

wanafunzi wetu sasa hivi sijui kwa sababu gani lakini wanapewa mzigo mkubwa au naweza kuita utitiri wa masomo ambayo mengine hayawasaidii.

Mhe. Spika, siku zote tunadaiwa fyagio mtoto kama imeshafika siku yake ya kupeleka fyagio atakwambia baba nigaie shilingi mia mbili, haya za nini, nakwenda kutafuta fyagio nipeleke skuli kumbe hilo nalo ni somo. Sasa ya nini haya jamani, tuna mambo muhimu kweli kweli ya kushughulikia, elimu yetu inashuka kila leo lakini bado wanafunzi wanaelimishwa mambo ambayo mimi sihisi kama yana faida sana. Kwa hivyo, lazima mitaala iangaliwe upya.

Halafu pia tunatakiwa tuwe na mfumo mmoja wa elimu utakaotambulika sio kila leo tunabadilisha mifumo. Mimi toka nimalize kusoma mifumo ya elimu imeshabadilika zaidi ya mara tatu au nne. Nilipokuwa nasoma mimi kulikuwa na darasa la nane, kabla yangu mimi ilikuwa haiko mtoto akimaliza darasa la saba anakwenda kidato cha kwanza. Tulipoingia sisi kulikuwa kuna darasa la nane hatujakaa vizuri ikaondolewa kukawa na *form I zero.* Sasa hii nayo inawababaisha wale watoto, inababaisha hata hiyo mitaala yenyewe haijulikani inakwenda vipi leo iko hivi kesho iko hivi.

Masuala haya Mhe. Spika, *once* unapokosea mfumo wa elimu basi athari yake hutaiona leo lakini baada ya miaka mitano inayokuja ndio utaona athari ya ule mfumo wa elimu uliobadilisha. Kwa hivyo, nilikuwa nahisi mimi tuwe na mfumo hii taasisi itakayoundwa basi iangalie kwa kina na ifanye utafiti. Nimeona humu miongoni mwa kazi zao ni kufanya utafiti, kwa hiyo ifanye utafiti wa kina lakini tukiibuka na mfumo wa elimu basi tuufuate huo twende nao moja kwa moja.

Mhe. Spika, wenzetu wanabadilika sasa hivi kuna nchi nyingi sasa hivi watoto wanawasomesha masomo yote katika ile elimu ya lazima wakifika darasa la saba mtoto anaanza sekondari ya kati ile anaanza ku-*specialize* masomo. Kwa hivyo, ule utitiri wa masomo wote sasa unaachwa na mtoto anaelekezwa kwenye masomo ambayo hay ohayo ndio atakuja kuyafanyia mpaka *degree*. Lakini sisi mpaka kidato cha nne tunamchukua mtoto na masomo 12 halafu unakwenda kumwambia mtoto afanye mitihani masomo yote yale hawezi kupasi kichwa hicho kitazingatia mambo mangapi.

Sasa nilikuwa nahisi mimi haya tuwachukue watoto kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba wasome masomo yote lakini *once* mtoto akianza kidato cha kwanza tuanze kumuelekeza kwenye masomo maalum na yale mengine tumpunguzie. Nafikiri tutakapofanya hivyo tutampa mtoto muda zaidi wa kushughulikia yale masomo ambayo anatarajia mwenyewe ayashughulikie zaidi.

Mhe. Spika, nilisema hapo awali kwamba hii bodi tuiite Baraza la Mitihani. Najua masuala ya elimu ya juu ni masuala ya Muungano lakini angalau basi mtihani wa kidato cha nne tufanye wenyewe kwanza, kidato cha nne sio elimu ya juu lakini bado tunafanya mitihani ya kidato cha nne kutoka Tanzania Bara. Mhe. Spika, tunapata athari kubwa sana katika hili, vijana wetu wanadhalilishwa sana.

Mhe. Spika, amini usiamini wenzetu katika suala hili la mitihani wana ubaguzi wa hali ya juu sana, wanaangalia hii *paper* ninayosahihisha sasa hivi ni ya nani. Watoto wetu wanafelishwa kwa makusudi kwa sababu wenzetu wamechanganya mambo mawili, wamechanganya elimu na biashara lakini wakati huo huo wanachanganya na mambo mengine zaidi ya kibaguzi. Hivi ndivyo aliyosema Mhe. Rashid Seif Suleiman na mimi nataka nimuunge mkono sana kwamba sasa tufike pahala yale matokeo ya watoto wetu basi yachapishwe tuyaone, sisi hatuamini kama vile wanavyofeli watoto wetu ndivyo inavyotokea.

Mhe. Spika, mwalimu ndie anayeweza kumjua mtoto vizuri, siku nyengine mwalimu anakuja anakwambia huyu hafeli kafelishwa lakini utakwenda kulalamika wapi masikini ya Mungu mtoto wa mzee wa Kizanzibari hata nauli ya daladala hana utamwambia aende Baraza la Mitihani Tanzania Bara akafuate matokeo ya mwanawe na akenda hayaoni. Kwa hivyo, inabakia ni kudhalilishwa na kudhalilishwa.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nafikiri mimi sasa hivi kuwa mitihani angalau ya kidato cha nne tufanye wenyewe tu Wazanzibari, hii iwe ni mwanzo lakini tufike pahala hata mitihani ya elimu ya juu tujitegemee. Mhe. Spika, hii ni nchi bwana ina vyuo mpaka vyuo vikuu vipo hapa kwa nini tutegemee kufanyiwa mitihani na nchi nyengine. Mimi nilikuwa nadhani wakati umeshafika kwa kweli sasa wa kufanya wenyewe tu mambo haya.

Mhe. Spika, sikuingia kwenye vifungu lakini niliona huku kuna uteuzi wa mkurugenzi na kazi za mkurugenzi. Ukisoma kifungu cha 18 naomba kunukuuk "Kazi za Mkurugenzi kwa mujibu wa masharti ya sheria hii atawajibika kufanya kazi za kila siku za bodi."

Lakini huku nyuma kuna katibu ambaye ni mwanasheria huyu kifungu kidogo cha 4, lakini baada ya marekebisho ya kamati kitakuwa kifungu kidogo cha 5. Kunakuwa na mwanasheria ambaye yeye atakuwa ni katibu wa hii bodi. Sasa hazikuelezwa kazi za mwanasheria hapa, lakini ukishamuita katibu mara nyingi anakuwa ndio mtendaji wa kazi za kila siku za ile taasisi, lakini na kule kuna mkurugenzi anafanya kazi za kila siku za taasisi. Sasa Mhe. Waziri nafikiri aje atuweke sawa hizi kazi za huyu katibu zitakuwa vipi ikishakuwa mkurugenzi ndio anafanya kazi za kila siku za bodi basi huyu katibu yeye kazi yake itakuwa nini.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mswada huu sijui kwa asilimia ngapi, nitaunga mkono mia juu ya mia ikiwa jina la Bodi litabadilishwa kuwa Baraza. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nami sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kupata nafasi ya kutoa mawazo yetu mafupi katika mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, niungane na wale wenzangu waliobahatika kuchangia asubuhi mwanzo wa hili jina la huu mswada. Mhe. Spika, nakubali na mimi kwamba ni vyema mswada huu ukapata jina lenye maneno mafupi lakini yenye maana pana. Kama walivyosema wenzangu kwamba kuliita Baraza la Mitihani Zanzibar hili si kosa, maana tunachukua maneno mengi ni sawa sawa na mtu anayetoka hapa tulipo anakwenda Malindi lakini akapita Uwanja wa Ndege, Amani, Bububu ndio akenda Malindi lakini kumbe njia rahisi ya kumfikisha Malindi ipo.
Kwa hivyo, Mhe. Spika, hakuna haja ya kuweka maneno mengi yote tukisema Baraza la Mitihani Zanzibar basi ndani yake humo mna vipimo, mna tathmini na kila kitu. Ni vyema hichi chombo tunachokiunda kikawa kina heshima kubwa na ikawa inajulikana dunia nzima kwamba na Zanzibar kuna Baraza la Mitihani.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo nataka nianze tu katika sehemu hii ya pili kuanzishwa kwa bodi. Mhe. Spika, naomba kunukuu "Kutakuwa na bodi ambayo itajulikana kama Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu ya Juu." Mhe. Spika, (2) (d) Bodi ina uwezo wa kuingia mikataba au makubaliano ya kufanya mambo ambayo yataleta ufanisi katika utekelezaji wa masharti ya sheria hii ambayo inaweza kufanywa kihalali na kutekelezwa na bodi."

Mhe. Spika, hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu chombo chochote kama kitakuwa hakina nafasi ya kuweka mikataba kwa kweli utakuwa umekinyima ule uwezo wake. Kama tunavyofahamu kwamba hichi chombo kimewekwa kinashtaki na kinashtakiwa kwa hivyo ni vyema wakawa na uhuru wa kuweka mikataba mbali mbali, mikataba ya kutafuta misaada na mambo mengine mbali mbali ili kuifanya hii bodi iweze kujitegemea kiuchumi na mambo mengine. Kwa hivyo, nakubaliana nacho hichi kifungu kuwepo katika hii bodi.

Lakini kifungu chengine Mhe. Spika, ni kifungu cha (f) katika kazi za bodi pale. Hichi kifungu kinasema "Kuweka na kuandaa miongozo kwa skuli na vyuo jinsi maendelezo ya kupima utendaji wa maendeleo wanayoyapata."

Mhe. Spika, kuweka na kuandaa mara nyingi katika skuli zetu hasa kuanzia lile madarasa yatakayojiandaa na mitihani darasa la sita kwenda la saba baadhi ya skuli tuna hawa ndugu zetu wa *tuition* kunatokea mivutano baina ya walimu wa skuli na hawa walimu wa *tuition*. Mwanafunzi anamthamini zaidi mwalimu wake wa *tuition* kuliko huyu mwalimu wa kawaida. Hii miongozo mara nyingi hawa ndugu zetu wa *tuition* hawaijali sana wanakuwa na yao miongozo na utakuta kadri inapofanywa mitihani baadhi ya skuli hawapati kutoa wanafunzi kuendelea mbele. Hili limedhihiri katika maskuli mbali mbali na tumewahi kusuluhisha baina ya walimu hawa wa *tuition* na walimu wetu wa kawaida.

Kwa hivyo, hii kazi ya bodi ni muhimu sana tusije tukaiacha katika sheria tu tumeshaiandika katika sheria na tumeshaipitisha lakini bodi wakashindwa kuisimamia kazi hii. Hii ipo skuli mbali mbali mavutano baina ya walimu wanaofundisha *tuition* na walimu wetu hawa wa kawaida. Kwa hivyo, ni vyema suala hili la kuandaa miongozo na kuandaa hii mitaala na hawa watu wetu wa *tuition* wakiwa na hii mitaala pia wanayo ili kuweza kutoa wanafunzi bora katika maskuli yetu.

Mhe. Spika, jengine nichangie katika kifungu cha 21 (1) kinachozungumza hesabu za bodi na ukaguzi naomba kunukuu "Bodi itasimamia utekelezaji wa hesabu sahihi za fedha na kumbukumbu zilizo sahihi kuhusiana nazo na hesabu sahihi za fedha na kumbukumbu hizo zitawekwa kwa mujibu wa miongozo inayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, kifungu hichi kimenipa mashaka kiasi fulani nimeona kwamba bodi ina watu wasiopungua 11 na kuendelea sasa nimejiuliza hesabu hizi mhusika mkuu atakuwa ni nani. Kwa hivyo, nimeunga mkono suala la Mhe. Salmin Awadh Salmin aliposema kwamba huyu Katibu wa Bodi hakupewa majukumu yake, nikaona kwamba na hili linaweza kuwa ni moja katika majukumu ya Katibu wa Bodi. Huwezi watu 11 na kuendelea wote ukawatia hatiani wakati mmoja itabidi kwamba bodi nzima atakapokuja Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kama bodi imefanya kosa basi watu wale 11 wote wafukuzwe kazi haiwezekani kwa hayo yote kutakuwa kuna mtu anayehusika.

Kwa hivyo, yule ambaye anahusika hichi kifungu alikuwa apewe mhusika isipewe bodi nzima. Mhe. Spika, nimeona kwamba hii ni sehemu moja ya Katibu wa Bodi kuweza kuwa na dhamana hii katika mahesabu haya ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, pia nilikuwa naomba kupata ufafanuzi kuhusu hii elimu ya juu. Hapa petu Zanzibar haijulikani mwanzo wake ni wapi na imeishia wapi. Kama elimu ya juu mwanzo ni kidato cha nne tuelezwe, au mwanzo ni kidato cha sita tuelezwe na mwisho tuambiwe ni wapi. Isiwe kwamba tunaambiwa suala hili ni suala la Muungano elimu ya juu lakini hatujui mwanzo ni wapi na mwisho wake ni wapi. Kwa hivyo, tungelimuomba Mhe. Waziri atuelimishe kuhusu hii elimu ya juu hapa Zanzibar imeanzia wapi na imeishia wapi.

Mhe. Spika, nikirudi nyuma kidogo katika hizi hizi kazi za bodi kifungu © kinasema kwamba "Kuweka utaratibu maalum wa mitihani, majaribio, upimaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyafanya kwa mujibu wa mtaala wa Zanzibar."

Mhe. Spika, katika Zanzibar hasa vijana wetu waliopo maskuli Mwenyezi Mungu amewajaalia wana vipaji mbali mbali, na unaweza ukakuta kama darasa la saba karibu yako kumi au kumi na mbili wote hao ni darasa la saba na tatizo tunaloliona ni kwamba tunawatoa vijana wetu katika vipaji kuwaweka, tujaalie wale waliofanya mitihani wakapasi kuanzia wa kwanza mpaka wa kumi, hawa tunawachanganyisha na kundi lile ambalo akili zao kidogo hazijawa vizuri, sasa ningeomba sana hii bodi ishughulikie wale vijana wenye vipaji. Tujaalie shule zenye madarasa 11 au 12, basi wale vijana wenye vipaji wakaanza kuwateua wakawa wana darasa lao maalum, ili kuwaboresha zaidi, kuwa na vipaji zaidi na fahamu zao zizidi kutanuka zaidi ili vijana wale watakua na uwezo wa kufika mpaka vyuo vikuu.

Hapa itakua kidogo vijana wetu tumewanyanyua kitaaluma na wale ambao wanajiona kwamba akili zao hazijawa vizuri kidogo basi watakua na uwezo wa kupambana na darasa hili ili kuhakikisha na wao wametoka katika lile eneo walilokua. Kwa hivyo, ningeomba sana bodi kazi hii waishughulikie ili kunyanyua vipaji vya vijana wetu.

Mhe. Spika, nimesema toka mwanzo kwamba mchango wangu utakua mdogo. Kwa hivyo, niseme kwamba naunga mkono mswada huu na yale maeneo ambayo tulisema yanahitaji kufanyiwa ufafanuzi, basi yakishafanyiwa ufafanuzi na sisi tutaweza kuyaunga mkono, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu unaohusu elimu. Kwanza naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuunda chombo cha kipimo na kutathmini shughuli zote za elimu. Kifungu cha 54 sheria ya kutunga chombo ya vipimo na tathmini ya elimu. Kwanza elimu ni ufunguo wa maisha, hilo ni suala tosha la kuweza kumpongeza Waziri kuweza kufungua chombo hiki na kuweza kupata nafasi Wizara hii kuweza kuchangiwa na wajumbe wote tuliomo humu Barazani, ili kuweza kua na nafasi nzuri ya kuweza kuunda jopo na vizuri kukaa na kuzingatia matatizo ya wanafunzi.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 cha sheria ya bodi ya kutunga mitihani kinasema, ni lazima wale walimu ambao wanatunga mitihani ni lazima wale kiapo ili kuweza kuhakikisha mitihani haiwezi kupenya, sio baada ya kumaliza mitihani ndio yanatokea matatizo ya kutilia mashaka mitihani. Kwa hivyo, ni vizuri kuhakikisha watungaji wa mitihani wanafanya vizuri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri alitilie uzito somo la sayansi ili wanafunzi waweze kufaulu vizuri.

Mhe. Spika, naomba kunukuu kifungu cha 13(1),

> "bodi itachagua watu watakua maafisa wenye mamlaka kwa mujibu wa kutathmini sheria hii".

Kifungu cha 13(2),

> **"**Maafisa waliochaguliwa chini ya kifungu cha kiwango, kifungu hiki kitafanya yafuatayo, atalazimika kuchagua majengo kabla ya kubadilisha majengo hayo kua vituo vya mitihani"

Anaweza kuingia muda wowote kuchagua majengo ya kufanyia mitihani. Ni muhimu walimu wanaotunga mitihani na wasimamizi ni lazima wapewe kozi maalum na sheria itachukua mkondo wake pindi ikigundulika kuvuja kwa mitihani ya taifa. Mhe. Spika, humu iwe ni kwa walimu na sio kwa wanafunzi kama inavyofanywa hivi sasa. Kwa sababu imekua kama kesi ya ng'ombe, anapigwa ng'ombe yule wa nyuma kumbe mwenye matatizo ni yule ng'ombe wa mbele.

Kwa hivyo, sio kuhukumiwa wanafunzi, wahukumiwe walimu ambao wamesababisha kuvuja kwa mitihani na kulikopelekea taifa katika hatua mbaya na kukosa kuwa na wanafunzi wazuri au kua na wanafunzi wa mashindano ya kitaifa. Kama tunavyojua hivi sasa nchi za dunia nzima zina mashindano. Hivi sasa tuna mashindano ambayo tunashindana na Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda na Tanzania. Kwa hivyo, tunahitaji tuwe na wanafunzi bora ambao wanaweza kuingia katika ushindani wa kimataifa. Kwa hivyo, iko haja walimu wote ambao wanasomesha au kusimamia mitihani basi wahakikishwe kua ni walimu bora na ndio wanaoweza kusimamia mitihani ya taifa.

Mhe. Spika, kutokana na ushauri wangu huo mdogo basi tujitahidi katika kipindi chengine isitokezee aibu tena kwa Tanzania kuweza kuvuja kwa mitihani kwa walimu na kuweza kuwasababishia wanafunzi kukosa haki zao za msingi kama ilivyotokea katika kipindi hiki kilichopita.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, na mimi naomba nitoe mchango mfupi sana katika mswada huu, kwa sababu mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambao mswada huu tuliupitia takriban kwa siku mbili.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu. Vile vile nimpongeze baada ya kupata uteuzi mwengine wa kwenda kwenye Wizara nyengine muhimu.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, nakumbuka maneno ambayo bibi yangu aliwahi kuniambia. Mhe. Spika, bibi yangu aliwahi kuniambia kwamba siku zote utambue kwamba pang'okapo jino basi hapaachi kukaa pengo. Vile vile akaniambia kwamba siku zote jino la pembe kamwe si dawa ya pengo. Kwa bahati mbaya sikuwahi kumuuliza tafsiri yake, alifariki mapema, lakini niliamini kwamba jino la pembe haitakua dawa ya pengo.

Mhe. Spika, nije kwenye mswada huu na niseme kwamba tangu wakati wa majadiliano kwenye kamati, baadhi ya wajumbe waliibua hoja hii ya kuwepo kwa Baraza la Mitihani badala ya bodi. Lakini Mhe. Ramadhan ni mtu wa busara ndio akajenga hoja kwamba kuna haja ya jambo hilo lakini tuliweke baadae, na kwa siku hiyo hoja hii alishinda kwenye kamati. Kwa sababu mswada huu ni mali ya Baraza sasa na mimi nimeshawishika kabisa baada ya kujenga hoja wajumbe wenzangu, basi nilishawishika kweli kwamba kumbe kuna haja ile hoja ya kwenye kamati tukubaliane kwamba sasa tuwe na Baraza la Mitihani Zanzibar, badala ya kuwa na Bodi ya Mitihani na Upimaji.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu ambazo nimezionesha. Kwanza nimeshawishika kuona Baraza la Mitihani, kwa sababu katiba yenyewe ya Zanzibar haitukatazi kuwa na Baraza la Mitihani Zanzibar kwa ile elimu ambayo sio elimu ya Muungano, kwa maana ya darasa la kwanza au elimu ya maandalizi mpaka darasa la kumi na mbili. Katiba yetu ya Zanzibar haijasema kwamba imetuzuwia kuwa na Baraza la Mitihani. Kwa hivyo, mimi binafsi naungana na Mhe. Salmin na wengine wote kwamba kuna haja kweli ya kuwa na Baraza la Mitihani Zanzibar badala ya kuwa na Bodi ya Vipimo na Tathmini.

Mhe. Spika, sababu ya pili ambayo imenishawishi kuunga mkono hoja hiyo ni kwamba elimu ya sekondari sio jambo la Muungano, kwa maana ya kwamba elimu ya maandalizi hadi darasa la 12 sio sehemu ya Muungano

kwenye elimu. Vile vile sera yetu ya elimu Mhe. Spika, tumeambiwa sera yetu kwamba elimu ya lazima ni kuanzia elimu ya maandalizi hadi darasa la 12. Kubwa zaidi ambalo limenishawishi kuamua kuwa na Baraza la Mitihani Zanzibar ni kua tutaokoa fedha nyingi za walipa kodi kulipia mitihani ya darasa la 12 kule NECTA. Mhe. Spika, hivi sasa sisi Zanzibar tunalipia kila mwaka si chini ya milioni 600 kwa ajili ya mitihani ya darasa la 12. Kwa hivyo, tukiwa na Baraza letu la Mitihani basi fedha zile zitaingia ndani ya chombo chetu na Wazanzibari wenyewe watasimamia na mitihani yetu itakua tumetunga wenyewe chini ya fedha zetu za ndani.

Mhe. Spika, najua Mhe. Waziri anaweza akajenga hoja kwamba hatuna uwezo au hatuna fedha, vitendea kazi na wataalamu. Mimi nasema hoja hiyo itakua ni dhaifu kwa sababu fedha tunazo, wataalumu watafunzwa na wapo na vitendea kazi pakiwa na fedha vitapatikana. Kwa hivyo, hoja ya kwamba hatuna fedha na wataalamu ni dhaifu na nimuombe sana Mhe. Waziri kwa busara zake na ndio maana tukampeleka sehemu nyengine, basi hoja hii asiijenge. Uwezo tunao, fedha zipo, labda atuambie ni nia ndogo ambayo tunayo pengine na woga, jambo ambalo tukiwa na woga ni udhaifu wa uongozi.

Mhe. Spika, kwa msingi huo basi nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba tukubaliane basi na hoja za wengi kwamba Zanzibar sasa imefika tuwe na Baraza la Mitihani la Zanzibar ambalo litasimamia mitihani yote mpaka darasa la 12, tuwache ile mitihani ambayo ni ya elimu ya juu ambayo ni jambo la Muungano.

Mhe. Spika, tukifanya hivyo basi kilio cha Wazanzibar kitapungua kwa kiasi kikubwa, kwani ni hivi karibuni tumepata matokeo ya mitihani ambayo zaidi ya wanafunzi 3,000 wamefutiwa matokeo kwa Tanzania. Zanzibar tumeambia ni wanafunzi 1,300, baada ya utafiti wa kina kumbe Zanzibar ni wanafunzi 2,097. Ina maana kwamba wanafunzi 1,054 ni *school candidates* na wanafunzi 1,043 ni *private candidates*. Kwa hivyo, jumla ni wanafunzi 2,097 wamefutiwa mitihani yao hapa Zanzibar. Kwa hivyo, kwenye wanafunzi 3,000 na Wazanzibari kufutiwa wanafunzi 2,097 ni mtihani mkubwa na kwa kweli ni pigo ambalo kwa muda mrefu litatugharimu na linahitaji majibu sahihi ya kuweza kuwaokoa Wazanzibari wetu.

Mhe. Spika, kama tungekua na Baraza letu la Mitihani, basi hata matokeo haya yangetokezea basi Wazanzibari ingekua rahisi kukimbilia kupata majibu juu ya zile hoja zao ambazo wanazo. Mhe. Spika, niseme tu kuwa baada ya matokeo hayo ya mitihani kufutiwa, basi Baraza la Mitihani la Taifa NECTA walitoa adhabu ya kuwazuilia wanafunzi wetu kwa miaka mitatu mfululizo wasifanye mitihani, ni kwa mujibu wa sheria yao.

Mhe. Spika, tumefanya utafiti na kushangaa kwamba wakati wanafunzi wamezuiliwa, tayari matokeo yanatoka kwa baadhi ya skuli pakiwa hapana rufaa, sasa umezuia nini. Kwa nini umezuia kwa miaka 3, lakini unaendelea kutoa matokeo ambayo kuna mwanafunzi ulimzuilia halafu leo unampa matokeo.

Mhe. Spika, jengine ambalo linasikitisha ni kwamba tumepata habari kua kuna wanafunzi ambao walifanya mitihani ya masomo ya *Art*, lakini wakaja kupata matokeo ya *Science* na kuna wale ambao walifanya mitihani ya *Science* wakaletewa matokeo ya *Art*. Kwa hivyo, yote haya tungekua na Baraza letu, basi udhaifu huu ungekua rahisi kuutathmini na kutafuta dawa yake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nasema kwamba kuna haja kuanzia leo ya kuanzisha Baraza letu la Mitihani, wala sio ajabu, wala hatuvunji katiba na wala hatufanyi miujiza ni jambo tu la kuamua kuanzia leo ili Wazanzibari wajenge imani na Wizara hii, wajenge imani na Wazanzibari wenziwao na wajenge imani na nchi yao kwamba tumeamua kuwatumikia kwenye suala zima la elimu, tuwache yale yote ambayo ni ya Muungano hatuwezi kuyaingilia, lakini yale ambayo sio ya Muungano na yako chini ya utaratibu wa sera ya elimu Zanzibar basi tuanze kuyatekeleza.

Mhe. Spika, kwa mchango wangu huu mdogo, iwapo Mhe. Waziri atanikubalia kuungana na wengi kuwa na Baraza la Mitihani, basi nitaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikupe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nikaweza kuzungumza machache sana. Mhe. Spika, wenzangu wengi sana wameshachangia kuhusu mswada huu na mimi nitaomba niende ndani kidogo tu ili kuongezea kwa yale maeneo ambayo yaliyobakia.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo aliyoifanya na nathubutu kusema kwamba leo wananchi wetu wote wa Zanzibar wanatuangalia waheshimiwa wao tutafanya nini au Wawakilishi wao tutafanya nini, hasa katika suala zima la mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kwa nini nampongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Nampongeza kwa kutekeleza kwa vitendo sera ya elimu ya Zanzibar. Mhe. Spika, mswada huu ndio unatekeleza hasa ile sera yetu ya elimu Zanzibar.

Mhe. Spika, tumepitisha hapa sera ya elimu ya Zanzibar kwamba ile elimu ya lazima basi tulisema mwanafunzi sasa hivi aanzie skuli ya chekechea na amalizie darasa la kumi na mbili. Mhe. Spika, kama hii ni sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi tunatakiwa yote tuyashughulikie sisi wenyewe.

Mhe. Spika, leo mitihani ya darasa la kumi na mbili kuacha kua na maamuzi yetu ndani ya Zanzibar, tukachanganya na wenzetu ambao hata sera pengine ziko tofauti. Mhe. Spika, tutakua hatujitendei haki, lakini vile vile hatuwatendei haki wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nchi yoyote duniani ina malengo yake na katika hayo malengo yake inaanzia na sera na nchi yoyote inakua na mahitaji yake vile vile. Kwa hivyo, kwa kua ni sera yetu ya elimu Zanzibar, elimu ya lazima anatakiwa mwanafunzi afike darasa la kumi na mbili. Kwa hivyo, sasa wakati umefika kuangalia mahitaji gani Zanzibar tunayahitaji, ili kila mwanafunzi anayemaliza mtihani wa darasa la kumi na mbili, basi ahakikishe kwamba angalau amepata moja, mbili au tatu.

Mhe. Spika, kwa kupitia mswada huu ingawa Mhe. Waziri alipouleta mswada huu hakujiandaa na hilo. Lakini nathubutu kusema kwamba mswada huu moja kwa moja sisi kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao nilipoangalia katika jina la mswada, basi miswada yetu yote tunaambiwa imetungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mswada huu ambao umeletwa, niende katika kifungu cha 3. Lakini kabla sijenda katika kifungu cha 3, kwanza nije kwenye jina la mswada. Mhe. Spika, mimi nakubaliana na wenzangu, kuanzia na Mhe. Salmin Awadh na wengine waliofuatia kwamba sasa hivi baada ya kuitwa Sheria ya Kuanzishwa kwa Bodi ya Vipimo na maneno mengine mengi, sasa hebu tuyafupishe haya maneno ili Kiswahili kieleweke.

Mhe. Spika, tafsiri hii ukimpelekea mwananchi huko kijijini, itabidi kwanza afumbe mbacho akusikilize unakusudia nini. Lakini ukimwambia kwamba tumeanzisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Mitihani la Zanzibar, nadhani haya mengine yote yanayokuja humo ndio madhumuni yake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hiki ndicho kilichokua kilio cha wananchi wa Zanzibar. Katika kipindi kifupi kilichopita ilitokezea taharuki kubwa sana Zanzibar, watu wakalia na wengine wakalizana, simu kumi kumi na *message* mia mia, watoto wetu wamefutiwa mitihani. Lakini je, ni mitihani gani waliyofutiwa. Ni mitihani ya elimu ya lazima. Sasa hebu tujiulize Zanzibar iliwajibika vipi katika suala hili. Matokeo yake jambo letu wenyewe tumempa Mjomba atuamulie, matokeo yake yamekua ndio kama haya.

Mhe. Spika, nadhani ili kufuta machozi ya Wazanzibar, machozi ya wazee wa wanafunzi na machozi ya watoto wetu. Mimi nadhani anjifu ya kufutia machozi yale ni kurekebisha jina la mswada huu tukaanzisha Baraza la Mitihani la Zanzibar, hakuna suala jengine Mhe. Spika. Kuendelea kusema kwamba hatuna uwezo au hatujajiandaa. Suala la kusema kua hatuna uwezo au hatujajiandaa, ingawa hili hajalitamka Mhe. Waziri mbele yetu, alitamka kwenye kamati kwa maelezo ya Mhe. Hija Hassan Hija. Mimi nataka kusema kwamba tuwe wajasiri na Zanzibar tumeshawahi kufanya ujasiri mkubwa tena mkubwa sana.

Mhe. Spika, Zanzibar hapa tumeanzisha mpaka vyuo vikuu, watu wakawa wanajiuliza maswali mengi, vipi Zanzibar wanaanzisha vyuo vikuu walimu wako wapi na uwezo uko wapi. Mhe. Spika, Zanzibar ina wataalamu wazuri na ina mabingwa wazuri ambao wanaweza wakafanya mambo hapa Mhe. Spika, hata katika nchi za wenzetu hawayawezi. Mhe. Spika, tuna ma-*professor* wengi Zanzibar na tuna watu wengi wenye taaluma, wengine wamo ndani ya Wizara, wanaweza wakaazimwa kwa muda wakajakufanya hii kazi.

Mhe. Spika, nafikiri jana tulilizungumza hili suala, katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hebu tuone ile *database* ya wataalamu. Mimi nadhani Mhe. Waziri jana tulianza kumpa hiyo kazi, nafikiri ameshaianza hiyo kazi, wataalamu wake Wizarani wameshaanza hiyo kazi. Tukipekua pekua wataalamu hawa tunao wa kutunga hii mitihani ya darasa la 12 kwa Zanzibar.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu, mimi nafikiri tusizunguke sana, tukisema hatuna wataalamu, basi itakua tunawadogosha wataalamu wetu waliokuwepo hapa Zanzibar. Kwa kua tunatekeleza kwa vitendo hii sera ya elimu ya Zanzibar, basi suala hili wala tusiwe na kigugumizi katika suala zima la kufanya maamuzi mazito kama haya kwa maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba wenzangu wamesema lakini wacha na mimi nikazie kidogo. Kwanza tunapozungumzia suala la elimu katika mambo ya Muungano, tumekubaliana katika suala la elimu ya juu tu, elimu ya darasa la kumi na mbili bado haijakua ni elimu ya juu. Kwa hivyo, kama mtu atasema mnakiuka katiba, mnakiuka sheria, bado tumo ndani ya katiba ya Zanzibar tunaitekeleza tena tunaitekeleza kwa vitendo.

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba rasilimali ya mwanzo ya nchi yoyote duniani ni elimu. Sasa kwa kuwa rasilimali ya nchi yoyote duniani ni elimu basi mimi nadhani wakati umefika sasa hivi tuanze kuweka *base* ya elimu yetu kwa Zanzibar, tuangalie mahitaji yetu Zanzibar kutokana na mazingira yetu tuliyokuwanayo, ili tuwe na vijana wazuri, hata wale ambao wanamaliza darasa la kumi na mbili basi waweze kuanza katika ile mitaala ambayo itaandaliwa kwa mazingira ya Zanzibar, ili waweze na wao kujitegemea.

Mhe. Spika, sitaki niende sana katika kuchangia huu mswada kwa sababu wenzangu wengi wamekwenda katika vifungu. Mhe. Spika, kuna mjumbe mwenzangu mmoja alilizungumza hili, nadhani Mhe. Radhid Seif Suleiman. Suala la hii sheria tumeita bodi, lakini hii bodi ukiiangalia kama ni chombo moja kwa moja cha utendaji, ndio maana tukasema kwamba kwa nini tuzunguke sana, kwa sababu ukiangalia bodi ambayo maana yake ni chombo kinachosimamia taasisi fulani katika uendeshaji wa shughuli zake. Kwa hivyo, mimi nadhani tusiwe na kigugumizi katika kurekebisha hili jina na huu mswada kupewa jina jengine.

Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri ataona kuwa huu hapana, huu mswada ulivyoandaliwa, kama ilibidi liwe Baraza, basi lazima tulete mswada mwengine. Nadhani hatuna haja ya kufanya haraka, kwa sababu mambo mengine yatakua yanajirejea haya haya, isipokua kuna baadhi ya mambo tu yakarekebishwe na muda bado tunao, ili tuweze kufanya jambo ambalo litaweza kuleta maslahi kwa Zanzibar.

Jengine kabla sijamaliza Mhe. Spika, kuna hili jambo ambalo lilitokezea kwa wanafunzi wetu waliofutiwa mitihani na wakapewa adhabu ya kukaa miaka mitatu bila ya kufanya tena mitihani. Mhe. Spika, kwa mtu yeyote ambaye, sitaki kusema mwenye akili timamu, lakini nataka niseme kwamba kwa mtu yeyote mwenye busara, basi kwa kweli adhabu hii ni kubwa sana.

Vile vile hebu tujiulize, adhabu hii kwa asilimia kubwa iliyowapata ni vijana wetu wa Zanzibar, pamoja na kwamba wenzangu wamesema wanafunzi karibu 3,000 waliofutiwa, lakini ukiangalia kwa idadi ya Zanzibar, wanafunzi ambao waliofutiwa ni karibu 2,900 jumla, ukiwacha wale wa *private* pamoja na wale ambao wako mashuleni. Mhe. Spika, kwa idadi yetu ya Zanzibar hawa ni vijana wengi kweli kweli na hapa taifa tutakua tumepoteza rasilimali kubwa na tusitegemee Mhe. Spika.

Mhe. Spika, leo mwanafunzi anaendelea kusoma mfululizo na bado matokeo yake katika mitihani unamkuta kajitahidi basi anapata *division three*, lakini wengi wanaishia *division four*. Je, leo mwanafunzi kakaa miaka mitatu, halafu hali ya wazee wetu, hali ya wananchi wetu majimboni tunaowajua, sio wengi wenye uwezo wa kuwapeleka *tuition* vijana wao kwa muda wa miaka mitatu na wakaweza ku-*sustain* kusoma ndani ya miaka mitatu kwa kusubiri kuja kufanya mtihani wa taifa.Mhe. Spika, hii ni adhabu kali sana na wala haikustahiki kwa vijana hawa.

Mhe.Spika, nadhani kama ingekuwa kile chombo ambacho kinachotunga mitihani, hicho chini ya usimamizi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nafikiri serikali ingekuwa tayari imeshachukua hatua. Lakini wanafunzi walioathirika ni wetu wa Zanzibar na wala Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiwezi kuchukua hatua yoyote hasa kwa wale waliohusika na lile suala.

Kwa mfano, ukiangalia Mhe.Spika waliovujisha mitihani sio wanafunzi, isipokuwa mitihani ilivuja ndipo baadae wakaletewa wanafunzi, ndio yale aliyozungumza mwenzangu Mhe. Mussa Ali Hassan Mwakilishi wa Jimbo la Koani, alisema kwamba leo anachelewa ng'ombe wa mbele unamchapa bakora ng'ombe wa nyuma na hivyo ni kumuonea. Kwa kweli kama yule ng'ombe wa mbele angekuwa amejitahidi kwenda mbele zaidi basi huyu wa nyuma asingechelewa.

Mhe.Spika, kwa mara ya kwanza wananchi wa Zanzibar bila ya kujali kulipwa posho, muda wao, yaani wazee wa Zanzibar wameamua kuunda Kamati yao kwa ajili ya kushughulikia suala hili, tena walihangaika sana na wamekwenda mpaka wizarani na kuitaka serikali lazima itoe tamko, lakini serikali itatoa tamko gani Baraza la Mitihani sio la Zanzibar.

Kwa hivyo, ndio maana tukasema suala hili sio jepesi, leo wazee wetu wale sio kama ni watu mambumbumbu, yaani wazee wamesoma, walikaa na kuangalia hii athari na kuona kwamba hili taifa kwa tunakoelekea ni kubaya, yaani watoto wetu hatuwatendei haki.

Mhe.Spika, athari yake suala hili. Kwa mfano, tumchukue kijana ambaye amefanya mtihani wa kidato cha nne (IV), tujaalie amefanya mtihani ule akiwa na umri wa miaka 17 au 18 labda ni mtoto wa kike ndani ya miaka mitatu hana shughuli ya kufanya, atafanya nini, nadhani mwisho ataingia kwenye mambo ambayo hayamuhusu.

Kwa maana hiyo, anapelekwa katika utu-uzima na wala bado hajafika, kwa sababu tunamjua kijana wetu akishamaliza mtihani tunaambiwa tayari ameshafika utu-uzima na huyu anasubiri matokeo, yaani bado ni mwanafunzi.

Kutokana na hali hiyo, tutakuja kujikuta tunao watoto wengi ambao hawakutarajiwa, kwenye wanafunzi 3,000 tunajua *population* kawaida wanawake wanakuwa wengi. Mhe.Spika, miongoni mwa wanafunzi 2,900 kama kutakuwa na takwimu sahihi, basi watoto wa kike hawatopungua 1,500 mpaka 2,000.

Sasa hebu tuangalie kati ya watoto 1,500, mfano hawa 500 wote wakipata mimba za ujari, na huku wanasubiri kwenda kufanya mtihani wa kidato cha nne (IV) athari yake ni kubwa. Mhe.Spika, hivi tunayo *Program* ya MKUZA kwa ajili ya kuondoa umasikini, basi katika utaratibu kama huu itakuwa umasikini tumeuongeza kwa kiasi kikubwa sana.
Mhe.Spika, jambo hili limetugusa sote wazanzibari, yaani kuanzia wazee wa watoto ambao wenye wanafunzi mpaka na sisi jamaa na ndugu ambao tuliokaribiana nao.

Mhe.Spika, ndio maana tukasema kwamba nadhani hivi sasa iko haja, kwa sababu wananchi wetu walituma *messages* na sijui kama wewe hukuletewa Mhe. Spika kama namba yako wanaijua, yaani wanasema hasa kuwa jamani tunataka hivi, sasa pamoja na wanafunzi wenyewe wanasema kuwa wanataka Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Kwa kweli ndio maana tukasema kwamba Mhe.Waziri amefanyakazi kubwa pamoja na kuwa anaiaga Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini leo ameitendea haki, yaani ameitendea haki wakati anaondoka na tunatarajia kama angekuwepo basi angeitendea mambo makubwa zaidi. Lakini tunamtakia kila la kheri huko anakokwenda, na Mwenyezi Mungu amjaalie kazi njema, ampe maarifa mazuri, matatizo yaliyokuwepo aweze kuyarekebisha. *(Makofi)*

Vile vile tunamuomba asijekutuangusha wakati atakapokuja kufanya majumuisho. Mhe.Spika, tunataka Mhe.Waziri wetu tumuage kwa vigeregere pamoja na hoi hoi kwa kupitishwa mswada huu vifungu vyote bila ya kupingwa hasa baada ya kusikiliza wananchi wa Zanzibar.

Mhe.Spika, rafiki yangu hapa Mhe.Ali Mzee Ali na hivi sasa tumempachika cheo chengine cha Walii, kwa sababu mara nyingi huwa anatuambia. Rais Mstaafu wa Zanzibar Mzee Aboud Jumbe Mwinyi wakati alipounda Baraza la Wawakilishi alisema kwamba tunaunda Ngome ya Wananchi. *(Makofi)*

Sasa Mhe.Spika, ngome ya wananchi inasema mswada huu ubadilishe jina na liwe Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa hivyo, sitegemei Mhe.Waziri kama atachukua nyundo kwa ajili ya kuibomoa hii ngome ya wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe.Spika, baada ya hayo machache napenda kukushukuru sana, pia nataka nikuthibitishie Mhe. Spika katika mswada ambapo wananchi wote wa Zanzibar, nadhani hivi sasa wamejazana kwenye *television* utafikiri wanaangalia *Timu* ya *Barcelona*. Kwa hivyo, wanamsubiri Mhe.Waziri ataiaga vipi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, je atawafurahisha au atawaliza. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe.Spika, kwa kuwa Mhe.Waziri anacheka pale, basi naamini jawabu zake zitakuwa nzuri na mswada huu tutaupitisha bila ya kuupinga. Nakushukuru sana Mhe.Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe.Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata fursa hii jioni ya leo kwa ajili ya kutoa maelezo mafupi, juu ya mswada huu uliopo mbele yetu.

Nianze kwa kumpongeza Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anayeondoka kwa kuondoka wizara hii, ambayo yenye matatizo kiasi na kwenda kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ambayo ina matatizo kiasi zaidi.

Kwa hivyo, upande mmoja nimpongeze na mwengine nimpe pole kidogo kwa kazi ngumu zinazomkabili, yaani kutoka kwenye kazi ngumu na kuingia kwenye kazi ngumu nyengine.

Vile vile nimpe pongezi za dhati kwa kutuletea mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe.Spika, Zanzibar tumekuwa tukifanya mitihani katika vyombo tofauti. Kwa mfano, watu waliosoma nyuma sana, vyeti vyao vilikuwa vinatoka katika Chuo kimoja cha Uingereza ambacho kinaitwa *Cambridge* hadi mwaka 1969, ambapo wanafunzi wa mwaka huo walifanya mitihani miwili pacha, yaani walifanya mtihani wa *Cambridge* na mwengine wa *East Africa*.

Sasa wanafunzi waliofanya mtihani mwaka 1970 hawa walifanya mtihani kutoka Zanzibar tu, yaani ni mtihani wa Zanzibar, kwa bahati mbaya mtihani uliotungwa Zanzibar haukuendelea. Kwa hivyo, kuanzia mwaka 1971 hadi hivi sasa tunafanya Mtihani wa Taifa wa Tanzania.

Mhe.Spika, nashukuru kwamba leo umekuja mswada ambao pengine utaturudisha pale tulipokuwa mwaka 1970, kuwa na chombo chetu wenyewe cha mitihani. *(Makofi)*

Hivyo, ninaloliomba kwa chombo hiki kwa jina lolote litakaloitwa, ikiwa ni Baraza la Mtihani, kwa sababu waridi utakavyoliita vyovyote basi ni waridi, na wala harufu yake haibadiliki kwa jina lake. Mhe.Spika, vyeti vyake kwa maana ya shahada na stashahada watakazozitoa zitambulikane.

Kwa kweli nakumbuka miaka ya 1980 wako vijana walipelekwa na Wizara ya Afya kwenda Korea kwa ajili ya kusoma, sasa waliporudi hapa nchini petu ndani ya Zanzibar, serikali haikuwaajiri pamoja na kuwa walikuwa na vyeti ambavyo walivyovipata nje ya nchi, nadhani vyeti vile hapa nchini ilikuwa havitambuliki. Kwa hivyo, sisi tunaanzisha taasisi ambayo itakuwa inatoa vyeti, shahada pengine na stashahada, kwa maana hiyo vyeti hivi viwe vinatambulika na sio ndani ya Zanzibar tu, isipokuwa vitambulike katika Afrika ya Mashariki.
Vile vile tukikumbuka kuwa hivi sasa tunao ushindani mkubwa ndani ya Afrika ya Mashariki, na wala sio Afrika ya Mashariki tu, kwa sababu wazanzibari wengine baada ya kupata elimu yetu wanaondoka na kwenda sehemu nyengine kutumika. Hivyo, cheti chake alichokipata Zanzibar kiwe kina hadhi na kiweze kutumika popote duniani. *(Makofi)*

Mhe.Spika, hivi sasa tunao wasomi wengi tena wa daraja mbali mbali, wako watu wanaosema kwamba elimu imepanda, pia wako wanaosema kuwa elimu imeshuka.Sasa kwa vyovyote vile idadi ya wasomi imeongezeka, ikiwa elimu imepanda au imeshuka, lakini idadi ya watu waliosoma imeongezeka.

Mhe.Spika, leo Zanzibar hii mtu mwenye elimu kama yangu anahesabiwa kama anajua kusoma na kuandika tu, na wala hahesabiwi kuwa ni mtu mwenye elimu. Kwa kweli wakati wangu elimu yangu ilikuwa ni kubwa sana, lakini leo elimu yangu mimi ni ya kujua kusoma na kuandika tu.

Kwa hivyo, hapa katikati Mhe.Spika tunayo matatizo kwenye skuli zetu, ya wanafunzi ku-*overflow* katika madarasa na ndio maana watu wengi wakasema elimu kuwa imeteremka.

Mhe.Spika, nilisoma kitabu kimoja ambacho kinaitwa *Teacher in the Making*. Kitabu hiki kilikuwa kinaelezea namna ya ufundishaji katika *Primary Schools*, mtunzi wa kitabu hiki alisema darasa moja lisizidi watoto au wanafunzi 20. Kwa upande wa mwalimu katika kufundisha kwake mtawalia asizidi dakika 15, yaani afundishe baadae afanye *break* kidogo na halafu aendelee na hilo ni darasa la kwanza.

Lakini darasa la kwanza la leo, mwalimu ambaye hana wanafunzi wengi zaidi kule kwetu Pemba najua zaidi, basi anao watoto 80, mwanafunzi ambaye ukamkamatisha penseli, sidhani kama mwalimu atakuwa na uwezo wa kuwapitia wote 80 kwa ajili ya kuwasomesha.

Kutokana na hali hiyo, ndipo pale tunaposema kwamba vijana wengi wanamaliza kama vile darasa la saba (*Std. VII*) la kumi (*Form II*), basi zaidi ya kuandika jina lake hajui jengine.

Kwa hivyo, iko haja kwa kuwa tunaanzisha chombo chetu wenyewe, basi niungane na wale ambao wanaotaka tuite Baraza la Mitihani la Zanzibar, yaani tunaanzisha Baraza letu la Mitihani la Zanzibar. Mhe.Spika, Baraza hili kwa kuwa itaundwa Kamati inayohusika na Mitihani, basi kamati hii ihakikishe kwamba inatunga mitihani, pamoja na kuleta mitaala ambayo itakubalika na itakayokwenda sambamba na wakati wa leo ulivyo.

Kwa mfano, hivi sasa Zanzibar Mitaala yetu ya Darasa la Kwanza mpaka la Saba tunatunga wenyewe hapa Zanzibar, lakini baadae tunachukua mitaala kutoka Tanzania Bara. Sasa hapa itakuwa kuna sehemu fulani ya elimu ambayo tunatafautiana baina yetu. Mhe.Spika, Baraza hili litakapoundwa basi lijiamini, na lifanye kazi zake kama vile ambavyo tunategemea wazanzibari watufanyie kazi hiyo.

Mhe.Spika, kabla sijachambua kidogo kwenye vifungu hivi, sasa naomba nizungumzie kuhusu msiba wa mtihani uliotokea wa mara hii ya watoto au wanafunzi wengi kufutiwa matokeo yao.

Kwa kweli kabla ya kuingia kwenye chumba cha mtihani kuna nidhamu zake, kwa mfano mimi niko kwenye *entrance form* aliyenisimamia ni Padre, na kalamu au karatasi yangu ikidondoka, basi *just* unanyanyua mkono, anakufuata na kukuuliza baadae anakuokotea au anakwambia inama uchukue mwenyewe, yaani kuna nidhamu pamoja na mambo yake.

Sasa kwa hali yoyote ile, mwanafunzi kufanya mtihani na matokeo yake yakafutwa na *penalty* yake ikawa ni kufungwa miaka mitatu kielimu. Mhe.Spika, hapa kuna msururu wa mambo yaliyotokea, kama vile yupo aliyemsimamia, yupo *Supervisor* Mkubwa wao. Kwa hivyo, itakuwaje mwanafunzi huyo afanye udanganyifu wote huo, na kwenye chumba yumo anayemsimamia na yeye awe hana kosa lolote, lakini *finally* mkosa awe huyu mmoja tu. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nadhani hapa wahusika wanajificha wasitambulikane, na huyu wa mwisho ndiye mwenyekuadhibiwa, yaani huyu mnyonge ndiye mwenye kunyongwa. Kwa hivyo, kitendo hiki kimetuathiri wengi na si kama kuzama kwa ile meli, kwa sababu meli ilipoteza maisha ya watu. Lakini hii imepoteza baadhi ya akili za watu, yaani wametafaruki kwa tukio hili. Kwa maana hiyo, ipo haja ya makusudi kabisa na sisi kujiandaa kuingia katika chombo chetu cha kielimu, na kuweza kujitoa katika matatizo kama haya yasitokee tena mara nyengine.

Mhe.Spika, kuna sehemu kuhusu kazi za Bodi, ambapo nikitaja Bodi wenzangu wataniambia kwa nini nasema Bodi na tumesema iwe Baraza, lakini niliponukuu nilinukuu kama ni kazi za bodi. *(Makofi)*

Kifungu cha 5(c) kinaeleza hivi:-

> (c) “Kuweka utaratibu maalum wa mitihani, majaribio, upimaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyafanya kwa mujibu wa mtaala wa Zanzibar”.

Mhe.Spika, kuweka utaratibu maalum wa mitihani (*examinations*) na majaribio (*tests*) na kupima kama haijabadilika wakati nilipokuwa Mwalimu wa *Primary* ni *assessment*, yaani unamu-*assess* mwanafunzi kazi zake kwa kila wiki.

Kwa hivyo, chombo hiki kiwepo na kisimamie, na wala sina hakika kwamba mambo haya yanaendelea maskulini, kwa sababu nimehama skuli miaka mingi kidogo. Kwa mfano, wakati nilipokuwepo mimi kuna mabuku manne ya lazima ya kazi, moja lilikuwa likiitwa *daily record*, *scheme*, *assessment* na *lesson plan* na wala sina hakika kama hayo leo yapo tena.

Mhe.Spika, Kamati hii ya Mitihani ije, kama hayapo basi iyarudishe haya, na kama yapo nitumie lugha ya sasa yaboreshwe, ili tufikie katika kiwango cha elimu kinachokubalika.

Mhe.Spika, katika kufikia kiwango bora cha elimu. Kwa mfano, zamani walimu ilikuwa wakipata *training* mbali mbali, na sijui miaka hii kama Nkrumah bado ni Chuo cha Kufundisha Masomo ya Ualimu au vipi, lakini nafikiri ni Kada ya Chuo Kikuu.

Sasa mwalimu wa skuli anapomaliza *Form VI* au *Diploma* tayari anakwenda kukamata chaki kufundisha, na wala hana mafunzo ya kielimu ya kusomesha aliyoyapata. Kwa maana hiyo, Baraza hili au chombo hiki kitakachoundwa au Wizara ya Elimu yenyewe, basi ninaomba irudishe Chuo cha Kufundisha Waalimu Taaluma ya Ualimu, yaani *Teacher Training* na wala sina hakika kama ipo.

Mhe.Spika: Mhe.Mjumbe zingatia muda, ninao wachangiaji wawili ambao nataka niwamalize.

Mhe.Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante sana nitazingatia wakati.Sasa nije katika kifungu cha 6(f) Mhe.Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 6(f) kinaeleza hivi:-

> "Kualika chombo au vyombo vyovyote nje ya Zanzibar, kama itakavyoonekana inafaa, kuendesha mitihani ya kitaaluma, kiufundi, na mengineyo katika Zanzibar na kuendesha mitihani hii kwa pamoja na Bodi, na kuruzuku vyeti au stashahada kwa wanafunzi watakaofaulu katika mitihani hii".

Mhe.Spika, hapa anarudia ile ile kuwa chombo hiki kitakuwa na uwezo wa kutoa hivyo vyeti na stashahada.Je, hivi vyeti vitatambulikana? Tunaanzisha chombo tukishatweka halafu kusijekuwa na sura nyengine ikawa kama wale wanafunzi tuliowasomesha Korea na kuja hapa ikawa vyeti vyao havifai kufanyakazi Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe.Spika, kwa hayo machache kwa vile umeniambia nizingatie wakati, basi naunga mkono hoja hii.Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe.Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliopo mbele yetu.

Lakini kabla ya kuanza kuingia kwenye hoja naomba nichukue fursa hii, kwanza kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi, pili kumpa pole jirani yangu hapa Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni na mkeretekwa wa Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kupoteza Jimbo la Arumeru Mashariki.Kwa hivyo, napenda nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba kujikwaa sio kuanguka, basi ni kuelekea mbele. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe.Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hoja.Kwa kweli sababu ya kuundwa kwa chombo hiki, yaani sheria hii inaunda chombo hiki na kwanza nimpongeze Mhe.Waziri kwa kutuletea mswada huu pamoja na kwamba anaihama wizara hii, lakini sisi tunampongeza kwa kuweza kutuletea mswada huu. Mswada huu ni ukombozi kwa vijana wetu pamoja na Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe.Spika, mswada kwa kiasi kikubwa utaweza kuipunguzia kazi Wizara ya Elimu, kwa sababu kabla mswada huu hakukuwa na chombo ambacho kilikuwa kazi yake kushughulikia mambo ya mitihani, badala yake wizara ilikuwa inashughulikia mambo ya utendaji, masuala ya kiserikali pamoja na masuala ya mitihani, jambo ambalo tulikuwa tunawapa kazi kubwa. Kwa hivyo, mswada huu utasaidia sana kuipunguzia kazi Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Vile vile mswada huu nimesema utatukomboa, kwa maana utatuondoshea kile kiburi cha *NECTA*. Mhe.Spika, kabla ya kuletwa kwa mswada huu wazanzibari tulikuwa tunanyanyasika sana, kwa kweli inasikitisha sana Mhe. Spika kwamba vijana wetu zaidi ya elfu moja wamefutiwa mitihani na *NECTA*, na huu ni unyanyasaji mkubwa.

Kwa maana hiyo ni sawa na Hakimu ambaye amemuhukumu mlaji wa nyama ya ng'ombe aliyeibiwa, na huku akiachiwa muibaji, mchinjaji na mwenye bucha, hivyo mswada huu utatusaidia sana. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupitishe haraka mswada huu, kwa ajili ya kumpelekea Mhe. Rais tena tumuombe kwa heshima kabisa na unyenyekevu wa hali ya juu, ili upite kusudi vijana wetu waweze kufanya

mtihani ndani ya mwaka huu. Kwa kweli kundi la vijana elfu moja ukiwaachia tu hawasomi wala hawana kazi, yaani hawana lolote, basi matokeo yake ni kuongeza jopo la wavuta unga katika nchi hii, jambo ambalo ni hatari sana. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu mno, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe.Spika waupitishe haraka mswada huu, kusudi baadae tumuombe Mhe. Rais ausaini haraka, ili vijana wetu waweze kufanya mtihani kipindi hiki. *(Makofi)*

Mhe.Spika, Zanzibar ni nchi ni moja kati ya nchi zinazofanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba zote mbili zinasema hivyo. Kwa kweli inasikitisha sana katika kipindi chote hiki kwamba, sisi tunashindwa kuunda chombo cha kusimamia taaluma katika nchi yetu tunategemea Bara. Kwa maana hiyo, mswada huu utaipa hadhi nchi, na wala hatuna sababu ya kuukataa Mhe.Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba mswada huu tuunge mkono tena kwa haraka Mhe.Rais kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe.Spika tumuombe Mhe. Rais ausaini, ili vijana wetu waweze kukomboka.

Nikiondoka hapo sasa niondoke kwenye jina la mswada.Mhe.Spika, kwa kweli kuna usemi unaosema kwamba ‘Jicho moja halioni mwezi’. Mimi ni mmoja miongoni mwa wajumbe wa ile Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Usatawi wa Jamii, na mswada huu uliletwa kwetu na tuliachie jina lile kwamba ni Mswada utakaoshughulikia masuala ya Bodi ya Vipimo pamoja na mambo mengine.Kwa kweli hapa ndani ya Baraza naamini kwamba jicho moja halioni mwezi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, jina la mswada Mhe.Spika nakubaliana na rai aliyoitoa Mhe. Salmin Awadh Salmin ya kwamba, watu bila ya kusita wala kubabaika, hii sheria iitwe Mswada wa Sheria ya Kuunda Baraza la Mitihani Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa wa 56 wa Mswada katika kipengele cha 3(a) inasema kwamba ni chombo kinachojitegemea wenyewe chenye uwezo wa kurithiwa, Mheshimiwa naiomba sana serikali na Wizara ya Elimu utakapopitishwa mswada huu hiki chombo kiwe huru, hiki chombo kijitegemee kweli kisiwe chombo cha kisiasa wala cha kidini kiwe kinaweza kutoa na kutoa misaada kwa yoyote, kisije kikawekewa mikakati kwamba msipokee miswada kutoka OIC tusipokee kutoka wapi sijui, watafute na kupokea miswada popote kusudi kuweza kuwa huru kisiwekee mkono kiwe na maamuzi ya mwisho na kiwe huru.
Mhe. Spika, jengine niende katika kipengele cha 4(1) ukurasa wa 56 kinasema kwamba muundo wa bodi katika muundo wa bodi nilikuwa napendekeza viwekwe vipengele viwili vidogo, awemo Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi na awemo Mkurugenzi wa mafunzo ya Walimu aingizwe, kwa hivyo hapa wawe wajumbe kumi na nne. Hii bodi kazi yake kubwa ni kutathmini panapo uzoefu na kuongeza taaluma katika nchi, sasa siku moja huyu Mkurugenzi wa mafunzo ya ualimu nadhani itakuwa hatukumfanyia haki kama hatukuiongeza nguvu hii bodi.

Mhe. Spika, ninachoshauri hapa kwamba hii bodi isiwe kama NECTA kwa sababu NECTA wao wanawapima wanafunzi kupitia mitihani na majaribio, jambo ambalo kumpima mwanafunzi kwa kutumia mitihani pekee basi itakuwa hukumfanyia haki na wataalam wanasema kwamba unapompelekea mwanafunzi mtihani pengine anaweza kuwa hayuko vizuri siku ile, lakini watumie hawa utaalam wao na wanao utaalam wa kutosha Wizara ya Elimu na kwa bahati japo kama hii bodi haijaundwa lakini Mkurugenzi ameshateuliwa Maalim Ameir Suleiman Njeketu ana uwezo. Kwa vile nadhani watumie utaalam wao katika kuona ile haki kwa watoto wetu inapatikana kabisa. Kwa hivyo mbali na kutumia mitihani wawe na vipimo vyengine kusudi kujenga taaluma halisi kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 7 kifungu kidogo cha 5 naomba viingizwe vifungu viwili vidogo isomeke wajumbe saba katika kutafuta koram waliandika kwamba wajumbe sita ndio watafanya koram, lakini sasa wawe wajumbe saba ndio watafanya akidi ya kikao chochote cha bodi napendekeza hivyo.l

Mhe. Spika, kifungu cha 7(ii) kinazungumzia vikao vya bodi anasema vinaweza kufanywa pahala popote ambapo bodi inahisi panafaa, mimi nadhani bodi hii itakwenda kupitia fedha za walipa kodi

Mhe. Spika: Una dakika mbili tu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Bodi hii itakuwa inafanya kazi zake kupitia fedha za walipa kodi kama tutawaachia tu wanataka kwenda kufanya vikao Nairobi haya nendeni, kesho Uganda haya nendeni itakuwa ni uharibifu wa fedha za Serikali nadhani tutumie uzoefu wa pale NECTA wao wana jengo lao la ofisi na mambo yao yote wanafanya hapo, nadhani vile vile hawa bodi mswada huu ungewapangia kabisa kwamba vikao vya bodi viwe vinafanyika kwa muda kadhaa, angalau mara tatu kwa mwaka na vya dharura vinaweza kufanyika wakati wowote itakapobidi. Lakini tukiachia tu hivi basi hawa wanaweza kukutana mara kwa mara, wanaweza kukutana nje ya nchi vikao vyao ikabidi na sisi tupo hap waangalizi wa pesa za walipa kodi hizi tunaona tu.
Nadhani mswada huu uweke hasa kwamba vikao vya bodi vitafanyika angalau mara tatu kwa mwaka na vile vile vya dharura vikafanyika wakati wowote pale itakapoonekana inabidi, tabaan vikao hivi vifanyike aidha katika Makao Makuu ya Elimu au Ofisi ya hiyo bodi itakapokuwepo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na ataadhima mimi na wananchi wangu wa jimbo la Wawi nawaomba vile vile waheshimiwa wawakilishi tuunge mkono mswada huu mia kwa mia. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba kukushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii, lakini la pili naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza na kumshukuru Mhe. Waziri wa Elimu kwa kuleta mswada huu na maandalizi waliyofanya.

Mimi mchango wangu sio mkubwa sana katika hili lakini nilihisi kwamba ni vizuri katika kipengele kimoja hiki na mimi nichangie na nitoe mawazo yangu ili tusaidie pengine katika kufanya maamuzi, madhumuni makubwa ya kuanzisha chombo hiki ni huko tunakotoka katika mfumo wetu wa elimu na bahati nzuri humu ndani wengi ni walimu nadhani asilimia 80 pamoja na mimi mwenyewe, kabla ya kusoma sheria nilisoma cheti cha ualimu, diploma ya ualimu na nikasomesha na nawajua walimu wenzangu wengi ambao tulisoma pamoja humu ndani.

Kwa hivyo bahati nzuri unafahamika vizuri huu mswada kwa sababu wengi humu ndani ni walimu na waliokuwa sio walimu basi wanafahamu vizuri mfumo wetu na matatizo yetu ya elimu, moja katika jambo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu ni kwamba ni kuwaandaa wanafunzi wetu katika kufanyiwa tathmini ya kile ambacho wamekisoma, wanafanyiwa lakini kikubwa kinafanywa pengine baada ya hizo *assessment, test* na mengineyo. Lakini hiki chombo kinachofanya mara nyingi hakuna chombo madhubuti na hakuna chombo mahususi ambacho kiliwekwa kwa ajili ya kulisimia hili jambo ambalo ni muhimu sana katika kuendeleza elimu na katika kuendeleza wanafunzi, pengine hata matatizo ambayo leo au mwaka huu yametokea yamechangiwa kwa kiasi fulani na kukosa hayo maandalizi na usimamizi imara tokea inapoanzia mpaka inapofika kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

Kwa hivyo nadhani huu mswada tukiangalia hiki chombo ambacho kinaanzishwa basi kitasaidia sana katika kusimamia suala la tathmini na vipimo vya wanafunzi na hao wanaopima vile vile kila siku takriban, ni tofauti sasa hivi ambapo una chombo ambacho kazi yake ni kuandaa ligi au kuandaa mechi, lakini hii ni kuwaandaa watu ili wakifika kwenye mechi basi waweze kushindana na kuweza kufanya vizuri katika mechi hizo, ndio madhumuni yake kwamba hiki hakitakuwa sawa sawa pengine na baraza la mitihani ambalo mimi pengine itakuwa sio mfano mzuri lakini nadhani ndio sahihi kuufananisha, maana yake inakuwa kama vile kazi pengine nina mtoto wa kike wa nje ya ndoa. Maana mpaka ukimuona kadhi basi ujue pana harusi na ikashakupita harusi hapiti tena mpaka harusi nyengine ndio atakuja, sasa ndio kama Baraza la mitihani lilivyo sasa hivi kwamba mpaka ukiliona limeshughulika kutoa fomu ujue kuna mtihani na ukimaliza mtihani hulioni tena baraza la mitihani mpaka mtihani mwengine vile vile.

Sasa hiki chombo chetu ni tofauti na hicho hiki kazi yake itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii tathmini inafanywa kila siku viwango, maelekezo, taaluma na kuweka vigezo vile vile, kwa hivyo hiki chombo kitafanya kazi zaidi ya Baraza la mitihani hilo ni moja na ambalo naamini wenzangu humu ndani kwa sababu na wao ni walimu wengi naamini hilo watakuwa wamelifahamu, kama mswada tumeusoma vizuri sana kazi za hii bodi ambayo inaanzishwa.

Lakini hoja ya pili iliyokuja ni kuhusiana na jina Mhe. Spika, kazi za chombo wakati mwengine hazitokani pengine na jina lake, maana mnawezekana mnafanya kazi za namna moja lakini majina mkatafautiana hili ni jambo la kawaida lipo, ukija mfano wakuu wa Mikoa hapa kwetu tunaita Wakuu wa Mikoa wenzetu wanaita P*rovincial commissioner,* wengine wanaita *governor* hata Bunge sisi tunaita Baraza la Wawakilishi, lakini haina maana kwamba nguvu yake ni ndogo kuliko Bunge inategemea tu kwa hicho chombo katika kufanya maamuzi ya kazi zake, lakini kuna majina mengi kuna *majlis tashria* kuna *legico* Ilikuwepo wengine Duma wengine *lock saber* sasa haya ni majina lakini cha msingi wanafanya kazi gani.

Sasa hapa mimi Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana tuzingatie katika hilo kwamba jina sio linalotoa mamlaka wala tofutti ya jina haina maana kwamba kile unachokusidia kifanyike hakitofanyika kwa sababu Baraza hili kwa sababu haliitwi Bunge tungeng'ang'ania libadilishwe jina liitwe bunge ndio lipitishe sheria itakuwa sio sawa, linapitisha sheria linafanya kazi zote za bunge na jina lake hili hili la Baraza la Wawakilishi.

Sasa mimi nadhani hilo ni vizuri tukalizingatia lakini nalisemea hili kwa sababu nina wasi wasi pengine ni vizuri sisi humu ndani ni watumishi wa watu , sasa tunaowatumikia ni vizuri wakatufahamu tunafanya nini katika jambo hili tusiwape tama, tusiwaeleze jambo ambalo kuwa halitofanyika kwa sababu tu ya kubadilisha jina la sheria hii, tujiulize kwamba je chombo hiki kikibadilishwa jina na kuitwa Baraza la Mitihani la Zanzibar ndio litaweza kufanya hiyo kazi ambayo baraza la Mitihani la taifa inafanya.

Mimi nadhani hilo ndio jambo la msingi kwamba hilo ndio litakalotokea maana wananchi hilo kama ni kusubiri nadhani wanasubiri hilo Mhe. Spika, kama je tukiwapa tama kwamba aa kwa kukiita chombo hiki Baraza la Mitihani la Zanzibar ina maana tumeshatatua lile tatizo ambalo limetokea, tuwe wakweli tuwaambie watu wetu wafahamu watuelewe tunafanya kitu gani. Kwa kufanya hivyo ndio tutakuwa tunatatua hilo tatizo tujiulize na tueleze ukweli, mimi ninachosema ni kwamba kwa kufanya hivyo tutakuwa bado hatujatatua tatizo ukweli ni mchungu, tatizo lililotokea linauma na limetugusa sote maana na sisi pita kila mtu ana ndugu yake ana mwanawe na jamaa yake au jirani yake, lakini hapa tunapofanya maamuzi makubwa kwa niaba ya wananchi tuseme kile ambacho kweli tunataka kukifanya kwa kubadili jina chombo hiki bado tutakuwa hatujatatua hilo tatizo ambalo limejitokeza.

Kwa sababu tukubali kwamba katika katiba ya Muungano kwanza kilichokuwa tumekubaliana kimazingira ni mambo ya muungano ni mambo mawili elimu ya juu chini ya *iterm ya 14* ya Katiba katika jaduweli la kwanza. Lakini *iterm ya* pili ni Baraza la Mitihani la Taifa na mimi nitawaomba wenzangu labda wanisaidie kulisoma, lakini lilivyoandikwa hapa limeandikwa. "*Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za baraza hilo".* Katiba hii si yangu, katiba hii sikushiriki kuitunga lakini katiba hii ni katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapa wenzetu walisema vizuri Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Salmin Awadh Salmin na wengine kwamba tumefundishwa hizi katiba awe ndio mpenzi wetu, mpaka tukafika kuambiwa kama kulala nazo basi tulale nazo sijui kama hatutoleta ugomvi nyumbani lakini ndio hayo tuliyosema kwamba hivyo ndio katiba inavyosema.

Sisi Serikali tumekaa na tukalizingatia tukasema aa kwa hilo uko mbele inafaa tulifanyie kazi kwanza vizuri tufike pahala tujiridhishe, huko tunakosema kwamba tunaweza kufika basi tunaweza tukafika lakini ni lazima hicho kitu tujiridhishe, sasa kama kuna mtu hapa anasema aaa kwa kubadili hichi chombo basi hizi kadhi au hii *iterm ya 16* kwenye katiba ya Muungano ndio tutakuwa nayo tunairekebisha basi atwambie hivyo tuelewe na tufahamu na tufahamu hoja yake ya kutueleza hivyo. Lakini hoja ya serikali tunavyosema ni kwamba hichi chombo tunaunda ni mbegu na kama ni mbegu inaweza kumea, ikaota ikafika ikakua na ikafika tunakotaka, lakini kwa sasa hivi tutakuwa hatusemi kweli kwa kusema kwamba kwa kuliita chombo hichi bodi kwamba ni Baraza la Mitihani la Zanzibar basi itakuwa moja kwa moja inachukua nafasi za kazi za Baraza la Mitihani mimi nadhani itakuwa sio sahihi.

Mhe. Spika, ni vizuri na nadhani tunapofanya haya maamuzi watu wanatusikia ni vizuri wajue kwamba tunafanya maamuzi kwa kuwafahamu kwa kuelewa, kama shida yetu ni nywele haina haja ya kuvaa wigi kwa sasa hivi tusubiri ziote tunazo lakini tumezikata wenyewe, sasa haina haja ya kuvaa wigi tukasema na sisi tayari nywele tunazo, tusubiri nywele zetu ziote Mhe. Spika, ili watu watakapotuona tuna nywele wajue kama hizi ni nywele wasije kuzivuta zikavuka wakaona kumbe ni kipara.

Sasa mimi ushauri wangu ni huo tu kwambwa katika hili mimi nadhani twende na kile ambacho serikali imekusudia kukifanya kimechangia na sote tumeona umuhimu wake, kama tunataka tufike huko tunaweza kufika uamuzi huo ni wetu lakini tutakapofika basi tuwe tumefika katika misingi ambayo imekubalika kisheria, misingi ambayo inakubalika kikatiba na mimi nawaomba waheshimiwa Wajumbe kwa sababu suala hili tusitafute kuwatia watoto wetu na ndugu zetu katika mgogoro ambao utakapowafika pia tutakuja kushindwa kuwasaidia. Kwa sababu suala la kwamba mtu una chombo kimefanya mtihani akatokea mtu akaje kuchalenji mtu tayari ameshapoteza gharama, mtu tayari ameshapoteza muda wake halafu anaambiwa hichi sio cheti halali kwa sababu hiyo mamlaka iliyofanyisha mtihani haina mamlaka ya kisheria, tutakuja kufika pahala tutawatia ndugu zetu na tutawatoa kwenye jivu na kuwatia kwenye moto.

Mhe. Spika, tutakapofanya maamuzi hayo tufanye maamuzi ya uhakika, tufanye maamuzi ambayo kweli wakati wake wa kuyafanyia maamuzi umefika na tuyafanyie kazi wala tusiyafanyie kwa kubadilisha jina tu la sheria hii, lakini ni kitu ambacho mimi nadhani ni wazo zuri lakini linahitajika kufanyiwa utafiti, linahitajika kufanyiwa matayarisho. Mimi nadhani kitu cha muhimu kwa sasa tupande hii mbegu na tusubiri imee izae matuna yale ambayo tunataka yazaliwe.

Mhe. Spika, inawezekana kuna wengine ambao tunatofautiana kwa hoja lakini nadhani wanasema ushujaa sio kusema tu, lakini ushujaa ni kusikiliza pia kwa hivyo nadhani hilo linahitajika ili tuweze kufanya maamuzi ambayo ni sahihi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia na naomba wenzangu wote tuunge mkono na tupitishe mswada huu ahsate sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri tumemsikia Mwanasheria Mkuu nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa mchango wake vile vile, sasa baada ya hayo naomba niakhirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 4/4/2012 Saa 3.00 za asubuhi.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 04/04/2012)